**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA TANZANIA**




# MIRATHI

## NCHINI TANZANIA

# MIRATHI
# NCHINI TANZANIA

**"MWONGOZO KUHUSU MIRATHI, WOSIA NA TARATIBU ZA KIMAHAKAMA TANZANIA"**




***Maisha ni zawadi kutoka kwa Mungu Muumba wetu, zawadi hii ya maisha sio ya milele kuna siku nitakufa. Kifo kinapotokea pamoja na mambo mengine kuna maswali mawili ya msingi huzaliwa; (i) Wapi inakwenda roho yangu? na (ii) Mali na ndugu zangu wanabaki vipi? Kitabu hiki kinajikita kwenye kipengele cha pili tu kwa kuwa kipengele cha kwanza kina watu maalumu wa kukiongelea.***

SIMON O. SWAI

# KUJITOLEA

Utukufu, sifa na shukrani zinarudi kwa Mungu Muumba wetu ambaye amenipa nguvu, afya, utulivu na amani hata kuweza kuandika kitabu hiki. Kwa ajili hiyo, nakitoa kitabu hiki kwa watu wake kikasaidie kutoa mwongozo katika masuala ya mirathi. Kitabu hiki kikasaidie kuzuia migogoro mingi ya kifamilia na kijamii inayotokana na kukosa uelewa wa masuala ya mirathi. Ni imani yangu kuwa kwa kusoma na kuelewa na kwa kuwaelimisha wengine yaliyomo katika kitabu hiki suala la kifo litabaki kuwa ibada pekee. Halitazaa chuki, uhasama na uadui kwa wale walioachwa duniani.

Pia natoa kitabu hiki kwa watoto wangu wapendwa Adriel, Adriella na Ariel mkakue katika hekima na kimo mkimpendeza Mungu na wanadamu. Na kwako Rachel, mke na rafiki yangu. Asante kwa kunipa moyo na kunivumilia nilipoandika kitabu hiki hata muda wa usiku sana.

Mungu uliniweka Mahakamani kama mtumishi wa umma kwa mapenzi na makusudi yako. Nitaendelea kutekeleza majukumu yangu kwa dhati, uweledi na uadilifu hadi hapo itakapokupendeza vinginevyo. Hivyo kitabu hiki ni kwa ajili ya Mahakama na kikatumike kwa manufaa ya taasisi hii na Taifa kwa ujumla wake.

# DIBAJI

Mirathi na taratibu zake ni eneo nyeti kwa sababu linawahusu wafu na walio hai. Licha ya kuwepo sheria zinazosimania eneo hili, ufafanuzi wa sheria hizo na maelekezo mahususi ya Majaji wa Mahakama ya Rufani na Mahakama Kuu kupitia hukumu mbalimbali, bado usimamizi wa mirathi ni changamoto kubwa katika jamii yetu. Wajane, na Watoto hasa waliozaliwa nje ya ndoa bado wanapitia changamoto nyingi kufikia haki zao kupitia mirathi. Kitabu hiki kinajaribu kuelezea kwa lugha nyepesi taratibu za kuzingatia ili kifo kisiwe chanzo cha migogoro katika jamii zetu. Kwa muktadha huo, mwandishi amesisitiza umuhimu wa kuandika wosia na utaratibu wa kufuata. Ameelezea pia, kwa ufasaha mkubwa, taratibu za kimahakama za usimamizi wa mirathi tangu Mahakama za Mwanzo hadi Mahakama ya Rufani. Ni matumaini yangu, kama yalivyo matumaini ya mwandishi, kwamba kitabu hiki ni kwa manufaa na kinaweza kusomwa na kueleweka kwa kila mwanajamii. Chafaa pia wa matumizi ya Wanasheria wanaosimamia mashauri ya mirathi, Mahakimu, Majaji na kufundishia vyuoni kama kitabu cha rejea.

Mwandishi wa Kitabu aliniomba ushauri kuhusu dhamira yake ya kuandika kitabu hiki mwaka 2018. Kwa kutambua uwezo wake nilimkubalia na hata kuandika dibaji hii. Kwa kujitolea kitabu hiki kwa matumizi ya taasisi anayoitumikia anaonyesha unyenyekevu, uaminifu na uadilifu wa kiutumishi. Kujitolea huku ni kwa kipekee na mfano wa kuigwa na vijana wengine na watumishi wa umma kwa ujumla.

Nampongeza sana *Ndugu* Simon Swai kwa hiki alichoifanyia Mahakama ya Tanzania na umma kwa ujumla. Mchango wake utakumbukwa na kizazi hiki na vijavyo kadri tunavyoendelea kujenga mfumo wa utoaji haki sawa hapa nchini.

**Ilvin Claud Mugeta**
**Jaji**
**Mahakama Kuu Kigoma**
**12/3/2021**



# SHUKRANI NA UTAMBUZI

Shukrani za kipekee zinaenda kwa Mhe. Jaji Ilvin Mugeta. Asante kwa kupokea wazo langu la kuandika kitabu hiki, kunishauri namna ya kwenda na kuandika Dibaji. Nawashukuru wazazi na walezi wangu Bw. & Bi. Devangwa Mmari kwa ushauri na miongozo yote waliyokuwa wakinipa katika maisha hadi 24/6/2019 mlipotwaliwa na Mungu. Mbegu mliyopanda kwenye maisha yangu itastawi na kuzaa kwa ustawi wa taifa letu.

Natoa shukrani zangu na utambuzi wa mchango mkubwa kwa uongozi wa Mahakama hasa Mhe. Jaji Kiongozi Feleshi, J (Ph. D), Mhe. Msajili Mkuu W. Chuma na Mtendaji wa Mahakama Kuu (Ndugu Leonard Magacha) kwa kuweka mazingira mazuri ya kazi na kwa kuruhusu kupokea mawazo ya watumishi mbalimbali. Uongozi wenu umenipa hamasa kubwa ya kuandika kitabu hiki.

Nawashukuru sana watumishi wenzangu tulioanza kama Wasaidizi wa Sheria wa Majaji na sasa ni Mahakimu Wakazi kwa msaada wao na ushauri wenye thamani kubwa katika kuandika kitabu hiki. Kila wazo mlilotoa limeenda moja kwa moja kwa Watanzania kupitia kitabu hiki.

# YALIYOMO


KUJITOLEA ..... i
DIBAJI ..... ii
SHUKRANI NA UTAMBUZI ..... iii
ORODHA YA SHERIA ..... viii
ORODHA YA MASHAURI ..... ix
**SURA YA KWANZA ..... 1**
**KIFO NA TARATIBU ZA KISHERIA ..... 1**
1. Utangulizi ..... 1
1.2 Kabidhi Wasii Mkuu ..... 1
1.3 Utaratibu wa Kusajili Kifo ..... 2
1.3.1 Taratibu za kupata cheti cha kifo ..... 2
**SURA YA PILI ..... 3**
**HAKI YA KURITHI NA MAMLAKA YA KUSIKILIZA MASHAURI YA MIRATHI ..... 3**
2. Mahakama kwa Ujumla ..... 3
2.1 Haki ya Kurithi ..... 3
2.2 Sheria Zinazotoa Haki ya Kurithi Tanzania ..... 4
2.2.1 The Indian Succession Act 1865 ..... 5
2.2.2 The Hindu Wills Act 1870 ..... 5
2.2.3 Sheria ya Mila ..... 5
3.2.3.1 Mila na Dhana ya Ubaguzi wa Wanawake ..... 7
2.2.4.1 Mambo ya Kuzingatia katika Mirathi ya Kiislamu ..... 11
2.2.6 Sheria ya Mtoto ..... 12
2.3 Taratibu za Kufikia Haki ya Kurithi ..... 12
2.4 Uchaguzi wa Sheria ya Kutumia ..... 13
2.4.1 Uchaguzi Kulingana na Maisha ya Marehemu ..... 13
2.4.2 Uchaguzi Kulingana na Matakwa ya Marehemu ..... 15
2.5 Umuhimu wa Kuchagua Sheria ..... 18
2.6 Mamlaka ya Kusikiliza Mashauri ya Mirathi ..... 19
2.6.1 Mahakama ya Mwanzo ..... 19
2.6.2 Mahakama ya Wilaya ..... 20
2.6.3 Mahakama Kuu ..... 21





2.6.3.1 Kusajili (re-seal) Mirathi Iliyosikilizwa Nje ya Nchi ..... 21
2.7 Mamlaka ya Mahakama ya Mwanzo kwenye Mashauri ya Mirathi ..... 25
2.7.1 Muda wa Kufungua Shauri la Mirathi Mahakama ya Mwanzo ..... 27
2.7.1.1 Athari zitokanazo na kuchelewa kufungua shauri la Mirathi ..... 29
2.8 Utaratibu wa Kufungua Shauri la Mirathi Mahakama ya Mwanzo ..... 30
2.9 Nyaraka za Kuambatanisha kwenye Maombi ya Usimamizi ..... wa Mirathi ..... 31
2.10 Vigezo vya Kuzingatia kwa Mleta Maombi ..... 32
2.11 Matangazo ya Mashauri ya Mirathi ..... 34
2.12 Taratibu Endapo Wahusika Hawajafika Mahakamani ..... 37
2.13 Usikilizaji wa Maombi ya Usimamizi wa Mirathi au Kuthibitishwa kuwa Mtekeleza Wosia ..... 38
2.14 Pingamizi katika Shauri la Mirathi ..... 38
2.15 Aina Za Mapingamizi ..... 39
2.15.1 Pingamizi Dhidi ya Maombi/ Mwombaji ..... 39
2.15.2 Pingamizi la Orodha ya Mali ..... 40
2.15.3 Pingamizi la Mgawanyo wa Mali ..... 41
2.16 Kuteua Msimamizi wa Mirathi au Kumthibitisha Mtekelezaji Wosia ..... 44
2.17 Mirathi pasipo Wosia ..... 45
2.18 Rufaa Kutoka Mahakama za Mwanzo ..... 46
2.18.4 Muda na Utaratibu wa Kukata Rufani ..... 46
2.18.5 Nini Kifanyike kama upo nje ya Muda? ..... 47
2.19 Taratibu za Uteuzi Mahakama ya Wilaya na Mahakama Kuu ..... 49
2.19.6 Uteuzi kwa Lakiri ya Mahakama na Dhamana ..... 50
2.20 Kabidhi Wasii Mkuu Mkuu wa Serikali ..... 50
2.20.1 Taratibu, Mahitaji au Mazingira ya Kabidhi Wasii Mkuu Kusimamia Mirathi ..... 52
2.20.1.1 Kwa Maombi ..... 52
2.20.1.2 Kuteuliwa moja kwa moja na Mahakama ..... 53
2.20.2 Mamlaka ya Mahakama Kumteua Kabidhi Wasii Mkuu ..... 53
2.21 Nguvu ya Msimamizi wa Mirathi ..... 54
2.22 Kutenguliwa kwa Msimamizi wa Mirathi ..... 55
2.23 Mahakama ya Rufani ..... 56
2.24 Wajibu wa Mahakama Katika Kumthibitisha Mtekelezaji Wosia au Kuteua Msimamizi wa Mirathi ..... 60
2.25 Miongozo ya Kimahakama ..... 61

2.25.1 Waraka wa Jaji Kiongozi Na. 4/2005 Kuhusu Mashauri ya Mirathi ... 61

2.25.2 Waraka wa Jaji Kiongozi Na. 1/2007 Kuhusu Kesi za Madai: Amri za Muda, Kesi za Kiuchumi, Mirathi na zile za Watumishi Serikalini ... 62

2.25.3 Chief Justice's Circular No. 1/2018 for District Delegates ... 62

2.25.4 Waraka wa Msajili Mkuu Na. 1/2019 Kuhusu Ufungaji wa Mirathi na Utumaji wa Taarifa za Mashauri ... 62

**SURA YA TATU ... 63**

**KUTUNZA MALI ZAKO NA WALE UWAPENDAO HATA BAADA YA KIFO ... 63**

3. Wosia ... 63
3.1 Faida ya Wosia ... 64
3.2 Nani Anaweza Kutoa Wosia? ... 64
3.3 Aina za Wosia ... 65
3.3.1 Wosia wa Mdomo ... 65
3.3.2 Wosia wa Maandishi ... 66
3.4 Hatua za Kuchukua Pale Mashahidi wa Wosia wa Mdomo Wanapofariki kabla ya Aliyetoa Wosia ... 66
3.5 Namna ya Kuandaa Wosia wa Maandishi ... 67
3.6 Mfano wa Wosia wa Kuandika ... 67
3.7 Namna ya Kutunza Wosia wa Kuandika ... 69
3.8 Namna ya Kubadili/ Kurekebisha Wosia Wako ... 69
3.9 Pale Inapotokea Mabadiliko ya Wosia Yanajulikana Baada ya Mahakama Kumthibitisha Msimamizi kwa Kuzingatia Wosia wa Zamani ... 70
3.10 Idadi ya Wosia Unaoweza Kuacha au Kuandika ... 72
3.11 Jinsi ya Kurithisha kwa Wosia ... 72
3.12 Mrithi Kunyimwa Urithi na Mwenye Kutoa Wosia ... 73

**SURA YA NNE ... 75**

**ANAYESTAHILI KUWA MSIMAMIZI WA MIRATHI ... 75**

4. Utangulizi ... 75
4.6 Nani awe Msimamizi wa Mali za Marehemu ... 75
4.7 Haki za Warithi au Wanufaika wa Mirathi ... 76
4.8 Maombi ya Kupewa Usimamizi wa Muda wa Mirathi ... 78
4.9 Mwangalizi wa Mali za Marehemu kabla ya Uteuzi ... 79





**SURA YA TANO ... 83**

**WAJIBU WA MSIMAMIZI WA MIRATHI NA TARATIBU ZA KISHERIA PALE ANAPOSHINDWA KUKAMILISHA WAJIBU WAKE ... 83**

5. Utangulizi. ... 83
5.1 Majukumu ya Msimamizi wa Mirathi na Mtekeleza Wosia ... 83
5.2 Hatua za Kuchukua Pale Msimamizi Anapokosea Kutekeleza Wajibu Wake ... 84
5.3 Utaratibu wa Usimamizi Pale Aliyeteuliwa au Kuthibitishwa na Mahakama Anapofariki Kabla ya Kumaliza Kazi Yake ... 86
5.4 Utaratibu Pale Mtekeleza Wosia Anafariki ... 88
5.4.1 Kabla ya Aliyetoa Wosia ... 88
5.4.2 Kama Mtekeleza Wosia anafariki kwa Pamoja na Aliyetoa Wosia ... 89

**SURA YA SITA ... 90**

**ULIPAJI WA FEDHA ZA MIRATHI KUPITIA MAHAKAMA ... 90**

6. Utangulizi ... 90
6.1 Utaratibu wa Malipo ... 91
6.2 Mambo ya Kuzingatia ... 92

**SURA YA SABA ... 93**

**MAPENDEKEZO NA HITIMISHO ... 93**

7. Mapendekezo ... 93
7.1 Elimu Ya Mirathi kwa njia mbalimbali ... 93
7.1.1 Elimu ya Mirathi Shule za Sekondari ... 93
7.1.2 Dawati la Elimu ya Mirathi ngazi ya Mahakama ya Mwanzo na Serikali ya Mtaa ... 94
7.1.3 Elimu kupitia vipindi vya Radio na Runinga ... 95
7.1.4 Elimu ya Mirathi kupitia Mitandao ya Kijamii ... 96
7.2 Mafunzo ya Mara kwa Mara kwa Majaji na Mahakimu juu ya Mirathi ... 96
7.3 Matangazo ya Vifo ... 97
7.4 Ulipaji wa Fedha za Mirathi kupitia Akaunti ya Mahakama ... 97

**Hitimisho ... 98**

**VIELELEZO ... 101**

# ORODHA YA SHERIA

- The Customary Law (Declaration) (No.4) Order of 1963, GN No. 219 of 1967.
- The Hindu Wills Act 1870.
- The Indian Succession Act 1865.
- The Islamic Law (Restatement) Act, Cap 375 R. E 2002.
- The Law of Limitation Act, Cap. 89 RE 2002.
- The Law of the Child Act, No. 21 of 2009.
- The Magistrates' Courts Act, Cap. 11 RE 2002.
- The Primary Courts (Administration of Estates) Rules, GN. 49 of 1971.
- The Probate and Administration of Estates Act, Cap. 352 RE 2002.
- The Probate Rules, GN. 369 of 1963.
- Judicature and Application of Laws Act, Cap. 358 RE 2002.
- The Succession (Non-Christian Asiatics) Act, Cap. 28 RE 2002.



# ORODHA YA MASHAURI

- Angela Philemon Ngunge vs Philemon Ngunge Probate and Administration Appeal No.2 of 2010 High Court at Mbinga (unreported).
- Angelo Bisiki vs Antonia Bisiki & Others (1989) TLR 225 HC.
- Elizabeth Mohamed vs Adolf John Magesa Administration Appeal No.14 of 2011 (unreported) Mwanza.
- Ibrahim Kusaga Vs Emmanuel Mweta (1996) TLR 26.
- Judith Patrick Kyamba vs Tunsume Mwimbe & 3 Others, Probate and Administration Cause No. 50 of 2016 HC at Dar es salaam
- Maagwi Kimito vs Gibeno Werema [1985] T.L.R 132
- Malietha Gabo vs Asamu Mtengu Misc. Land Appeal No. 21 of 2020 HC Kigoma (Unreported)
- Masudi Ally vs Chiku Masudi (1992) TLR 50 HC.
- Mgeni Seif vs Mohamed Yahaya Halifani Civil Application No 1 of 2009 CA (unreported).
- Mwaka Musa vs Simon Obedi Simchimba Civil Appeal No. 45 of 1994 CA at Dar es salaam (unreported).
- Rashid Hassan vs Mrisho Juma (1998) TLR 134.
- Shomari Abdalha Vs Abdalha Hussen and another (1991) TLR 135.
- Sofia Said & Yusufu Mohamed Musa vs Awadhi Mohamed Abeid & 3 others. (1992) TLR 20 (CA).
- Violet Ishengoma Kahangwa & Jovin Mutabuzi vs Administrator General & Mrs Eudokia Kahangwa (1990) TLR 72 (CA).

# SURA YA KWANZA

# KIFO NA TARATIBU ZA KISHERIA

## 1. Utangulizi

Kifo kinapotokea wanandugu wanatakiwa kusajili kifo hicho ndani ya siku thelathini (30) tangu tarehe ya kifo kilipotokea. Usajili wa kifo unafanyika kwenye Ofisi ya Usajili wa Vizazi na Vifo ambayo iko kwenye ofisi ya Mkuu wa Wilaya au kwenye ofisi za Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini. Usajili wa kifo huthibitishwa kwa cheti cha kifo ambacho ni nyaraka muhimu Mahakamani katika kuomba usimamizi wa mirathi au kuthibitiswa kwa mtekeleza wosia pale ambapo marehemu ameacha wosia.

### 1.2 Kabidhi Wasii Mkuu

Kabidhi Wasii Mkuu *(Administrator General)* anateuliwa na kifungu cha 4 cha sheria ya Kabidhi Wasii Mkuu (Nguvu na Mamlaka), (Sura ya 27 marejeo ya 2019)[1]. Pamoja na majukumu mengine Kabidhi Wasii Mkuu ni kiongozi wa juu wa Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini (RITA)[2] Sheria hii inaelekeza juu ya umuhimu na kuweka ulazima wa usajili wa matukio muhimu ya vizazi na vifo. Ni lazima kwa kila mtu anayezaliwa na anayefariki kusajiliwa kwa mujibu wa sheria.

Pamoja na kuwa miundombinu ya usajili iliyopo si rafiki katika kuhakikisha kuwa kila tukio linasajiliwa, Serikali imejitahidi kusogeza huduma hii muhimu karibu na wananchi ili kupunguza gharama katika upatikanaji wa huduma za usajili na kuhakikisha taarifa na takwimu za matukio ya vifo zinapatikana kwa wakati. Ni sera ya Serikali kuwa usajili na utoaji vyeti vya vifo unapatikana ndani ya siku 30.

1 Registration, Insolvency and Trusteeship Agency.
2 The Births and Deaths Registration Act, Cap 108 R.E 2002.

### 1.3 Utaratibu wa Kusajili Kifo

Iwapo kifo kimetokea katika kituo cha tiba (hospitalini, kituo cha afya au zahanati) mhusika wa kituo cha tiba (ambaye ndiye Msajili Msaidizi) anawajibika kuhakikisha taarifa za usajili wa kifo zimejazwa kwenye fomu ya usajili na kujaza cheti cha kifo. Kwa upande mwingine kifo kikitokea nyumbani au mahali pengine mwombaji atoe taarifa ya tukio la kifo kwa Mtendaji wa Kijiji au Mtaa ambaye atajaza fomu maalum ya taarifa *(notification form)* na kuwasilisha kwa Afisa Mtendaji wa Kata. Mtendaji wa Kata ndiye atakayehusika kutoa cheti cha kifo kilicho andikwa kwa mkono kama uthibitisho wa Usajili wa kifo kilichotokea katika kata yake. Kwa hali yoyote ile ni muhimu kupata kibali cha mazishi kutoka kwa Ofisa Mtendaji wa Kijiji/Mtaa, au kwa Msajili wa Wilaya.

Kimsingi jukumu la kusajili vifo liko kwa daktari aliyethibitisha kifo, au ndugu wa karibu wa marehemu ambao walikuwepo wakati wa kifo chake au walikuwepo wakati wa mwisho wa ugonjwa wake, au mmiliki wa nyumba, au mkazi wa nyumba, au mtu yeyote aliyechukua jukumu la kumzika marehemu huyo.

#### 1.3.1 Taratibu za kupata cheti cha kifo

Ndugu anayefuatilia au muhusika mwingine yeyote anatakiwa kuwasilisha kibali cha mazishi kwa Msajili wa wilaya ambaye kifo kimetokea katika eneo lake la utendaji. Cheti hutolewa baada ya malipo ya ada iliyowekwa. Cheti ndio uthibitisho wa kisheria kuwa kweli kifo cha fulani kimetokea. Cheti hiki ndio nyaraka muhimu sana katika kufungua shauri la mirathi Mahakamani.



# SURA YA PILI

# HAKI YA KURITHI NA MAMLAKA YA KUSIKILIZA MASHAURI YA MIRATHI

## 2. Mahakama kwa Ujumla

Mahakama ndio chombo pekee chenye mamlaka ya kutoa haki nchini Tanzania. Mamlaka haya yanatokana na Ibara ya 107A (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977. Kwa wepesi wa uelewa Ibara husika inasomeka kama ifuatavyo: -

*107A. (1) Mamlaka yenye kauli ya mwisho ya utoaji haki katika Jamhuri ya Muungano itakuwa ni Mahakama.*

Kwa msingi huo, mashauri yanayohusu mirathi, wosia na kusimamia mali zinazoachwa na marehemu ni jukumu la Mahakama kama inavyofanya katika aina nyingine za mashauri kama vile ya jinai na madai. Katika kutekeleza utoaji haki katika mashauri yanayohusu mirathi, usimamizi wake na hata mgawanyo wa mali za marehemu, Mahakama inaongozwa na sheria za nchi zilizotungwa na bunge kwa ajili ya madhumuni hayo. Hata hivyo mila, desturi, utamaduni, na dini ya marehemu huzingatiwa pia wakati wa mirathi kulingana na aina ya maisha ya marehemu enzi za uhai wake.

### 2.1 Haki ya Kurithi

Haki ya kurithi ndio kiini cha hatua mbali mbali ambazo mwombaji au mrithi huzipitia ili kuhakikisha haki hiyo inapatikana. Haki ya kurithi inashabiiana na Ibara ya 24(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungao wa Tanzania ambayo inajenga dhana ya haki ya kumiliki mali. Mmiliki anapofariki, lazima apatikane mwingine wa kumikiki

mali hiyo. Upatikanaji wa haki ya kurithi unachagizwa na hatua za kuchagua msimamizi wa mirathi au mtekeleza wosia ambazo ni daraja tu la kufikia haki ya kurithi. Ugomvi na kutokuelewana kwa wanandugu au wanufaika wa mirathi huchochewa na kiu ya kulinda haki yao ya kurithi. Endapo marehemu ameacha wosia, warithi watapata haki yao ya kurithi kwa mujibu wa wosia na pale ambapo hakuna wosia basi kuna sheria mahususi ambazo zinatoa haki ya kurithi kulingana na mila, desturi na dini. Hivyo Mahakama hutumia sheria hizo zinazotoa haki ya kurithi kwa mujibu wa maisha ya marehemu kwa kuzingatia dini yake na mila.

## 2.2 Sheria Zinazotoa Haki ya Kurithi Tanzania

Haki ya kurithi nchini Tanzania inatamkwa na sheria kadhaa kama ifuatavyo hapa chini kutokana na asili ya mtu au imani yake ya dini. Sheria hizo ni kama zifuatavyo: -

i. The Indian Succession Act 1865[3];
ii. Sheria ya Mila[4];
iii. Sheria ya Dini ya Kiislamu[5];
iv. The Hindu Wills Act 1870;
v. The Succession (Non-Christian Asiatics) Act[6]; na
vi. The Law of the Child Act[7].

Sheria Na. I na Na. IV hapo juu zinatumika nchini kwa kupitia nyongeza ya II ya Sheria ya Judicature and Application of Laws Act[8] (JALA) hivyo ni sehemu ya sheria za nchi.

3 Sheria ya Urithi ya India.
4 The Customary Law (Declaration) (No.4) Order of 1963 GN No. 219 of 1967 read together with GN No. 436 of 1967.
5 The Islamic Law (Restatement) Act, Cap 375 R. E 2002.
6 Cap. 28 R.E 2002.
7 No. 21 of 2009.
8 Cap. 358 R.E 2002 (JALA).



### 2.2.1 The Indian Succession Act 1865

Sheria hii imerasimishwa kutoka sheria za India na chimbuko lake ni sheria za Uingereza ambazo zilitungwa mahususi kwa jamii ya waingereza nchini India ambao ni wakristo pekee dhidi ya waislamu na wahindu. Sheria hii inatumika kwenye mirathi yenye wosia na ile isiyo na wosia. Sehemu ya V ya sheria hii inaelezea juu ya haki ya kurithi ikijumuisha wajane, wagane na wanufaika wengine isipokuwa watoto wa nje ya ndoa.

### 2.2.2 The Hindu Wills Act 1870

Sheria hii inaongelea haki ya urithi kwa watu wenye asili ya Hindu ambao sio wakristo wala waislamu na pia jamii ambayo sheria ya *Indian Succession Act* haitumiki. Kimsingi sheria hii inaongelea juu ya kutengeneza wosia na taratibu za kupima uhalali wa wosia kwa watu ambao wanafuata sheria hii.

### 2.2.3 Sheria ya Mila

Sheria ya Mila yaani *The Customary Law (Declaration) (No.4) Order of 1963*[9], ikisomwa pamoja na GN No. 436 of 1967 imetokana na mamlaka ya kifungu cha 12(3) cha JALA. Katika tamko/sheria hii haki ya kurithi inaongelewa kwenye aya ya 30 ya nyongeza ya II ambapo haki ya kurithi hutegemea jinsia na umri. Kwa ujumla wake wanawake hawapewi haki sawa na wanaume ambapo kanuni ya 5 inawaweka wanawake daraja la chini pamoja na watoto.

Kimsingi sheria hizi zilitambua na kurasimisha kisheria mila na desturi za wananchi wa Tanzania ambao hawana asili ya Asia na Ulaya ambao katika maisha yao wameishi kwa kufuata na kuzingatia taratibu za mila, tamaduni na desturi zao. Sheria hii inatoa haki ya kurithi kwa wale ambao wameishi kwa kuzingatia

9 GN No. 219 of 1967

mila na desturi katika jamii husika. Kwa kufuata misingi hiyo, pale ambapo inathibitika na Mahakama kuridhika kuwa enzi za uhai wake marehemu aliishi kwa kufuata, kuzingatia na kuheshimu mila na desturi za kabila lake, basi mirathi itafuata sheria za mila za kabila/jamii hiyo kama zinavyotumiwa na wahusika. Kwa sehemu kubwa sheria za urithi wa kimila zikitumika hufuata upande wa mwanaume ambapo warithi huwa ni watu wanaoangukia katika ngazi tatu kama ifuatavyo: -

**(i) Ngazi ya kwanza**

Ngazi hii inalenga mtoto wa kiume wa kwanza kutoka katika boma/ nyumba ya kwanza kama marehemu alikuwa na ndoa ya wake wengi. Pia huangaliwa mtoto wa kiume aliyezaliwa kwanza kutoka boma/nyumba yoyote, endapo marehemu hakubahatika kuwa na mtoto wa kiume katika Boma/nyumba ya kwanza.

**(ii) Ngazi ya pili**

Katika ngazi hii warithi au wanufaika ni watoto wote wa kiume waliosalia ambao hurithi sehemu kubwa kuliko watoto wa kike ambao huangukia katika ngazi ya tatu.

**(iii) Ngazi ya tatu**

Ngazi hii ni ya mwisho kabisa ambapo watoto wa kike hujumuishwa pamoja bila kujali tofauti zao za umri na au nafasi za mama zao katika ndoa. Mgao wao huwa sehemu ndogo kuliko mgao wanaopata watoto wa kiume. Hata hivyo endapo itatokea marehemu hakubahatika kupata watoto wa kiume, basi watoto wa kike huongezewa urithi.



#### 3.2.3.1 Mila na Dhana ya Ubaguzi wa Wanawake

Sehemu kubwa ya mila na tamaduni za watanzania zimekuwa na mrengo wa kupendelea au kuegemea kwa wanaume zaidi na kubagua haki ya mwanamke katika kurithi au kumiliki mali. Ili kuweka usawa mbele ya sheria, mnamo mwaka 1999 Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 5 ilifuta dhana nzima ya ubaguzi wa sheria za kimila. Kwa ufupi sheria hii ilileta usawa baina ya mwanaume na mwanamke katika kumiliki ardhi. Sheria imetamka kuwa;

*"... sheria yoyote ya kimila inayowanyima wanawake, watoto au watu wenye ulemavu uhalali wa kumiliki mali, kutumia au kupata ardhi, basi sheria hiyo ya mila itakuwa **batili**..."*

Pamoja na hayo, mila na desturi zimekuwa hazimtambuwi mjane kabisa katika dhana nzima kurithi mali za marehemu mume wake. Mila hazikuzingatia kabisa ushiriki au uchangiaji wa mjane katika kuchuma mali za familia ambazo mwisho wa siku hutambulika kama za mwanaume tu. Hata hivyo kwenye shauri la ***Maagwi Kimito vs Gibeno Werema***[10] Mahakama ya Rufani iliweka bayana kuwa sheria zote za kimila katika nchi hii lazima ziwe na hadhi sawa kwenye Mahakama kama sheria nyingine isipokuwa tu kama Katiba au sheria za nchi zitaelekeza tofauti. Kwa nukuu Mahakama ilisema: -

*"...The customary laws of this country now have the same status in our courts as any other law subject only to the Constitution and any statutory law that may provide to the contrary..."*

10 [1985] TLR 132 (CA)

Kuna mifano kadhaa ambapo Mahakama zetu za juu zimetoa miongozo juu ya sheria za mila katika mirathi. Kwenye kesi ya ***Violet Ishengoma Kahangwa & Jovin Mutabuzi vs Administrator General & Mrs Eudokia Kahangwa***[11] Mahakama ya Rufani pamoja na mambo mengine ilielekeza kuwa;

*"…that under paragraph 43 of the Local Customary Law (Declaration) (No.4) Order, 1963, G.N. No.436 as applied to the Bahaya tribe vide G.N. No. 605 of 1963, an illegitimate child cannot inherit from the father's side upon his dying intestate…"*

Kwa tafsiri rahisi Mahakama ya Rufani imesema kuwa katika mila za Wahaya mtoto wa nje hawezi kurithi mali za marehemu baba yake pale anapofariki bila ya kuacha wosia.

Mfano mwingine tunaupata kwenye shauri la ***Masudi Ally vs Chiku Masudi***[12] ambapo Mahakama Kuu ilisema:

*"…that under paragraph 26 of the 2nd schedule of the Customary Law Declaration 436/1963 only children of the deceased have the right to inherit from their deceased's parents' property… it is the children - them alone - of the Deceased that are customarily entitled to inherit the entire property, (without exception), of their late father. The appellant having been a complete stranger to the family of the Respondent's late father, he is equally a stranger to the property of the Respondent's late father..."*

Kwa Kiswahili Mahakama Kuu imesema kuwa ni watoto wa marehemu pekee wanaoweza kurithi mali za marehemu baba yao. Mtu baki haruhusiwi kurithi chini ya sheria za mila.

Inatupasa kuelewa vema kuwa kwenye shauri la ***Violet Ishengoma*** (Supra) Mahakama ya Rufani ilitafsiri haki ya kurithi kwa mtoto wa nje ya ndoa kwa kuzingatia sheria za mila pekee. Hata hivyo kwa kwa upande mwingine na kwa kuzingatia kuzingatia Sheria ya Mtoto na shauri la ***Elizabeth Mohamed vs Adolf John Magesa***[13] Mahakama Kuu imesema kuwa mtoto wa nje ya ndoa anayo haki ya kurithi mali za marehemu baba yake. Pia kwenye shauri la ***Judith Patrick Kyamba vs Tunsume Mwimbe & 3 Others***[14] ambapo pamoja na mambo mengine Mahakama Kuu imekuwa na mtazamo kuwa mtoto hapotezi haki ya kurithi mali ya mzazi wake kwa kigezo cha kuzaliwa nje ya ndoa. Kwa kuzingatia maamuzi ya Mahakama ya Kuu hadi sasa, (kwa kuwa bado maamuzi haya hayajatenguliwa na Mahakama ya Rufani) mtoto anastahili kurithi hata kama amezaliwa nje ya ndoa. Maamuzi haya ya Mahakama Kuu hayakinzani na maamuzi ya Mahakama ya Rufani kwenye shauri la ***Violet Ishengoma*** kwa kuwa sheria zilizotumika ni tofauti.

### 2.3.4 Sheria ya Dini ya Kiislamu

Sheria ya Kiislamu inatumika kwa wale wanaokiri au kuamini imani ya dini hiyo. Imani ya Kiislamu kuhusu mirathi ni kuwa mirathi ya peponi na duniani ni ya Mwenyezi Mungu[15]. Taratibu za kuendesha mirathi katika sheria hii zinajengwa kwenye dhana kuwa wanufaika wa mali za marehemu ni uhusiano wa karibu kwa kuzaliwa *(consanguinity)* au uhusiano wa ndoa[16]. Hata hivyo haki ya kurithi na taratibu zake zipo kwenye Kuruani Tukufu *(The Holy Qur'an)*. Taratibu hizi zinapata nguvu ya sheria kutoka kwenye sheria ya *The Islamic Law (Restatement) Act*[17] ambapo kifungu cha 2 cha sheria kinampa Waziri wa Sheria kuandaa tamko la sheria ya Kiislamu kwenye jambo lolote kuhusu imani ya Kiislamu *(The*

11 (1990) TLR 72 (CA)
12 (1992) TLR 50

13 Administration Appeal No. 14 OF 2011 (unreported) Mwanza
14 Probate and Administration Cause No. 50 of 2016 HC at Dar es salaam
15 Suraat Al-Imraan (2:180)
16 Doi, A. Sharia the Islamic law, pg. 272
17 Cap 375 R. E 2002

*Statements of the Islamic law).* Hata hivyo hadi sasa Waziri ametoa Tamko la Kiislamu kwenye sheria ya ndoa (Tamko la Sheria za Kiislamu la mwaka 1967)[18]. Hivyo hakuna tamko la aina hiyo kwenye sheria za mirathi. Hii inamaanisha kuwa kwenye imani ya Kiislamu mirathi inafuata utaratribu ambao upo kwenye Kuruani Tukufu *(The Holy Qur'an)* pekee. Mistari inayoongelea mirathi katoka *Qur'an* tukufu ni pamoja na Surat Annisaa[19].

Kwa kuondoa utata kifungu cha 4 cha sheria ya *The Islamic Law (Restatement) Act* kimeeleza kuwa tamko lolote litakalotolewa chini ya sheria hiyo litakuwa na nguvu kwenye mambo ambayo sheria za Kiislamu zinatumika kwa mujibu wa *The Succession (Non-Christian Asiatics) Act*[20] Kifungu cha 6 cha sheria hii kinatamka ifuatavyo: -

S. 6(1*) Subject to the provisions of this Act or any other Act or applied Act for the time being in force in Mainland Tanzania, the succession to the movable property in Mainland Tanzania of a deceased Non-Christian Asiatic who at the time of death is domiciled in Mainland Tanzania and to the immovable property in Mainland Tanzania of such a Non-Christian Asiatic whether or not domiciled in Mainland Tanzania at the death,* ***shall be regulated by the law of the religion professed by that Non-Christian Asiatic at death*****:**

18 GN 222 of 1967
19 4:11, 12, 176
20 Cap. 28 R.E 2002



*Provided that–*

*(a) so much of the law of any religion as deprives any person of a right of succession to property by reason of that person having renounced or having been excluded from the communion of any religion or having been deprived of caste shall not be in force in Mainland Tanzania; and*

*(b) every creditor shall have the same rights and remedies against the estate of a deceased Non-Christian Asiatic, including the right to follow assets, as the creditor has against the estate of a deceased Christian.*

*(2) This section shall apply to the estate of a Non-Christian Asiatic who died before the commencement of this Act in like manner as it applies to the estate of a Non-Christian Asiatic who dies after the commencement of this Act:*

*Provided that no part of an estate which has been distributed before the commencement of this Act shall be recoverable by reason only of any alteration in the law effected by this Act.*

*(3) This section shall not apply to Jews.*

Kwa ujumla wake kifungu cha 6 hapo juu kinatoa utaratibu wa kuendesha mirathi kwa mtu ambaye amekufa akifuata imani ya Kiislamu. Kifungu kinasema kuwa mirathi ya mtu huyo itafuata sheria za dini aliyokiri marehemu wakati wa uhai wake.

#### 2.2.4.1 Mambo ya Kuzingatia katika Mirathi ya Kiislamu

Kwanza kabisa sheria za mirathi ni za Mwenyezi Mungu na amri yake ni ya mwisho na hakuna mwenye mamlaka ya kubadilisha au kutengua sheria za mirathi ya Kiislamu. Hivyo kwa Muislamu anayeamini katika Mwenyezi Mungu na maandiko yake ni lazima azingatie kwa dhati sheria na taratibu za mirathi ya Kiislamu.

Pili, Mwenyezi Mungu ni muweza wa yote na mwingi wa busara na anajua kila kitu kwa kuwa yeye ni Muumba wa kila kitu. Mwenyezi Mungu anajua kwa nini ametupa gawio na amri zake zinazingatia maarifa, hivyo Muislamu anawajibika kwa jumla kuheshimu mapenzi ya Mwenyezi Mungu.

### 2.2.5 Sheria ya The Succession (Non-Christian Asiatics) Act[21]

Sheria hii inatumika na kutoa haki ya kurithi kwa watu ambao ni *Non – Christian Asiatics*. Sambamba na kifungu cha 6 kama kilivyonukuliwa hapo awali, utaratibu wa haki ya kurithi unazingatia sheria ya dini ambayo marehemu alikuwa amekiri. Sheria hii inalinda haki ya mirathi hasa pale ambapo marehemu anakuwa ametengwa *(excommunicated)* kwenye imani yake.

### 2.2.6 Sheria ya Mtoto[22]

Chini ya kifungu cha 10 cha sheria hii ni kosa kisheria kumnyima mtoto haki yake ya kurithi mali za wazazi wake. Pamoja na kuwa mtoto hajafikia umri wa mtu mzima (miaka 18) sheria hii inatoa msimamo thabiti kuwa mtoto asinyimwe haki ya kurithi. Mahakama Kuu ilitilia mkazo kwenye haki ya kurithi kwa mtoto kwenye shauri la ***Elizabeth Mohamed*** (Supra) ambapo ilisema hata mtoto wa nje ya ndoa anayo haki ya kurithi.

## 2.3 Taratibu za Kufikia Haki ya Kurithi

Katika kufikia haki ya kurithi ni lazima kufuata sheria zilizopo kwa ajili hiyo. Kuna sheria ambazo zinatumika Mahakama ya Mwanzo na nyingine zinatumika Mahakama za juu. Sheria hizi ni pamoja na: -

21 Cap. 28 R.E 2002
22 No. 21 of 2009



i. Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama ya Mwanzo (The Primary Courts (Administration of Estates) Rules[23]);
ii. Sheria ya Usimamizi wa Mirathi (The Probate and Administration of Estates Act[24]);
iii. Kanuni za Mirathi (The Probate Rules[25]);
iv. Sheria ya Mahakama za Mahakimu (The Magistrates' Courts Act[26]);
v. Sheria ya Usimamiaji Haki na Matumizi ya Sheria (Judicature and Application of Laws Act[27]);
vi. Sheria ya Ukomo wa Muda (The Law of Limitation Act[28]);
vii. Sheria ya Mtoto (The Law of the Child Act[29]).

## 2.4 Uchaguzi wa Sheria ya Kutumia

Matatizo na malalamiko mengi yasingetokea juu ya sheria za mirathi na ugawaji wa mali za marehemu kama jamii ingejua ni sheria ipi itumike juu ya mali zao wakati hawapo duniani. Uandaaji wa wosia na uchaguzi wa sheria ya kutumika wakati wa usimamizi na hatimaye ugawaji wa mali za marehemu ni jambo nyeti sana.

### 2.4.1 Uchaguzi Kulingana na Maisha ya Marehemu

Kama tulivyoona hapo awali, sheria imetambua na kuruhusu kutumika kwa mila na desturi za jamii husika katika kutatua migogoro mbalimbali ya jamiihiyo. Kwa upande wa mashauri yanayohusu mirathi mfano mzuri tunaupata katika kesi ya ***Innocent Mbilinyi (Deceased)***[30] ambapo katika kesi hii mwanaume mmoja wa *Kingoni* alimuoa dada wa *Kichaga* kwa kufuata ndoa ya kikristo na wawili hao walikuwa wanaishi mkoani Dar es salaam. Marehemu (Innocent) aliondoka nyumbani kwao Songea tangu akiwa na miaka 7 na amepata masomo yake hadi elimu ya juu akiwa nje ya mkoa

23 GN. 49 of 1971
24 Cap. 352 R.E. 2002
25 GN. 369 of 1963
26 Cap. 11 R.E. 2002
27 Cap. 358 R.E 2002
28 Cap. 89 RE 2002
29 No. 21 of 2009
30 (1969) HCD No. 283

wake. Mara chache amekuwa akitembelea nyumbani Songea au Moshi. Wawili hao walibarikiwa watoto watatu katika maisha yao ya ndoa. Wakati wa kusikiliza shauri la mirathi mjane alisisitiza sheria ya serikali *(statutory law)* itumike ili aweze kupata haki yake ya kurithi. Kwa upande mwingine kaka wa marehemu alitaka sheria ya mila itumike ili mjane asipate urithi kabisa. Mahakama Kuu (Georges, C.J) *aliamua kuwa, marehemu aliachana na maisha ya kimila kwa kuishi kama mkristo na kutofuata taratibu za mila na desturi.* Mahakama iliendelea kusema kuwa kuna ushahidi wa kujitosheleza kuwa marehemu alijitenga na familia yake na hata watoto wake hawana muunganiko na mambo ya mila, hivyo sheria ya serikali ilitumika.

Mfano mwingine tunaupata katika kesi ya ***George Kamwenda vs. Fides Nyirenda***[31] katika shauri hili marehemu Merten Kumwenda alikuwa raia wa Malawi aliyeishi wilaya ya Temeke, Dar es salaam. Baada ya kifo chake marehemu aliacha nyumba moja. Mjane alitaka kurithi nyumba kwa kupitia sheria ya serikali. Hata hivyo kaka wa marehemu alipinga hilo akitaka sheria ya mila itumike ili mjane asipate urithi wa nyumba hiyo bali iuzwe fedha zitakazopatikana zigawanywe kwa kaka, dada, wazazi na watoto wa marehemu. Mahakama ya Mwanzo iliamua kutumia sheria za mila lakini Mahakama ya Wilaya iliamua kutumia sheria ya serikali. Shauri lilipofika Mahakama Kuu, (Kisanga, J.) iliamuliwa kuwa shauri lianze upya kwa kusikilizwa kwa kuwa Mahakama za chini zilipotoka/ zilikosea kisheria na kimantiki kwa kutokuchukua jitihada za kutosha kuchunguza maisha ya marehemu wakati wa uhai wake ili kubaini ni sheria gani itumike katika shauri hilo.

31 [1981] TLR 211



Kwa kuzingatia mifano miwili ya kesi hapo juu haina shaka kusema kuwa ili kutambua sheria gani ya kutumia kuendesha shauri la mirathi (endapo marehemu hakutamka) basi Mahakama lazima ijiridhishe kikamilifu aina ya maisha ya marehemu enzi za uhai wake. Hata hivyo, pamoja na kuwepo kwa dhana ya jumla kuwa mwafrika anayeishi kijijini au mjini sheria ya kutumia ni ile ya mila kama ilivyoamuliwa kwenye kesi ya ***Abdallah Shamte vs. Mussa***[32] dhana hii inaweza isitumike endapo itabainika kuwa marehemu hakuishi kwa kufuata mila na desturi za jamii yake.

### 2.4.2 Uchaguzi Kulingana na Matakwa ya Marehemu

Pale inapotokea marehemu alikuwa akifuata Imani ya dini ya Kiislamu mara nyingi hutokea mgongoro juu ya sheria ipi hasa itumike kuendesha shauri la mirathi kati ya sheria ya mila, sheria ya kiislamu au ile ya serikali. Kifungu cha 88 cha Sheria ya Mirathi[33] kinaongelea utaratibu wa kufuata. Nanukuu kifungu hicho kwa lugha ya Kiingereza na baadae tafsiri yake (isiyo rasmi) kwa lugha ya Kiswahili.

*88 (1) The estate of every deceased person by virtue of which an order direction under Part IX applies shall be administered according to the following provisions–*

Kwa tafsiri rahisi ni kuwa, 'mali ya marehemu ambayo utaratibu au maelekezo yake yapo katika sehemu ya IX ya sheria hii itasimamiwa kwa mujibu wa vifungu vifuatavyo': -

32 (1972) H.C.D. No. 9
33 Sura 352 ya Marejeo ya Sheria ya 2002

(a) *The estate of a member of a tribe shall be administered according to the law of that tribe unless the deceased at any time professed Islam religion and the court exercising jurisdiction over his estate is satisfied from the written or oral declarations of the deceased or his acts or manner of life that the deceased intended his estate to be administered, either wholly or in part, according to Islamic law, in which case the estate shall be administered, either wholly or in part as the case may be, according to that law.*

(a) Mali ya marehemu wa kabila husika itasimamiwa kwa kufuata mila za kabila hilo isipokuwa pale ambapo marehemu alifata imani ya dini ya Kiislamu na Mahakama ikiridhika kuwa kwa njia ya maandishi au maneno ya marehemu au matendo yake au tabia/mtindo wa maisha ya marehemu unaonesha alikusudia mali zake zote au kwa sehemu zisimamiwe kwa sheria za Kiislamu, basi mali hizo zitasimamiwa kwa sheria hizo.

(b) *The estate of a Swahili shall be administered according to Islamic law unless the court exercising jurisdiction over his estate is satisfied from the written or oral declarations of the deceased or his acts or manner of life that he intended his estate to be administered, either wholly or in part, according to any customary law, in which case the estate shall be administered, either wholly or in part, as the case may be according to that customary law.*

(b) Mali za marehemu mswahili zitasimamiwa kwa kufuata sheria ya Kiislamu isipokuwa Mahakama inayosikiliza shauri la mirathi yake itajiridhisha kwa maandishi au kwa maneno ya marehemu au matendo yake au mtindo wa maisha yake alikusudia mali zake zote au kwa sehemu, zisimamiwe kwa kufuata sheria za mila basi mali hizo zitasimamiwa kwa sheria hizo.



*(2) If at any time any person to whose estate this Act applies by virtue of an order, or direction under Part IX thereof professed the Christian religion, and the court exercising jurisdiction over his estate is satisfied in the manner aforesaid that the deceased intended his estate to be administered, either wholly or in part, according to the law applicable in Tanzania to the administration of the estates of persons professing the Christian religion then his estate shall be administered, either wholly or in part, as the case may be, according to that law.*

Ikiwa wakati wowote mtu yeyote ambae mali zake zinasimamiwa kwa amri au maelekezo ya sehemu ya IX ya sheria hii na anafata imani ya dini ya Kikristo na Mahakama ikiridhika hivyo kuwa marehemu alikusudia mali zake zote au kwa sehemu zisimamiwe hivyo kwa kufuata sheria za Tanzania za usimamizi wa mirathi, basi mali hizo zitasimamiwa kwa sheria hizo.

Kwa kufuata vifungu vya sheria vilivyorejewa hapo juu, na hasa pale inatokea kuwa mtu amekufa akifuata imani ya dini ya Kiislamu, hiyo pekee haitoshi kusema moja kwa moja mali zake zitasimamiwa kwa kufuata misingi ya dini ya Kiislamu. Mtazamo huo unabaki kuwa sio sahihi. Kwenye kesi ya ***Re Kusundwa***[34] ilisemwa kuwa;

*Mara nyingine imedhaniwa kuwa kwa kuwa mtu alikuwa muislamu, hivyo ametengwa na sheria za mila, hiyo sio sawa. Kwa kuwa kwenye kesi hii marehemu hakuacha wosia wa maandishi au wa maneno, mtindo wa maisha ya marehemu utatumika kama kipimo. Kutokana na matendo ya marehemu na tabia yake imethibitika kuwa marehemu alikusudia sheria za Kiislamu zitumike kusimamia mali zake baada ya kifo chake.* Pia kwenye kesi ya ***Tatu Abdallah vs Waziri Mussa***[35] Mahakama ilitumia kipimo hicho cha mtindo wa

34 [1965] E. A 24B (T)
35 [1967] HCD No. 159

maisha wa marehemu kwa kusema kuwa kwenye mazingira ya kesi hii hakuna chochote kinachoonesha kuwa marehemu alikusudia sheria ya dini itumike kama sheria binafsi dhidi ya sheria za mila za Wangoni. Pia unaweza kurejea shauri la ***The Matter of the Estate of the Late Salum Omari Mkeremi***[36]**.**

## 2.5 Umuhimu wa Kuchagua Sheria

Kama tulivyoona hapo awali kuwa haitoshi tu kuwa na dini fulani au kabila fulani ambako kutapelekea sheria ya aina fulani kutumika. Kama marehemu hakuacha wosia juu ya sheria ipi itumike katika kusimamia mali zake baada ya kifo chake, basi kigezo kikuu ambacho Mahakama itakizingatia kuchagua sheria gani itumike kitakuwa ni mtindo au tabia ya maisha ya marehemu. Hivyo ili kuondoa migogoro isiyo ya lazima ni vizuri kuweka wazi sheria ya kutumika kusimamia mali zako hasa baada ya kuelewa vema aina ya sheria zinazotumika mahakamani na sababu zake.

***Tuzingatie mfano huu.***

*Huko nchini Kenya mwanasheria mmoja Silvanus Otieno alifariki ghafla. Mwanasheria huyo alikuwa wa kabila la Wajaluo na alikuwa ameoa mwanamke wa Kikuyu. Baada ya kifo chake, kaka yake alitaka kuzika mwili wake kijijini kwao alipozaliwa marehemu karibu na ziwa Victoria kwa mujibu wa tamaduni zao. Kwa upande mwingine mjane alitaka mume wake azikwe kwenye shamba lao mjini Nairobi. Baada ya mgogoro huu Mahakama nchini humo iliamua marehemu azikwe kwa mujibu wa mila na tamaduni zake. Mgogoro huu ulisababisha mwili wa marehemu kukaa mochwari kwa miezi kadhaa kabla ya Mahakama kutoa uamuzi.*

36 (1973) L.R.T No. 80



Kuna mifano mingi ya mazingira ya namna hiyo hapa nchini. Sina sababu ya kuiandika hapa, ila cha muhimu ni kufanyia kazi elimu uliyopata hapa. Saidia kuondoa usumbufu, ugomvi na chuki kwa ndugu zako na wale unaowapenda kwa kuandika wosia na au kuchagua sheria ya kutumika kusimamia na kugawa mali zako baada ya kifo chako. Uchunguzi unaonesha migogoro ya mirathi inaleta mgawanyiko mkubwa katika familia na jamiii kwa ujumla. Tafadhali usikubali kuwa chanzo cha kufakaranisha wale uwapendao ikiwa utatangulia kufariki na kuwaacha duniani. Kwa kuwa unawapenda chukua hatua sasa.

## 2.6 Mamlaka ya Kusikiliza Mashauri ya Mirathi

### 2.6.1 Mahakama ya Mwanzo

Mahakama za Mwanzo nchini zimeanzishwa kwa mujibu wa kifungu cha 3 (1) cha Sheria ya Mahakimu[37] *(The Magistrates Court Act, Cap. 11 R.E 2002)*. Mahakama hizi zimeanzishwa kwenye kila Wilaya nchini. Pamoja na mashauri mengine ya madai na jinai, mahakama ya Mwanzo imepewa mamlaka ya kusikiliza mashauri yote ya mirathi endapo sheria husika ni ile ya **Mila** au **Kiislamu**. Mamlaka ya Mahakama ya Mwanzo ni ndani ya Wilaya ambapo imeanzishwa. Hivyo endapo kuna msiba umetokea katika wilaya "A" shauri la mirathi litapelekwa kwenye Mahakama ya Mwanzo iliyopo kwenye wilaya hiyo "A" endapo sheria ya kutumika ni ile ya mila au Kiislamu. Kwenye kesi ya ***Ibrahimu Kusaga v. Emmanuel Mweta***[38] Mahakama Kuu ilisema: -

*"…A primary Court may hear matters relating to grant of administration of estates where it has jurisdiction, that is the law applicable is customary law or Islamic law…"*

37 Sura ya 11 ya Marejeo ya Sheria
38 (1986) TLR 26

Kwa tafsiri nyepesi Mahakama Kuu ilisema kuwa Mahakama ya Mwanzo inaweza kusikiliza mashauri ya mirathi na usimamizi wake pale inapokuwa na mamlaka ya kufanya hivyo, yaani kama sheria inayotumika ni ile ya Mila au ya Kiislamu.

Kifungu cha 1 (1) cha nyongeza ya 5 ya Sheria ya Mahakimu kinaelezea mamlaka ya Mahakama ya Mwanzo katika mashauri ya mirathi, kifungu hiki kinasema: -

*"The jurisdiction of a Primary Court in the administration of deceased's estates, where the law applicable to the administration or distribution of the succession to, the estate is customary law or Islamic law, may be exercised in cases where the deceased at the time of his death,* ***had a fixed place of abode within the local limits of the court's jurisdiction****"* (bolding supplied).

Tafsiri ya kifungu hiki kwa Kiswahili chepesi ni kuwa; "mamlaka ya Mahakama ya Mwanzo katika mashauri ya mirathi ni pale sheria inayotumika kuwa ya Mila au ya Kiislamu na mamlaka hayo yatatumika pale ambapo **marehemu alikuwa na makazi ya kudumu kwenye eneo (wilaya) ambapo Mahakama ina mamlaka**. (Maandishi yamekolezwa wino kuonesha msisitizo).

### 2.6.2 Mahakama ya Wilaya

Mahakama ya Wilaya imeanzishwa chini ya kifungu cha 4 (1) cha Sheria ya Mahakimu[39] ambapo inaanzishwa na kuwa na mamlaka kwenye Wilaya ambapo imeanzishwa. Mahakama hii ina nguvu na mamlaka ya kisheria kusikiliza mashauri ya awali na yale ya rufani kutoka Mahakama ya Mwanzo. Pia Mahakama ya Wilaya inaweza kufanya mapitio au marejeo ya mashauri yaliyosikilizwa

39 The Magistrates Courts Act, Cap. 11 R.E 2002.



katika Mahakama ya Mwanzo. Rejea vifungu vya 20, 21 na 22 vya Sheria ya Mahakimu.

### 2.6.3 Mahakama Kuu

Mahakama Kuu imeanzishwa na Ibara ya 108 (1) ya Katiba[40]. Ibara hii inasema: -

108 (1) *Kutakuwa na Mahakama Kuu ya Jamhuri ya Muungano (itajulikana kwa kifupi kama "Mahakama Kuu") ambayo mamlaka yake yatakuwa kama ilivyoelezwa katika Katiba hii au katika sheria nyingine yoyote.*

Mahakama hii ina mamlaka ya awali na ya rufaa katika mashauri mbalimbali. Kwa upande wa mashauri ya mirathi kifungu cha 3 cha Sheria ya Mirathi na usimamizi wa Mali za Marehemu[41] kinaipa Mahakama Kuu mamlaka ya kusikiliza na kutolea maamuzi mashwala yote yanayohusu mirathi na usimamizi wa mali za marehemu.

#### 2.6.3.1 Kusajili (*re-seal*) Mirathi Iliyosikilizwa Nje ya Nchi

Mahakama Kuu pekee ndio ina mamlaka ya kusajili *(re-seal)* mirathi iliyothibitishwa na mahakama za nje ya nchi. Ufafanuzi katika hili ni kwamba, endapo mtu amefia nje ya nchi na mirathi yake ikasikilizwa huko alipofia na msimamizi kuteuliwa, na kama huyo marehemu alikuwa na mali zake nchini Tanzania basi yule msimamizi atapashwa kuja nchini na kusajili mirathi yake kwenye Mahakama Kuu. Bila kufanya usajili katika Mahakama Kuu mirathi hiyo inakosa nguvu za kisheria na msimamizi hataweza kufanya kazi yake ya kukusanya mali za marehemu kwani atakuwa anakosa

40 Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977.
41 The Probate and Administration of Estates Act, Cap. 352 R.E 2002.

nguvu za kisheria za kufanya hivyo. Kifungu kinachoongoza Mahakama Kuu kusajili mirathi iliyofanyika nje ya nchi ni kifungu cha 95 cha Sheria ya Mirathi na Usimamizi wa Mali za Marehemu[42] ambacho kinasema ifuatavyo: -

95. *Where a court of probate in any part of the Commonwealth, has, either before or after the passing of this Act, granted probate or letters of administration in respect of the estate of a deceased person, the probate or letters so granted may, on being produced to, and a copy thereof deposited with the High Court, be sealed with the seal of that court, and thereupon shall be of the like force and effect, and have the same operation in Tanzania as if granted by that court.*

Hivyo utaratibu wa kusajili mirathi iliyokamilika nje ya nchi utafanyika Mahakama Kuu kwa njia ya maombi ambapo yatasikilizwa na kutolewa maamuzi na Mahakama. Hata hivyo katika kusikiliza maombi hayo na kabla ya kusajili mirathi hiyo, Mahakama Kuu chini ya kifungu cha 96 cha Sheria ya Mirathi na Usimamizi wa Mali za Marehemu[43] inapashwa kujiridhisha kuwa amana ya kutosheleza thamani ya mali zilizopo Tanzania, kama zipo, imetolewa kikamilifu kwa usalama wa mali husika. Mahakama Kuu pia kama itaona inafaa itapokea ushahidi kuhusu makazi ya marehemu.

*96. The High Court shall, before sealing a probate or letters of administration under this Part, be satisfied in the case of letters of administration, that security has been given in a sum sufficient in amount to cover the property, if any, in Tanzania to which the letters of administration relate, and may, in any case, require such evidence as it thinks fit, as to the domicile of the deceased person.*

42 The Probate and Administration of Estates Act, Cap 352 R. E 2002
43 The Probate and Administration of Estates Act, Cap 352 R. E 2002



Hivyo basi, tunapokuta mazingira kuwa ndugu amefia nje ya nchi ambapo pia alikuwa na makazi huko, na mirathi yake ikafunguliwa na kusikilizwa huko nje ya nchi, utaratibu wa kuifanya mirathi hiyo iwe na nguvu za kisheria hapa nchini ni kuisajili Mahakama Kuu kama tunavyoongozwa na vifungu vya hapo juu pamoja na Kanuni 97 hadi 104 za Mirathi[44].

Taratibu za kufungua, kusikiliza na kuteua msimamizi wa wa mirathi au kumthibitisha mtekeleza wosia zinafanana kwa kiasi kikubwa katika ngazi zote za mahakama. Hata hivyo utofauti uliopo ni kwenye sheria zinazotumika na Fomu maalumu zinazohusika kwenye mchakato wa kumpata msimamizi wa mirathi. Kwenye aya zinazofata tutaona taratibu za mashauri ya mirathi hasa kwenye mahakama za mwanzo na pia kurejea vifungu vya sheria vinavyohusika kwenye mahakama za Wilaya na Mahaakama Kuu kwa eneo husika.

Ni muhimu kuzingatia sana mahali pa kufungua shauri la mirathi kwani sheria inataka shauri lifunguliwe katika Mahakama ambayo ipo eneo au Wilaya ambayo marehemu si tu alikuwa anaishi bali alikuwa na makazi ya kudumu. Tunaweza kuona mfano katika shauri la ***Ashura M. Masoud vs Salma Ahmad***[45] ambapo shauri lilihamishiwa Mahakama ya Wilaya na kusikilizwa na Hakimu ambaye hakuwa na mamlaka ya kusikiliza na pia shauri lenyewe lilikuwa halistahili kusikilizwa na Mahakama ya Wilaya kwa kuwa thamani ya mali ya mirathi ilitakiwa isikilizwe na Mahakama ya Mwanzo. Hivyo baada ya shauri hili kufika Mahakama Kuu kwa njia ya rufani, iliamuliwa shauri lirudi na kusikilizwa upya katika Mahakama ya Mwanzo yenye mamlaka ya kusikiliza. Hatua hii ilipelekea kuchukua muda wa miaka saba (7) hadi Mahakama Kuu ilipotoa amri ya shauri kusikilizwa upya. Hii ina athari kubwa kwa wanufaika kwani muda mwingi unapotea Mahakamani

44 The Probate Rules
45 PC. Civil Appeal No. 213 of 2004.

na pia kuchelewesha upatikanaji wa haki. Hivyo ni muhimu sana kuzingatia kufungua shauri lako kwenye Mahakama yenye mamlaka ya kusikiliza.

Mfano mwingine tunaupata katika kesi ya ***Christina Alexander Ntonge vs Limi Mbogo***[46] ambayo pia inasisitiza umuhimu wa kuzingatia mamlaka ya Mahakama ya Mwanzo katika kusikiliza mashauri ambayo ni yale ya sheria ya Mila au ya Kiislamu pekee. Katika shauri hili Mahakama Kuu ilisisitiza kuwa pale ambapo mume na mke walikuwa na dini tofauti, Mahakama ya Mwanzo inakosa mamlaka ya kusikiliza kesi hiyo kwa kuwa sheria ya Kiislamu haitumiki, na pia kwa kuwa kumbukumbu za shauri hazionyeshi kuwa marehemu alikuwa akiishi kwa kufuata misingi na taratibu za mila.

Mtazamo wa Mahakama Kuu katika shauri tajwa hapo juu kuwa Mahakama ya Mwanzo haina mamlaka ya kusikiliza mashauri ya mirathi ambayo mali za marehemu zinahusisha viwanja au mashamba yaliyosajiliwa na Wizara ya Ardhi ulitenguliwa na Mahakama ya Rufani katika shauri la ***Scolastica Benedict vs Martin Benedict***[47] ambapo Mahakama ya Rufani ilitoa maelekezo kuwa kwa kupitia Tamko la Serikali No. 320[48] Jaji Mkuu alitoa mamlaka kwa Mahakama za Mwanzo kusikiliza na kuamua mashauri ya mirathi na usimamizi wa mali za marehemu bila ya kujali kuwa mali husika zimesajiliwa chini ya sheria za usajili wa ardhi. Jambo la muhimu katika kufanya hivyo Mahakama ya Mwanzo itazingatia kuwa sheria inayotumika ni ama ya Mila au ya Kiislamu. Kwa kunukuu Mahakama ya Rufani ilisema: -

46 PC Civil Appeal No. 11 of 2017
47 1993 TLR 1 (CA)
48 la mwaka 1964



*"While section 15(1)(c) of the Magistrates Courts Act 1963 (now s. 19 of the Magistrates' Courts Act 1984) did not specify the particulars relating to the administration of estates, the order of the Chief Justice published as Government Notice No. 320 of 1964 conferred jurisdiction on primary courts in matters of administration of estates regardless of whether the subject-matter is land registered under the Land Registration Ordinance, provided the applicable law is customary or Islamic law, other than matters falling under the Marriage, Divorce and Succession (Non-Christian Asiatics) Ordinance."*

Kwa kuzingatia mwongozo wa Mahakama ya Rufani kama inavyoonekana hapo juu, Mahakama ya Mwanzo inayo mamlaka ya kusikiliza mashauri ya mirathi na usimamizi wa mali za marehemu hata kama mali husika zimesajiliwa kwa sheria za ardhi. Kitu pekee cha kuzingatia ni sheria inayotumika lazima iwe ile ya Mila au ya kiislamu.

### 2.7 Mamlaka ya Mahakama ya Mwanzo kwenye Mashauri ya Mirathi

Sehemu ya I ya nyongeza ya 5 Sheria ya Mahakimu inaeleza mamlaka ya Mahakama hii katika mashauri ya mirathi. Hata hivyo kwa kuzingatia Aya ya 1(2) ya Sehemu ya I ya nyongeza ya 5 kuna mazingira ambayo Mahakama ya Mwanzo haiwezi kuteua msimamizi wa mirathi. Mfano ni pale ambapo msimamizi tayari ameteuliwa kwa kufuata Sheria ya Mirathi[49] na pia inakosa mamlaka ya kusikiliza migogoro ambayo msimamizi ameteuliwa na Mahakama nyingine. Kwa ufupi Aya 2 ya sehemu ya I ya nyongeza ya 5 inatabanaisha mamlaka ya Mahakama ya Mwanzo kuwa inaweza: -

49 The Probate and Administration Estate, Cap. 352 R.E 2002

a. Kuteua mtu mmoja au zaidi kusimamia mirathi, au
b. Afisa wa Mahakama, au
c. Kuteua mtu yeyote asiye na maslahi, mwadilifu na aliye na utayari wa kusimamia mirathi bila gharama.

Izingatiwe kuwa Afisa wa Mahakama (b) hapo juu hawezi kuwa Hakimu kwani atawajibika kutatua mgogoro endapo msimamizi atashindwa kuwafikisha warithi kwenye maridhiano ya pamoja. Kwa ujumla wasimamizi wa mirathi wakishindwa kusimamia mirathi wanawajibika kurudi Mahakama ya Mwanzo iliyowateua ili watenguliwe sawa sawa na nyongeza ya 5 ya Sheria ya Mahakimu.

Msimamizi wa mirathi aliyeteuliwa na Mahakama ya Mwanzo anawajibika kutoa hesabu kamili ya usimamizi wa mirathi kupitia fomu maalumu (Na. V & VI) za Mahakama ya Mwanzo sawa na matakwa ya Sehemu ya II ya nyongeza ya 5 ya Sheria ya Mahakimu. Uwasilishaji wa hesabu hizi unawezesha Mahakama kuhitimisha na hatimaye kufunga mirathi husika na kuepusha migogoro mingi inayoweza kuibuka baadae endapo mirathi haijafungwa.

Katika kusajili mashauri ya mirathi kuna ada ya kulipia ambayo inaongozwa na *Court Fees Rules*. Ada hii siyo kubwa na mwombaji anatakiwa kulipia ili shauri lake liweze kusajiliwa. Ikitokea mtu hana uwezo kabisa wa kulipa ada ya usajili anatakiwa kwenda Mahakamani na kutoa hoja yake ambapo baada ya kumsikiliza, mahakama itakubali au kukataa ombi lake. Hivyo ni rai kuwa hakuna sababu ya kutosajili shauri la mirathi kwa kukosa uwezo wa kulipa ada.



### 2.7.1 Muda wa Kufungua Shauri la Mirathi Mahakama ya Mwanzo

Mashauri ya mirathi katika Mahakama ya Mwanzo yanaongozwa na Tangazo la Serikali Na. 49 la mwaka 1971[50]. Kanuni ya 3 ya Tangazo hili inasema: -

*An application for the appointment of administrator under paragraph 2(a) or 2(b) of the Fifth Schedule to the Act shall be made in Form I1.*

Ni muhimu kuvifahamu vifungu 2(a) au 2(b) vya nyongeza ya 5 ya Sheria ya Mahakimu vilivyorejewa hapo juu. Ninavinukuu hapa chini: -

2. *A primary court upon which jurisdiction in the administration of deceased's estates has been conferred may: -*

   (a) *either of its own motion or on an application by any person interested in the administration of the estate appoint one or more persons interested in the estate of the deceased to be the administrator or administrators thereof, and, in selecting any such administrator, shall, unless for any reason it considers inexpedient so to do, have regard to any wishes which may have been expressed by the deceased;*

   (b) *either of its own motion or an application by any person interested in the administration of the estate, where it considers that it is desirable to do for the protection of the estate and the proper administration thereof, appoint an officer of the court or some reputable and impartial person able and willing to administer the estate to be administrator either together with or in lieu of an administrator appointed under subparagraph (a);*

50 G.N. No 49 OF 1971 The Primary Courts (Administration of Estates) Rules

Kwa kifupi vifungu hivi vinaeleza kuwa Mahakama yenyewe au kwa maombi inaweza kumteua mtu yeyote mwenye maslahi kusimamia mali za marehemu na katika kuteua huko Mahakama itazingatia matakwa ya marehemu.

Kumekuwa na mitazamo tofauti katika swala la ukomo wa muda kwa mashauri ya mirathi kwa kuwa sheria haipo bayana juu ya muda wa kufungua shauri la aina hiyo mara baada ya kifo. Mtazamo wa kwanza ni kuwa kwa kuwa maombi ya usimamizi wa mirathi yanafunguliwa chini ya vifungu 2(a) au 2(b) vya nyongeza ya 5 ya Sheria ya Mahakimu, muda wa ukomo unaangukia katika sehemu ya 3 ya nyongeza ya Sheria ya Ukomo[51] ambayo inatamka kuwa maombi yeyote yanayofanywa chini ya Sheria ya Mahakimu ukomo wake ni siku 60 tangu tarehe ya chanzo cha maombi, endapo muda wa ukomo haujatajwa. Hivyo kwa kuzingatia Sheria ya Ukomo, maombi ya uteuzi wa usimamizi wa mirathi au kutekeleza wosia yanapaswa kufikishwa Mahakamani ndani ya siku 60 baada ya kifo kutokea.

Hata hivyo Mahakama Kuu (Mhe. Mruma, J.) katika kesi ya ***Majuto Juma Nshahuzi vs Issa Juma Nshahuzi***[52] ilitoa mtazamo mpana zaidi juu ya ukomo wa kufungua mashauri ya mirathi. Mahakama ilisema: -

*"...there is no specific time limit for petition for letters of administration and in my view it would not be in the interest of justice to have such a provision..."*

51 The Law of Limitation Acy, Cap. 89 R.E 2002
52 PC Civil Appeal No. 9 of 2014 HC at Tabora



**Kwamba: -**

"…Hakuna muda maalumu wa kufungua mashari ya mirathi na kwa mtazamo wangu haitakuwa kwa maslahi ya haki kama kutakuwa na kifungu cha namna hiyo…"

Pamoja na hayo Mahakama ya Rufani katika shauri la ***Mwaka Musa vs Simon Obedi Simchimba***[53] imesisitiza kuwa endapo shauri la mirathi litapelekwa Mahakamani miaka 3 baada ya kifo cha marehemu, maombi yanapashwa kuambatana na maelezo ya sababu za uchelewaji huo.

### 2.7.1.1 Athari zitokanazo na kuchelewa kufungua shauri la Mirathi

Marehemu anapoacha mali zake duniani zinakosa msimamizi anayetambulika kisheria hadi hapo atakapoteuliwa na Mahakama. Katika kipindi hicho uwezekano mkubwa wa kuficha, kuiba au kutumia vibaya mali za marehemu unaongezeka. Hivyo ni vema sana kupata msimamaizi wa mirathi na mali za marehemu haraka iwezekanavyo baada ya kifo chake.

Kuna mazingira ambayo pia kama shauri la mirathi litacheleweshwa kufunguliwa Mahakamani na kuteuliwa kwa msimamizi wa mirathi, kuna haki ambazo zinaweza kupotea. Mfano mashauri ya madai yanafungwa na sheria ya ukomo, hivyo kama marehemu alikuwa na madai yake kwa mtu mwingine na msimamizi wa mirathi yake akichelewa kuteuliwa sheria ya ukomo (miaka 6 tangu dai la marehemu kuanza) itamzuia kudai haki hiyo ya marehemu. Hali pia ipo hivyo katika madai ya umiliki wa ardhi. Kama msimamizi hakuteuliwa kwa wakati na ukapita muda wa miaka 12 basi msimamizi hataweza kudai haki ya ardhi ya marehemu kwa kuwa atafungwa na sheria ya ukomo wa muda.

53 Civil Appeal No. 45 of 1994 CA at Dar es salaam (unreported) uk 8

## 2.8 Utaratibu wa Kufungua Shauri la Mirathi Mahakama ya Mwanzo

Maombi ya kuteuliwa kuwa msimamizi au kuthibitishwa kuwa msimamizi wa mirathi pale ambapo kuna wosia huanza na Fomu Na. I[A] (ona mfano mwisho wa kitabu) ambayo ni fomu maalumu ya maombi ya kumteua msimamizi wa mirathii mbele ya Mahakama ya Mwanzo. Fomu hii inapatikana Mahakamani. Endapo marehemu aliacha wosia basi mleta maombi ataambatanisha na wosia, au kama wosia haupo kwenye milki yake ataieleza Mahakama kwa njia ya maandishi jina na anwani ya mtu ambae ametunza wosia huo au, kama wosia unadaiwa kupotea, kuharibika au kutoonekana, basi mleta maombi anapashwa katika mazingira hayo kupeleka Mahakamani kwa njia ya maandishi kile kinachodaiwa kuwa ndani ya wosia na aambatanishe na kiapo cha kuthibitisha usahihi wa madai hayo.

Ikitokea mleta maombi ameshindwa kuambatanisha wosia kwenye maombi yake ya kuthibitishwa kuwa msimamizi wa mirathi na ameshindwa kueleza kwa njia ya maandishi na kuthibitisha kwa kiapo nini kilikuwa ndani ya wosia, Mahakama itachukulia kuwa hakuna wosia ulioachwa na marehemu au kutokana na mazingira ya maombi/shauri itachukuliwa wosia umepotea, umeharibika au kutoonekana. Kwa upande mwingine endapo mleta maombi ataambatanisha kinachodaiwa kuwa wosia wa marehemu kwenye maombi yake, afisa wa Mahakama atapashwa kutoa nakala ya wosia huko na kuweka nakala halisi sehemu salama.



## 2.9 Nyaraka za Kuambatanisha kwenye Maombi ya Usimamizi wa Mirathi

Kuepusha usumbufu usio wa lazima, mtu yeyote anayetaka kuomba kuwa msimamizi wa mirathi ni vema akaandaa nyaraka zifuatazo na kuziwasilisha Mahakamani pamoja na Form I iliyojazwa kikamilifu. Nyaraka muhimu ni pamoja na: -

a. Cheti cha kifo cha marehemu na

b. Muhtasari wa kikao ndugu wa marehemu.

Hata hivyo Mahakama Kuu (Chocha, J) kwenye shauri la ***Angela Philemoni Ngunge vs Philemon Ngunge***[54] ilikuwa na haya ya kusema: -

*"... In answer to the issue before, the required procedure is for the potential applicant to simply file an application using the prescribed forms. Otherwise, the minutes are a mere worth encouragement, but lacks legal effect upon omission…*

*in exercise its power in terms of section 2 (a) of part I of the 5th schedule of the Magistrate Court Act Cap. 11 R.E 2002, dully appoint them all as administrators of the deceased estate and issue to them the necessary relevant documents (forms) in accordance with the legal requirements for them to effectively pursue the estate.* ***For avoidance of doubts, no clan minutes whatsoever shall be required****..."*

Kwa ufafanuzi katika shauri hili Mahakama Kuu ilikuwa na mtazamo kuwa jambo la msingi la kuzingatia katika maombi ya usimamizi wa mirathi ni kwa mleta maombi kujaza fomu maalumu kwa ajili hiyo. Vinginevyo muhtasari wa kikao cha ukoo/familia inafaa kuzingatia tu lakini hakuna madhara ya kisheria kwa kutoleta muhtasari… katika kutekeleza mamlaka yake chini ya kifungu cha 2 (a) cha Sheria ya Mirathi Sura ya 11 Mahakama

54 Civil Application No. 2 of 2002

itawateua wasimamizi wa mirathi na kuwapa fomu maalumu kwa mujibu wa matakwa ya sheria ili waweze kusimamia mirathi hiyo. **Kwa kuondoa utata, muhtasari wa kikao cha ukoo/ familia hautahitajika**. (Maandishi yamekolezwa wino kuonesha mkazo).

Hata hivyo ni muhimu kupitia Fomu I kuweka wazi taarifa zifuatazo katika maombi ya usimamizi wa mirathi: -

i. Tarehe na mahali alipofia marehemu.
ii. Wasifu wa familia na ndugu wa marehemu.
iii. Haki zinazoombwa na mleta maombi.
iv. Kiasi na asili ya mali za marehemu zinazoweza kupatikana kwa urahisi na mleta maombi kipindi akiwasilisha maombi yake.
v. Kwamba upekuzi makini umefanyika na kujiridhisha marehemu hakuacha wosia wowote.
vi. Kutoa taarifa kama kuna maombi mengine yanayofanana au kuhusiana na mirathi ya marehemu katika Mahakama nyingine yenye mamlaka ya kusikiliza maombi hayo.
vii. Kutoa maelezo juu ya maskani ya marehemu.

### 2.10 Vigezo vya Kuzingatia kwa Mleta Maombi

Vitu muhimu ambavyo Mahakama lazima ijiridhishe navyo katika kupokea na kusikiliza maombi ya usimamizi wa mirathi ni kwamba; Mleta maombi lazima awe mtu mzima, awe na akili timamu, awe mwaminifu na mwenye uwezo wa kukusanya, kutunza hesabu na kugawa mali za marehemu kwa warithi halali. Kwa kuzingatia haya, ni muhimu kufahamu kuwa muomba kusimamia mirathi sio lazima awe ndugu wa damu na marehemu, ila tu vigezo vya muhimu ni hivyo vilivyotajwa hapo juu. Katika eneo hili ni vizuri kuelewa



zaidi kuwa msimamizi wa mirathi sio lazima awe mrithi ila ni yule mtu atakaetekeleza majukumu ya usimamizi wa mirathi. Katika shauri la ***Sekunda Mbwambo vs Rose Ramadhani***[55] Mahakama Kuu (Rutakangwa, J) akiongelea madhumuni ya kuteua msimamizi wa mirathi alisema: -

*"…the objective of appointing an administrator of the estate is the need to have a **faithful person** who will, with reasonable diligence, **collect all the properties of the deceased**. He will do so with the **sole aim of distributing the same to all those who were dependants** of the deceased during his life-time. The administrator, in addition, has the duty of **collecting all the debts** due to the deceased and **pay all the debts owed** by the deceased. If the deceased left children behind, it is the responsibility of the administrator to ensure **that they are properly taken care** of and well brought up using the properties left behind by their deceased parent…" (Emphasis supplied)*

Katika kesi hii Mahakama ilisema kuwa madhumuni ya kuteua msimamizi wa mirathi ni uhitaji wa kupata **mtu mwaminifu** ambae kwa uadilifu na umakini **atakusanya mali za marehemu**. Atakusanya mali hizo kwa **lengo kuu la kuzigawanya kwa wale wote waliokuwa wakimtegemea marehemu** enzi za uhai wake. Msimamizi ana wajibu wa **kukusanya madeni** yote marehemu anayodai na **kulipa yote anayodaiwa**. Na kama marehemu ameacha watoto, ni wajibu wa msimamizi **kuhakikisha kuwa wanatunzwa ve**ma na kukuzwa kwa kutumia mali zilizoachwa na marehemu mzazi wao. *(Maandishi yamekolezwa wino kuonesha mkazo)*

55 [2004] TLR 439.

Kwa kuzingatia maelekezo ya Mahakama katika shauri tajwa hapo juu, uhusiano wa undugu sio mojawapo ya kigezo cha mtu kuteuliwa kuwa msimamizi wa mirathi. Kinachozingatiwa ni sifa tajwa hapo juu na Mahakama ijiridhishe kuwa kweli mwombaji anakidhi kuteuliwa kufanya kazi hii muhimu. Muhimu kuzingatia zaidi kuwa, maombi ya usimamizi wa mirathi lazima yaeleze bayana juu ya yafuatayo;

a. *Kiasi na aina ya mali iliyoachwa na marehemu;*
b. *Majina na anwani za warithi; na*
c. *Sehemu atokayo marehemu na mahali mali zilipo (hii ni muhimu kwani husaidia kuamua ni mahakamani gani stahiki inaweza kupokea maombi ya ufunguzi wa mirathi).*

## 2.11 Matangazo ya Mashauri ya Mirathi

Mara baada ya maombi kupokelewa Mahakamani chini ya kifungu 2 (a) au 2 (b) au kama Mahakama imeamua yenyewe bila ya kuwepo kwa maombi chini ya kifungu kidogo (1) au kifungu cha 3 Mahakama itatoa wito wa kufika Mahakamani kwa watu wote wanaodiwa kuhusika na mirathi ya marehemu au watu wa karibu na marehemu. Pia Mahakama itatoa wito kwa mtu aliyetajwa kwenye wosia kama msimamizi wa mirathi. Isipokuwa wito huo hautatolewa kwa mleta maombi[56].

Wito huu wa Mahakama unatolewa kwa Fomu Na. II (ona mfano mwishoni mwa kitabu) ukiwataka watu wote wanaodaiwa kuwa na maslahi na mali za marehemu kufika katika Mahakama husika katika siku na muda uliopangwa ili shauri husika la mirathi liweze kusikilizwa. Hata hivyo sheria imezingatia endapo mwenye maslahi na mali za marehemu ni mtoto (chini ya miaka 18) au ni mtu mwenye ulemavu wa akili basi wito huo utatolewa kwa mlezi au kwa mtu anaeishi nae. Utaratibu wa kutoa wito na kuupeleka kwa wahusika unasimamiwa na Amri ya V ya Sheria ya Mashauri

56 Kanuni 5 (1) & (2) cha G.N. No 49 OF 1971 The Primary Courts (Administration of Estates) Rules



ya Madai *(Order V ya Civil Procedure Code[57])* Pamoja na utaratibu huu wa kisheria, Mahakama inaweza kutoa amri ya kutangaza kwa njia inayotumika katika eneo husika katika kutangaza matangazo ya umma au inaweza kutoa amri tangazo hilo lichapishwe katika gazeti. Mahakama ipo huru kutoa amri ya njia yeyote kadri itakavyoona inafaa kulingana na mazingira ya shauri husika.

Lengo la kutangaza ni kuhakikisha kila mwenye maslahi na mali za marehemu anapata taarifa ili awepo kwenye usikilizwaji wa maombi ya usimamizi wa mirathi. Hatua hii ya utangazaji ni kuepusha haki ya marehemu kupotea au wale wenye haki juu ya mali ya marehemu kuwepo kwenye shauri kuepusha migogoro isiyo na lazima.

Kwa kutilia uzito na umuhimu wa matangazo ya mashauri ya mirathi, Jaji Kiongozi kupitia waraka wake No. 4 wa mwaka 2005 pamaja na mambo mengine alitoa maelekezo kuwa: -

*"...Kuna umuhimu mkubwa sasa kuliko wakati wowote ule waheshimiwa Majaji na mahakimu wote wenye uwezo kisheria, kuyapa kipaumbele mashauri ya mirathi mara yanapofikishwa mahakamani na* ***kuepuka mazoea ya kutangaza mirathi kwa miezi mitatu (Siku 90)****. Hata hivyo, utangazaji wa mirathi ni lazima ili hata wale wanaoona kuwa wana haki wapate nafasi za kumjua msimamizi wa mirathi ili kupata kudai haki zao, lakini isiwe ni sababu ya kuchelewesha uteuzi wa msimamizi wa mirathi. Kila ombi litaangaliwa kwa mazingira yake, kabla Jaji au Hakimu hajatoa amri ya siku za kutangaza maombi hayo ya mirathi. Hata pale ambapo kuna pingamizi (caveat) siku za kusikiliza pingamizi na kutoa uamuzi ziwe za muda mfupi..."* (Msisitizo umeongezewa)

57 Sura 33 Marejeo 2002. Hii ni kwa Mahakama Kuu na Wilaya.

Mahakama Kuu (Mlacha, J) katika shauri la ***Hadija Said Matika vs Awesa Said Matika***[58] baada ya Mahakama kupokea maombi ya usimamizi wa mirathi alisema: -

*"... The court will react by issuing a citation in Form No. II. The citation must be published in any local News Paper and further be affixed at the court premises and other key buildings in the locality (see rule 5 of GN 49 of 1971). **The aim is to ensure that information is circulated to all interested parties particularly the heirs, debtors and creditors**. The usual practice is to advertise for three (3) months **but that period can be reduced by the court on special reasons to be recorded**. The emphasis here is that where it is advertised for a shorter period the reasons must be recorded. It is not therefore for the court to act on pressures of parties who come to court at an eleventh hour and seek quick appointments. Quick appointments are dangerous and are the source of many complaints and misdeeds. The court must act judiciously and ensure that the information circulate to all interested people. To accomplish that aim, in my view, the **citation must stand for at least four (4) weeks**. The court must stand firm on this aspect to avoid future complaints and protect its respect..."* (Emphasis supplied)

Katika shauri hili Mahakama imesisitiza kuwa utangazaji wa shauri la mirathi ufanyike kwenye gazeti na pia tangazo libandikwe kwenye jengo la Mahakama na majengo mengine muhimu katika eneo hilo. **Lengo la kufanya hivi ni kuhakikisha taarifa ya uwepo wa shauri unafika kwa watu wote wenye maslahi hasa warithi, wadaiwa na wadai**. Utaratibu wa kawaida ni kutangaza kwa muda wa miezi mitatu (3) **lakini muda huu unaweza kupunguzwa na Mahakama kwa sababu maalumu ambazo zitaaandikwa** kwenye jalada la shauri. Msisitizo ni kwamba kama shauri litatangazwa kwa muda mfupi zaidi sababu za kufanya hivyo

58 PC Civil Appeal No. 2 of 2016. Imerejewa kwenye Shauri la ***Elias Madata Lameck vs Joseph Makoye***. Lameck PC Probate and Administration Appeal No. 1 of 2019 HC at Musoma.



lazima ziandikwe. Kwa hiyo Mahakama haipaswi kufanya hivyo kwa msukumo wa wadaawa. Kwamba uteuzi wa haraka ni hatari na ni chanzo cha migogoro. Hivyo Mahakama lazima itende kwa haki na kuhakikisha taarifa zinafika kwa watu wote wanaohusika. Ili kufikia lengo hilo, **matangazo yafanyike angalao kwa muda usiopungua wiki nne (4)**. Mahakama haina budi kusimamia hili na kuepuka na migogoro ya baadae na kulinda heshima yake. (Msisitizo umeongezewa)

## 2.12 Taratibu Endapo Wahusika Hawajafika Mahakamani

Ikitokea kuwa mmoja wa wanaoomba kuteuliwa kusimamia mirathi, au mtu yeyoye ambae wito umetumwa kwake ukimtaka kufika Mahakamani siku na muda uliopangwa na akishindwa kufika, Mahakama inaweza kuahirisha shauri na kulipangia tarehe nyingine au kwa maombi ya mmoja wa waleta maombi au mtu yeyote aliyeudhuria kwa mujibu wa wito na akithibitisha kuwa yupo tayari kufanya kazi hiyo ya usimamizi wa mirathi ya marehemu, basi Mahakama inaweza kuendelea kusikiliza maombi na ikifikia mwisho inaweza kutoa amri ya kumteua msimamizi wa mirathi au inaweza kukataa kumteua mleta maombi[59].

Kwa lugha nyepesi ni kuwa, kama umepata wito wa kufika mahakamni na ukaamua kutohudhuria Mahakamani siku na muda uliopangwa ama kwa makusudi au kutokana na dharula Mahakama inaweza kutoa amri ya kuendelea kusikiliza shauri. Hivyo endapo kuna dharula yoyote ni muhimu kuitaarifu Mahakama kwa nini haujafika, usipotoa taarifa Mahakama haiwezi kujua kwa nini haujafika na inaweza kuendelea bila wewe kuwepo. Hata hivyo Mahakama haiwezi kutoa amri ya kuendelea kusikilizwa kwa shauri kama wito haujatumwa kikamilifu kwa watu wenye maslahi. Kipimo hapa ni wito ufike kwa wakusudiwa wote bila kificho kwa watu wengine ambao nao wana maslahi na mali za marehemu.

59 Kanuni 6 (1) cha G.N. No 49 OF 1971 The Primary Courts (Administration of Estates) Rules

Kwa upande mwingine endapo wito umetumwa kwa mtu yeyote kwa kuwa ni mlezi wa mtoto au mwangalizi wa mtu mwenye ulemavu wa akili na akashindwa kuhudhuria Mahakamani siku na muda uliopangwa, Mahakama inaweza kuendelea kusikiliza shauri isipokuwa kama mtoto au mtu huyo mwenye ulemavu wa akili hajapata msimamizi au mwangalizi Mahakama itaahirisha shauri hilo hadi hapo msimamizi au mwangalizi atakapoteuliwa.

### 2.13 Usikilizaji wa Maombi ya Usimamizi wa Mirathi au Kuthibitishwa kuwa Mtekeleza Wosia

Baada ya maombi kupokelewa na baada ya amri ya matangazo kutolewa na kufanyiwa kazi na wadaawa, hatua inayofata ni usikilizaji wa shauri/maombi. Katika hatua hii Mahakama itasikiliza na kumteua mleta maombi au kumkatalia kuwa msimamizi wa mirathi na badala yake kuteua mtu mwingine. Katika hatua ya usikilizaji na uteuzi, Mahakama inazingatia iwapo marehemu aliacha wosia au alifariki bila wosia wowote. Na kama itadaiwa kuwa marehemu aliacha wosia, basi itajiridhisha kuwa wosia huo umezingatia vigezo vyote vya wosia unaokubalika kisheria. Pia Mahakama itajiridhisha juu ya uhalali wa watu walioorodheshwa kama warithi au wanufaika wa mali za marehemu.

### 2.14 Pingamizi katika Shauri la Mirathi

Pingamizi ni kitendo cha mtu yeyote kwenda Mahakamani na kuzuia au kupinga kisheria kwa Mahakama kutoa amri ya aina fulani kwenye shauri la mirathi. Mfano kunaweza kuwa na pingamizi la kumteua mleta maombi au kumthibitisha kuwa mtekelezaji wosia, pingamizi la mgao wa mali, pingamizi la orodha ya mali na madeni na hata pingamizi la warithi wa marehemu. Pingamizi husikilizwa Mahakamani baina ya pande zote mbili (mleta pingamizi na mleta maombi) na kisha Mahakama inatoa uamuzi juu ya pingamizi husika.



Kwa njia ya pingamizi, mtoa pingamizi hutoa sababu za kupinga uthibitishwaji au uteuliwaji wa mtekelezaji au msimamizi wa mirathi ya marehemu. Baada ya kuwasilisha pingamizi Mahakamani, maombi ya mirathi huchukua mfumo wa shauri la kawaida la madai na mwombaji wa mirathi hupewa muda wa kujibu malalamiko ya mweka pingamizi. Hivyo Mahakama husikiliza pingamizi hilo na inaporidhika na sababu zitolewazo katika pingamizi, inaweza kubatilisha uthibitishwaji wa mtekeleza mirathi au kukataa uteuzi wa mwombaji usimamizi wa mirathi.

Kwa upande mwingine endapo muda wa kuwasilisha pingamizi utapita na Mahakama ikamthibitisha au kumteua mtekelezaji au msimamizi wa mirathi, na baadae ikathibitika kwamba kulikuwapo na kughushi, au udanganyifu kuhusiana na usimamizi, au utekelezaji wa wosia, basi maombi yanaweza kupelekwa Mahakamani kutaka mtekelezaji au msimamizi aondolewe na/ au usimamizi wake kutenguliwa. Kama kuna lalamiko au pingamizi lolote juu ya mteule wa usimamizi wa mirathi lipelekwe katika Mahakama ile ile iliyomteua. Hoja itasikilizwa na mwongozo utatolewa.

### 2.15 Aina Za Mapingamizi

#### 2.15.1 Pingamizi Dhidi ya Maombi/ Mwombaji

Aina hii ya pingamizi hulenga kupinga maombi yaliyowasilishwa na mleta maombi. Mleta pingamizi katika kipengele hiki anatakiwa kuieleza/kuithibitishia Mahakama kuwa maombi yameletwa kinyume na sheria ama mleta maombi hana sifa za kuwa msimamizi wa mirathi au mtekelezaji wa wosia. Endapo mleta maombi sio mtu mwaminifu, hana uwezo wa kutunza hesabu na kusimamia mali za marehemu au ni mfujaji wa mali basi mtu yeyote mwenye maslahi anaweza kuweka pingamizi la aina hii Mahakamani. Pia katika pingamizi la namna hii kama tayari kuna mtu mwingine amewahi kuteuliwa na Mahakama nyingine kusimamia mali za marehemu

huyo huyo basi ni halali kwa mtu yoyote mwenye maslahi katika mali hizo kupeleka pingamizi katika Mahakama ambayo mwombaji mwingine ameenda kuomba kuteuliwa kusimamia mirathi hiyo.

### 2.15.2 Pingamizi la Orodha ya Mali

Baada ya Msimamizi wa mirathi kuteuliwa au mtekeleza wosia kuthibitishwa na Mahakama kupitia Fomu Na. IV atapaswa kukusanya mali zote za marehemu na kuandaa orodha yake ikionesha na thamani na kuipeleka Mahakamani. Orodha hii inakuwa katika fomu maalumu, yaani Fomu Na. V. Orodha hii siyo ya siri wala mali ya msimamizi wa mirathi pekee, ni orodha ambayo kila mwenye maslahi au mwenye kudai haki kutoka mali za marehemu anaweza kuipitia na kujiridhisha nayo. Kifungu cha 10 (2)[60] kinatoa fursa kwa watu wenye maslahi kama wadai, Kabidhi Wasii Mkuu, warithi au wanufaika wa mirathi kupeleka maombi Mahakamani ili apate fursa ya kupitia orodha ya mali za marehemu ili kujiridhisha na usahihi wake.

Dosari katika kuandaa orodha ya mali za marehemu, wakati mwingine ni kwa kujua/makusudi au kwa kutokujua. Kuna kuorodheshwa mali ambazo siyo za marehemu au kutoorodhesha baadhi ya mali za marehemu. Katika mazingira ya namna hiyo mtu mwenye maslahi anatakiwa kuitaarifu Mahakama (ni muhimu kuzingatia pingamizi linawekwa katika Mahakama ile iliyomteua msimamizi wa mirathi) kuhusiana na dosari ya orodha ya mali na kuleta ushahidi wa kuthibitisha hayo. Hoja itaamliwa kwa mujibu wa kifungu cha 8 (d)[61] na Mahakama itatoa maamuzi juu ya pingamizi hilo.

Katika shauri la ***Joseph Mniko & Others***[62] Mahakama Kuu – Dar es salaam (Shangwa, J) alikubali maombi ya kuwaondoa kwenye nafasi ya usimamizi wa mirathi ya marehemu Faustine Mniko

60 G.N. No 49 OF 1971 The Primary Courts (Administration of Estates) Rules
61 G.N. No 49 OF 1971 The Primary Courts (Administration of Estates) Rules.
62 Probate No. 48 of 1996.



Mahende baada ya kujiridhisha kuwa msimamizi wa mirathi Daudi Mahende Kichonge ametumia vibaya nafasi yake ya usimamizi wa mirathi.

Katika shauri hili Mahakama Kuu imesisitiza kuwa kitendo cha msimamizi wa mirathi kushindwa kutoa hesabu ya mali za marehemu kwa zaidi ya miaka tisa (9) baada ya kuteuliwa kuwa msimamizi wa mirathi kinaondoa sifa yake ya kuendelea kuwa msimamizi. Tabia yake mbaya ya kufuja mali za marehemu hasa kodi ya nyumba Na. 4 Kawe, Dar es salaam inafanya mambo kuwa mabaya zaidi na kudhibitisha kuwa msimamizi hafai kuendeleana wajibu huo. Sheria ipo bayana kuwa msimamizi anapaswa kupeleka Mahakamani na orodha ya mali za marehemu ndani ya kipindi cha miezi 4[63] kama shauri limesikilizwa Mahakama ya Mwanzo na ndani ya miezi sita kama ni Mahakama Kuu au ya Wilaya[64].

### 2.15.3 Pingamizi la Mgawanyo wa Mali

Wajibu wa msimamizi wa mirathi au mtekeleza wosia hauishii kwenye kukusanya mali tu, bali unaendelea hadi kugawa mali hizo kwa warithi au wanufaika halali. Kifungu cha 10 (1)[65] kinaelezea wajibu mkubwa na wa msingi wa kazi za msimamizi wa mirathi. Kifungu hiki kinamtaka msimamizi wa mirathi kukabidhi Mahakamani orodha ya ukweli na kamilifu ya mali za marehemu kwa mujibu wa Fomu Na. V, akionyesha pia madeni ya marehemu na kwa muda kadri Mahakama itakavyopanga. Kifungu hiki kinamtaka msimamizi wa mirathi kutoa hesabu ya mali za marehemu kupitia Fomu Na. VI akionyesha fedha zote za marehemu kama zilivyopokelewa, malipo yaliyofayika na mali zingine zilizouzwa au kuhamisha umiliki kulikofanywa na msimamizi. Kifungu kinasomeka kama ifuatavyo: -

63 Kifungu 10 (1) G.N No. 49 of 1971 The Primary Courts (Administration of Estates) Rules.
64 Kifungu cha 107 cha The Probate and Administration of Estates Act, Cap. 352 R.E 2002.
65 G.N. No 49 of 1971 The Primary Courts (Administration of Estates) Rules.

10 (1) *Within four months of the grant of administration or within such further time as the liabilities court may allow, the administrator shall submit to the court a true and complete statement, in Form V, all the assets and liabilities of the deceased persons' estate and, at such intervals thereafter as the court may fix, he shall submit to the court a periodical account of the estate in Form VI showing therein all the moneys received, payments made, and property or other assets sold or otherwise transferred by him.*

Mantiki ya kifungu hiki ni kuhakikisha mali zote za marehemu zimeingia kwenye orodha moja na kwamba zinagawanywa au zitagawanywa kwa kuzingatia haki za warithi wote au wanufaika wote. Kwa kuzingatia kifungu hiki kama warithi au wanufaika hawajaridhika na orodha au na mgawanyo wa mali za marehemu atapeleka pingamizi hilo Mahakamani chini ya kifungu cha 8 (f)[66] na Mahakama itasikiliza na kutoa maamuzi juu ya mgawanyo wa mali hizo za marehemu. Pingamizi litasikilizwa kama shauri la kawaida la madai ambapo mashahidi wataitwa kwa pande zote mbili na maamuzi kutolewa. Katika shauri la ***Mgeni Seif vs Mohamed Yahaya Halifani***[67] Mahakama ya Rufani ilisisitiza kuwa pingamizi lolote juu ya umiliki wa mali katika orodha ya mali za marehemu au umiliki juu ya mali iliyogawanywa wakati wa mirathi linatakiwa kusikilizwa na Mahakama iliyomteua msimamizi wa mirathi. Hata hivyo ni muhimu kuzingatia kuwa katika kusikiliza pingamizi la aina hii Mahakama inatakiwa kuzingatia kuwa haina jukumu la kugawa mali za marehemu kwa warithi ila inachotakiwa kusimamia ni kutolea maamuzi kwenye pingamizi tu. Katika shauri la ***Shabani Omary vs Mary Joseph***[68] Mahakama kuu ilisisitiza kuwa ni kosa kwa Mahakama kugawa mali za marehemu. Jukumu hilo ni la msimamizi wa mirathi aliyeteuliwa na Mahakama na sio vinginevyo.

66 G.N. No 49 OF 1971 The Primary Courts (Administration of Estates) Rules.
67 Civil Application No 1 of 2009 CA (unreported)
68 Prob. Cause No. 23 of 2003 HC Moshi



Kwa kuzingatia wigo wa kanuni ya 10[69] **msimamizi wa mirathi anapaswa na anawajibika** kufanya mambo makuu yafuatayo ndani ya miezi mine (4) tangu kuteuliwa kwake: -

i. Kukusanya mali zote za marehemu na kuandaa orodha timilifu na yenye ukweli mtupu na kuiwasilisha Mahakamani ndani ya miezi mine (4)[70] tangu ateuliwe kuwa msimamizi.
ii. Kugawa mali za marehemu kwa warithi au wanufaika halali.
iii. Kuweka sawa kumbukumbu na hesabu za fedha na mali za marehemu.
iv. Kurudisha Mahakamani hesabu za fedha na mali za marehemu kwa kutumia Fomu Na. VI.

Ni muhimu pia kuzingatia kuwa kifungu cha 11 cha nyongeza ya 5 ya Sheria ya Mahakimu[71] pia kinatoa takwa la msimamizi wa mirathi kutoa hesabu za mali za marehemu baada ya kumaliza kazi ya usimamizi au kama atakavyoagizwa na Mahakama. Kifungu hicho kinasoma hivi: -

*After completing the administration of the estate and, if the primary court orders, at any other stage of the administration an administrator shall account to the primary court for his administration.*

Hivyo ieleweke kuwa pale mtu anapoteuliwa kuwa msimamizi wa mirathi ana wajibu wa kisheria kurudisha Mahakamani hesabu za mali za marehemu. Anapaswa kukamilisha kazi hiyo ndani ya miezi minne (4) au kadri Mahakama itakavyopanga. Kwa upande mwingine ieleweke kuwa ***shauri la mirathi halifikii mwisho wake pale msimamizi wa mirathi anapoteuliwa na Mahakama au mtekeleza wosia anapothibitishwa, mwisho wa shauri la aina hii ni pale msimamizi anapowasilisha hesabu za mwisho kwa mujibu wa Form Na. VI***.

69 G.N. No 49 of 1971 The Primary Courts (Administration of Estates) Rules
70 Miezi sita kwa Mahakama ya Kuu na Wilaya.
71 Sheria ya Mahakama za Mahakimu (The Magistrates Courts Act, Cap. 11 R.E 2002)

## 2.16 Kuteua Msimamizi wa Mirathi au Kumthibitisha Mtekelezaji Wosia

Uteuzi wa msimamizi wa mirathi au mtekeleza wosia unasimamiwa na kifungu cha 7[72]. Uteuzi huu huja baada ya maombi kusikilizwa na Mahakama kujiridhisha kuwa mleta maombi anao uwezo wa kusimamia mali za marehemu. Pia kama kulikuwa na pingamizi (kama tulivyoona hapo awali) lazima kwanza lisikilizwe na kukamilika. Baada ya uteuzi, msimamizi ataweka saini kwenye Fomu ya uwajibikaji (Fomu Na. IV) lakini kabla ya kuweka saini kwenye Fomu hiyo ya **uwajibikaji Mahakama inapaswa kumweleza msimamizi vipengele vilivyopo kwenye Fomu kwa lugha ambayo msimamizi anaielewa.** Jukumu hili la Mahakama kumweleza mteule wa usimamizi wa mirathi ni jambo la msingi sana ili mteuliwa ajue kwa uwazi majukumu yaliyo mbele yake na madhara ya kutokufanya kazi ya usimamizi kwa uwazi, uadilifu na uaminifu.

Hata hivyo, Mahakama inaweza kumtaka mtu aliyeteuliwa kuwa msimamizi wa mirathi kuweka dhamana kwa ajili ya usimamizi wa mirathi ya mali za marehemu. Na endapo Mahakama itatoa amri hiyo uteuzi hautakuwa na maana, yaani hautafanya kazi hadi pale dhamana hiyo itakapokuwa imewekwa kwa kiwango kilichowekwa na Mahakama.

72 G.N. No 49 OF 1971 The Primary Courts (Administration of Estates) Rules



## 2.17 Mirathi pasipo Wosia

Neno *Mirathi* limetafsiriwa na Mahakama ya Rufani katika shauri la ***Mark Alexander Gaetje na Two Others vs Brigitte Gaetje Defloor***[73] ambapo imeeleza kuwa "Mirathi" inajumuisha wosia na usimamamizi ambapo katika wosia mtekeleza wosia anaelekezwa kutimiza matakwa ya marehemu katika mali zake. Mahakama pia imemuelezea msimamizi wa mirathi ni mtu anayeteuliwa na Mahakama kama hakuna wosia ili asimamie mirathi husika. Kwa mwongozo huo pale ambapo kifo kinatokea bila ya marehemu kuacha wosia, Mahakama huteua msimamizi wa mirathi ili afanye kazi ya kusimamia mali za marehemu.

Kama tulivyoona awali, katika kipindi cha siku thelathini (30) tangu mtu anapofariki ndugu au wahusika wanapaswa kusajili kifo cha marehemu kwenye Ofisi ya Vizazi na Vifo ambayo iko kwa Mkuu wa Wilaya wa kila wilaya Tanzania Bara. Kama wahusika watachelewa kusajili kifo ndani ya siku (30), basi wafike kwenye Ofisi hiyo ya vizazi na vifo kwa maelezo. Kifo kinasajiliwa kwenye Ofisi ya Mkuu wa Wilaya iliyopo mahali kilipotokea, na sio katika wilaya yeyote ile. Kama kuna matatizo kuhusu wapi kifo kisajiliwe, wahusika wanaweza kuwasiliana na msajili Mkuu wa Vizazi na Vifo, Makao Makuu, yaliyopo Dar es Salaam au wawakilishi wake waliopo katika ngazi ya Wilaya. Katika mirathi ambapo hakuna wosia kwa mazoea (sio Sheria) maombi ya msimamizi kuteuliwa Mahakamani kwa huzingatia kuwa ametimiza hatua zifuatazo: -

i. Msimamizi au wasimamizi wa mirathi huteuliwa au kuchaguliwa na kikao cha wanandugu au ukoo.
ii. Mwombaji hupeleka maombi yake Mahakamani akiomba kuteuliwa kuwa msimamizi wa mirathi. Maombi hayo yanatakiwa yaambatane na vitu vifuatavyo: -

73 Civil Revision No. 3 of 2011, CAT (unreported).

a. Nakala ya cheti cha kifo cha marehemu;
b. Nakala ya kikao cha wanandugu cha kumchagua msimamizi wa mirathi;
c. Tamko la mwombaji kwamba atasimamia mirathi kwa uaminifu;
d. Kiapo cha wanandugu kwamba wanamteua mwombaji kuwa msimamizi wa mirathi; na
e. Kiapo cha mashahidi wakimdhamini mwombaji na kwamba wako tayari kutoa fidia - endapo mwombaji atashindwa kusimamia vizuri.

## 2.18 Rufaa Kutoka Mahakama za Mwanzo

Baada ya Mahakama ya Mwanzo kusikiliza shauri la mirathi na kutoa maamuzi, upande wowote (yaani mleta maombi au mpinga maombi) au mwenye maslahi na mali za marehemu, na alikuwa mdaawa kwenye shauri husika, anaweza kupinga uamuzi huo kwa njia ya rufani katika Mahakama ya Wilaya. Pia ieleweke vizuri kuwa, rufaa kutoka Mahakama ya Mwanzo itapelekwa kwenye Mahakama ya Wilaya ambapo Mahakama hiyo ya Mwanzo ipo. Sheria hairuhusu kukata rufani kutoka Mahakama ya Mwanzo iliyopo Wilaya tofauti na Mahakama ya Wilaya. Kwa mfano, kama shauri la awali la mirathi lilifunguliwa Mahakama ya Mwanzo Magomeni basi rufaa yake itapelekwa Mahakama ya Wilaya Kinondoni.

### 2.18.4 Muda na Utaratibu wa Kukata Rufani

Mahakama zinaongozwa na sheria, kanuni na taratibu. Pia ili kuwepo na ukomo wa mashauri Mahakamani, kuna muda wa kuzingatia ili shauri lako liweze kusajiliwa kama rufaa.



Kwa upande wa mashauri ya mirathi rufani zake kwenda Mahakama ya Wilaya zinasimamiwa na Sheria ya Mahakimu. Kifungu cha 20 (3) cha Sheria ya Mahakimu[74] kinatoa muda wa ukomo wa kupeleka rufaa Mahakama ya Wilaya na pia kinatoa utaratibu wa kufungua au kusajili rufaa Mahakamani. Endapo upande wowote haujaridhika na maamuzi ya Mahakama ya Mwanzo unapaswa kukata rufani Mahakama ya Wilaya ndani ya kipindi cha siku thelathini (30) tangu tarehe ya maamuzi ya Mahakama ya Mwanzo. Kifungu hiki kinasema: -

20 (3) *Every appeal to a district court* ***shall be by way of petition*** *and shall be filed in the district* ***court within thirty days after the date of the decision*** *or order against which the appeal is brought.* (Msisitizo umeongezwa).

### 2.18.5 Nini Kifanyike kama upo nje ya Muda?

Swali hili ni la msingi sana kwani kutokana na changamoto za maisha unaweza ukajikuta muda huo uliowekwa na sheria umepita, hivyo ukawa nje ya muda. Sheria imezingatia mazingira ya namna hiyo na kuruhusu Mahakama ya Wilaya kuongeza muda ama kabla au baada ya muda kuisha. Kifungu kidogo cha (4) cha kifungu cha 20 cha Sheria ya Mahakimu kinaeleza bayana.

20 (4) *Notwithstanding the provisions of subsection (3)–*

(a) *the district court may extend the time for filing an appeal either before or after such period has expired; and*

(c) *if an application is made to the district court within the said period of thirty days or any extension thereof granted by the district court, the district court may permit an appellant to state the grounds for his appeal* orally and shall record them and hear the appeal accordingly.

74 Sheria ya Mahakama za Mahakimu (The Magistrates Courts Act, Cap. 11 R.E 2002)

### Angalizo:

Endapo umechelewa kusajili rufaa yako Mahakama ya Wilaya ni lazima uwe umezuiliwa na sababu za msingi kabisa. Na pia ni lazima utoe hesabu ya kila siku uliyochelewa hadi uiridhishe Mahakama kwa nini ulishindwa kusajili rufaa yako ndani ya muda uliopo kisheria. Mahakama Kuu katika mashauri kadhaa imeongelea eneo hili na kuonya kuwa muda utaongezwa endapo tu muombaji atathibitisha na kuiridhisha Mahakama kuwa kweli kuna sababu za msingi zilizomzuia kufungua shauri ndani ya muda. Tuone mashauri yafuatayo kama yalivyoamuliwa na Mahakama Kuu.

***Tanzania Revenue Authority vs TRA Consolidated***[75] *where it was clearly stated that in determining whether or not to grant extension of time the court must be guided with the following elements; one, the* ***length of delay****, two,* ***the reasons for delay*** *and the degree of prejudice to the defendant if the application is granted.*

Katika shauri hili Mahakama Kuu ilikuwa na mtazamo kuwa katika kupima iongeze muda kwa muombaji au la, inapaswa kuangalia mambo yafuatayo: -

i. Muda wa kuchelewa; na
ii. Sababu za kuchelewa kwa kila siku ya uchelewaji.

Pia katika shauri la ***Registered Trustee of Sos Children's Villages Tanzania vs Igenge Charles & 9 Others***[76] Mahakama ya Rufani ilirejea shauri la ***Regional Manager Tanroads Kagera vs Ruaha Conxcrete Company Limited***[77] ambapo ufafanuzi wa maana ya 'sababu za msingi' za kuchelewa kupeleka shauri Mahakamani ulitolewa. Mahakama ya Rufani ilisema: -

75 Civil Application No 4 of 2009 and 9 of 2008.
76 Civil Application No. 80/08 of 2017 CA at Mwanza.
77 Civil Application No. 96 of 2007 (unreported).



*"What constitutes sufficient cause as it was Rule 8 of the Court of Appeal Rules, 1979, which now is good cause of the current Rule 10 of the Rules, 2009, cannot be laid down by any hard and fast rules. This must be determined by reference to all the circumstances of each particular case.* ***This means that, the applicant must place before the Court material which will move the Court to exercise its judicial discretion in order to extend time limited by the rules. "***

Kwa kifupi Mahakama ya Rufani imesema kuwa sababu za msingi zinapimwa kulingana na mazingira ya kila kesi. Hivyo muuombaji anapashwa kuieleza Mahakama mambo muhimu na ya msingi yaliyomfanya akashindwa kufika Mahakamani ili Mahakama iweze kutumia mamlaka yake na kutoa amri ya kuongeza muda. Hivyo jambo la msingi ni kuelewa kuwa kama umechelewa kuja Mahakamani kwa sababu ambazo hazina mashiko basi Mahakama haiwezi kutumia mamlaka yake na kuongeza muda. Ni rai kuwa kama unadai haki kwenye mali za marehemu na hujaridhika na maamuzi ya Mahakama ya Mwanzo uzingatie muda wa kukata rufaa ili haki yako isipotee.

### 2.19 Taratibu za Uteuzi Mahakama ya Wilaya na Mahakama Kuu

Katika Mahakama ya Wilaya na Mahakama Kuu, utaratibu wa kuteua msimamizi wa mirathi hautofautiani na Mahakama ya Mwanzo, isipokuwa katika ngazi hii maombi yanafanyika kwa mujibu wa nyongeza ya nne (4) ya Sheria ya Mirathi[78] . Mahakama ya Wilaya na Mahakama Kuu zinaongozwa na Kanuni za Mirathi[79] katika mashauri ya mirathi. Kanuni ya 85 inamtaka muombaji wa mirathi kujaza Fomu Na. 76 iliyopo kwenye nyongeza ya kwanza ya kanuni7. Baada ya maombi kusikilizwa na mapingamizi kama yapo, mwishowe Mahakama itateua msimamizi wa mirathi

78 The Probate and Administration of estates Act, Cap. 352 R.E 2002.
79 The Probate Rules.

kwa kupitia Fomu Na. 78 katika nyongeza ya kwaza ya kanuni. Nyongeza ya kwanza ya Kanuni za mirathi imeorodhesha jumla ya sampuli 86 za Fomu mbalimbali zinazotumika katika mirathi Mahakama ya Wilaya na Mahakama Kuu. Kila hatua inatumia Fomu hizi maalumu tofauti kabisa na aina nyingine ya mashauri mahakamani.

Pingamizi katika Mahakama hii linawekwa kwa kufata Fomu Na. 62 na usikilizwaji wakehuchukua sura ya shauri la madai tofauti na Mahakama ya Mwanzo.

### 2.19.6 Uteuzi kwa Lakiri ya Mahakama na Dhamana

Katika kuteua msimamizi wa mirathi Mahakama ya Wilaya au Mahakama Kuu zinatakiwa kufanya hivyo kwa lakiri ya Mahakama na itamtaka msimamizi wa mirathi kutia saini ya utekelezaji wa kazi ya usimamizi kwa uaminifu. Sambamba na hayo Mahakama ikiona inafaa itamtaka msimamizi wa mirathi kuweka dhamana ya kusimamia mirathi kadri itakavyoona inafaa. Angalia vifungu vya 76 na 77 Sheria ya Mirathi[80].

## 2.20 Kabidhi Wasii Mkuu Mkuu wa Serikali

Kabidhi Wasii Mkuu[81] ni kiongozi wa Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA)[82]. Kiongozi huyu anateuliwa chini ya kifungu cha nne (4) cha sheria ya Kabidhi Wasii Mkuu (Mamlaka na Wajibu)[83]. Jukumu la msingi la nafasi hii ni kusimamia mirathi ama kwa kuomba kufuatia kuteuliwa na Mahakama, au kwa kuteuliwa moja kwa moja na Mahakama. Katika masuala ya usimamiaji mirathi RITA huongozwa na Sheria ya Kabidhi Wasii Mkuu (Mamlaka na Wajibu), Sura ya 27 R.E ya 2002.

80 The Probate and Administration of Estates Act, Cap 352 R. E 2002.
81 The Administrator General.
82 Registration, Insolvency and Trustship Agency.
83 Sura ya 27 Marejeo ya 2002 (The Administrator-General (Powers and Functions) Act, Cap. 27 R.E 2002)



Inafaa kusema kwa maneno mengine kuwa, Ofisi ya Kabidhi Wasii Mkuu wa Serikali pamoja na mambo mengine inajishughulisha katika usimamizi wa mirathi kwenye mazingira mawili. Moja ni pale marehemu ameacha wosia kwamba mirathi yake isimamiwe na ofisi ya Kabidhi Wasii Mkuu wa Serikali au endapo Mahakama itateua ofisi hii kuwa msimamizi wa mirathi. Hii hutokea endapo kuna pingamizi dhidi ya wasimamizi wa mirathi au kukosekana maelewano. Kwa wepesi wa rejea kifungu cha 75[84] kinasoma ifuatavyo: -

75 (1) *Where a district court is of the opinion that, having regard to the safety of the estate and the proper administration thereof, it is desirable that the estate should be administered by the Administrator-General or an officer of the district court or some reputable or impartial person able and willing to administer the estate it may adjourn an application for an appointment in order that it may be ascertained whether the Administrator-General will undertake the administration of the estate under section 52 of the Administrator-General (Powers and Functions) Act or may appoint an officer of the district court or some such person aforesaid as administrator.*

(2) *An appointment of an administrator under this Part shall not be made if there has been a previous grant of probate of the will of the deceased or letters of administration of his estate, or if the Administrator-General has himself lawfully undertaken the Administration of the estate.*

84 The Probate and Administration of Estates Act, Cap 352 R. E 2002.

Kifungu kidogo cha pili (2) hapo juu kinatoa angalizo kuwa Kabidhi Wasii Mkuu hatateuliwa kusimamia mirathi ambayo tayari kulikuwa na msimamizi aliyethibitishwa au kuteuliwa na Mahakama hapo awali au kama Kabidhi Wasii Mkuu alikuwa amechukua usimamizi wa mirathi hiyo kwa mujibu wa sheria.

### 2.20.1 Taratibu, Mahitaji au Mazingira ya Kabidhi Wasii Mkuu Kusimamia Mirathi

#### 2.20.1.1 Kwa Maombi

Kabidhi Wasii Mkuu anaweza kuwa msimamizi wa mirathi kwa kuombwa kufanya hivyo na watu au mtu mwenye maslahi na mali za marehemu. Taratibu za kufuata ili kumpata Kabidhi Wasii Mkuu kuwa msimamizi wa mirathi zinaanza kwa kuwasilisha barua ya maombi RITA au kwa Katibu Tawala wa Wilaya (DAS)[85] katika wilaya inayohusika ambako marehemu ameacha mali zake. Baada ya kupokea maombi hayo DAS atajaza fomu maalumu (Fomu AG7) na kuiwasilisha RITA akiomba Kabidhi Wasii Mkuu kusimamia mali za marehemu huyo. Ni muhimu kuzingatia kuwa kigezo muhimu ni lazima mwombaji awe mtu mwenye maslahi katika mali za marehemu au mtu ambae kama mirathi haitasimamiwa basi atapoteza mali au ataathirika.

Baada ya kupokea Fomu AG7 kutoka kwa DAS, Kabidhi Wasii Mkuu atachambua maombi na akiyaona yanafaa kwa kusimamia mali atapeleka maombi Mahakamani akiomba ateuliwe kuwa msimamizi wa mirathi husika. Ikitokea Kabidhi Wasii Mkuu ataona haifai kwa yeye kusimamia mirathi kama alivyoombwa atawashauri wahusika njia mbadala ya kuitumia. Pia ni muhimu kuzingatia kuwa kuna ada za kulipia ambazo zinategemea ukubwa wa mali za marehemu.

85 District Administrative Secretary.



#### 2.20.1.2 Kuteuliwa moja kwa moja na Mahakama

Mtu yeyote mwenye maslahi na mali za marehemu anaweza kuomba Mahakama imteue Kabidhi Wasii Mkuu kuwa msimamizi wa mirathi ya marehemu anayehusika. Maombi ya aina hii yatakayopelekwa Mahakamani lazima mwombaji apeleke nakala ya maombi hayo kwa Kabidhi Wasii Mkuu. Maombi haya yatasikilizwa kama maombi ya kawaida ya usimamizi wa mirathi. Hata kama kuna anayepinga Kabidhi Wasii Mkuu asiteuliwe kusimamia mirathi, atasikilizwa na pingamizi lake litatolewa maamuzi. Mwisho Mahakama inaweza kumteua Kabidhi Wasii Mkuu kusimamia mirathi au isimteue kabisa. Pia Mahakama inaweza ikamteua pamoja na mtu mwingine ili wasimamie pamoja.

Endapo Kabidhi Wasii Mkuu atateuliwa kusimamia mirathi atatekeleza jukumu la kukusanya mali, kulipa madeni na mwishoni kugawanya mali kwa warithi kulingana na sheria inayotumika au makubaliano ya wanaogawiwa, au kwa kufuata wosia, kama upo. Taratibu zote za kuwasilisha orodha ya mali na hesabu za mwisho lazima aziwasilishe Mahakamani kwa wakati.

### 2.20.2 Mamlaka ya Mahakama Kumteua Kabidhi Wasii Mkuu

Kifungu cha 75[86] cha Sheria ya Mirathi kinaipa Mahakama mamlaka ya kumteua Kabidhi Wasii Mkuu wa Serikali au afisa wa Mahakama au mtu mwingine asiye na maslahi kwenye mali za marehemu na aliye na uwezo na utayari wa kusimamia mirathi, kumteua ili afanye kazi hiyo ya usimamizi. Mazingira yanayopelekea Mahakama kufanya hivyo ni pale itakapoona kwa usalama wa mali za marehemu na usimamizi mzuri inafaa kumteua Kabidhi Wasii Mkuu wa Serikali. Katika mazingira hayo Mahakama itaahirisha maombi ya kuteuliwa kuwa msimamizi wa mirathi na kuangalia kama Kabidhi Wasii Mkuu wa Serikali atasimamia mirathi hiyo kwa mujibu wa kifungu cha 52 cha Sheria ya Kabidhi Wasii Mkuu wa Serikali[87].

86 The Probate and Administration of Estates Act, Cap 352 R. E 2002
87 The Administrator General Act, Cap. 27 R. E 2002

## 2.21 Nguvu ya Msimamizi wa Mirathi

Endapo Mahakama imeteua au kumthibitisha msimamizi wa mirathi na kumpa barua ya kuthibitisha hayo, msimamizi huyo atakuwa na nguvu, mamlaka na haki kamili ya kusimamia mali zote za marehemu. Anaweza kukusanya mali zote, kulipa madeni na kugawa mali hiyo kwa warithi na wanufaika. Pia anaweza kushtaki au kushitakiwa kuhusiana na mali za marehemu. Hata hivyo uteuzi wa Mahakama haumpi msimamizi uhalali wowote wa kumiliki au kutumia mali za marehemu kwa maslahi yake binafsi. Endapo msimamizi ni sehemu ya warithi au wanufaika atatakiwa kufanya kazi hiyo kwa uaminifu mkubwa kama sheria inavyoelekeza.

Katika shauri la ***Malietha Gabo vs Asamu Mtengu***[88] Mahakama Kuu (Mugeta, J.) ilirejea mashauri kadhaa ya Mahakama Kuu na kuweka bayana nafasi na wajibu wa msimamizi wa mirathi hasa kwenye mashauri au madai ya ardhi yanayotokana na mali alizoacha marehemu. Katika hili Mahakama imetoa ufafanuzi wa kina juu ya dhana kuwa, iwapo kuna mgogoro wa ardhi na kama ni sehemu ya mali ya marehemu, basi mgogoro huo unapashwa kusikilizwa na kutatuliwa kwenye shauri la mirathi. Katika mazingira ya namna hii Mahakama imefafanua kuwa;

*"…kwa mujibu wa sheria, mahakama ya mwanzo inayosikiliza shauri la mirathi haina mamlaka ya kuamua mgogoro wa ardhi unaohusu mali ya marehemu. Mamlaka ya mahakama hizi imefungwa kwenye kuteua msimamizi, kuthibitisha warithi halali na kumsimamia msimamizi wa mirathi kukamilisha kazi yake…"*

88 Misc. Land Appeal No. 21 of 2020 HC at Kigoma (Unreported).



Mahakama Kuu imeongeza zaidi kuwa;

*"…kwenya mgogoro kama ardhi inabishaniwa kama ni sehemu ya mali ya marehemu au la, mgogoro huo unapashwa kuamuliwa na ama mahakama za kawaida za madai au mahakama za ardhi, kadri itakavyokuwa…*

*Utofauti uliopo wa kisheria na utendaji ni pale madai yanasimamia kwenye haki ya kurithi au kununua kwa thamani wakati bado shauri la mirathi lipo mahakamani na msimamizi wa mirathi hajasajili hesabu za mwisho, na mahakama haijafunga shauri. Kwenye mazingira hayo mahakama inayosikiliza mirathi hiyo inaweza kuamua iwapo umiliki wa ardhi umehamia kwa mtu mwingine kupitia msimamizi wa mirathi. Ikiwa kama mgogoro hauangukii kwenye mazingira hayo mawili, lakini msimamizi wa mirathi amesajili hesabu za mwisho na mirathi imefungwa, mahakama hiyo ya mirathi haiwezi kuwa na mamlaka…"*

Hivyo ni muhimu kutofautisha mazingira ambayo mahakama inayosikiliza shauri la mirathi inaweza kuamua juu ya umiliki wa ardhi inayobishaniwa kama tulivyoona hapo juu. Kimsingi mamlaka ya kusikiliza migogoro ya ardhi ipo kwenye Mabaraza ya Ardhi ya Kata, Wilaya na Mahakama Kuu. Hii inamaanisha kuwa Mahakama ya Mwanzo wala ya Wilaya haina mamlaka ya kusikiliza mashauri ya ardhi.

## 2.22 Kutenguliwa kwa Msimamizi wa Mirathi

Katika jamii yetu mara nyingi watu wanaamini kuwa msimamizi wa mirathi akishateuliwa au kuthibitishwa na Mahakama basi hakuna jambo lingine linaloweza kufanyika kumpinga. Ukweli ni kwamba msimamizi wa mirathi au mtekeleza wosia anaweza kutenguliwa au kuondolewa katika nafasi hiyo endapo chochote kati ya vifuatavyo vitadhibitika;

i. Kwamba maombi ya usimamizi yalikuwa na makosa makubwa katika maudhui yake *(defective in substance)*;
ii. Kwamba uteuzi uligubikwa na udanganyifu kwa kupeleka Mahakamani taarifa za uongo au kuficha taarifa muhimu;
iii. Kwamba uteuzi ulipatikana kwa njia ya kusema tuhuma za uongo katika pointi ya sheria ili kuhalalisha uteuzi, na kuwa tuhuma hizo zilitolewa kwa kutokujua au bila kujali;
iv. Kama uteuzi umekuwa hauna maana na haufanyi kazi; au
v. Kama msimamizi wa mirathi kwa hiari yake ameacha au ameshindwa kuonyesha mali na hesabu za mali za marehemu au ametoa hesabu za uongo.

Ni muhimu kuzingatia kuwa mtu yeyote aliyeteuliwa na Mahakama kuwa msimamizi wa mirathi kwa ulaghai au kwa namna yoyote inavyoonekana hapo juu, uteuzi wake unakuwa ni batili na unapashwa kwenda katika Mahakama iliyemteua na kufanya maombi ya kutengua uteuzi wake. Agalia kifungu cha 49 cha Sheria ya Mirathi na Usimamizi wa Mali za Marehemu[89].

## 2.23 Mahakama ya Rufani

Ibara ya 117 (1) ya Katiba[90] inaanzisha Mahakama ya Rufani. Ibara hii inatamka yafuatayo: -

117 (1) *Kutakuwa na Mahakama ya Rufani ya Jamhuri ya Muungano ("itakayojulikana kwa kifupi Mahakama ya Rufani") ambayo mamlaka yake yatakuwa kama ilivyoelekezwa katika Katiba hii au katika sheria nyingine yoyote. Kazi za Mahakama ya Rufani itakuwa kusikiliza na kutoa uamuzi juu ya kila rufaa inayoletwa mbele yake kutokana na hukumu au maamuzi ya Mahakama Kuu au Mahakama yoyote iliyopewa mamlaka maalum ya Mahakama Kuu*[91].

89 The Probate and Administration of Estates Act, Cap. 352 R. E 2002.
90 Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977.
91 Ibara ya 117 (3) Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977.



Utaratibu wa Kusajili Rufani katika Mahakama ya Rufani Awali ya yote ni vizuri kufahamu kuwa Mahakama ya Rufani inapokea rufani ambazo kimsingi zinajikita kwenye hoja za kisheria tu na sio mambo mengine. Taratibu za mashauri katika Mahakama hii ya juu kabisa nchini zinasimamiwa na Kanuni za Mahakama ya Rufani 2019 kama zilivyofanyiwa marekebisho kupitia Gazeti la Serikali[92]. Kwa lugha nyepesi utaratibu wa kukatia rufaa maamuzi au hukumu ya Mahakama Kuu ni kama ifuatavyo: -

i. Kuweka nia au kutoa taarifa ya kuwa na nia ya kukata rufani kwa mujibu wa kanuni ya 46 ambayo inasema: -

46.-(1) *where an application for a certificate or for leave is necessary,* ***it shall be made after the notice of appeal is lodged.*** (Msisitizo umeongezwa)

Kanuni ya 83[93] inaeleza kuwa mtu yeyote mwenye kutaka kukata rufaa katika Mahakama ya Rufani anapaswa kuweka nia ya kufanya hivyo kwa msajili wa Mahakama Kuu ndani ya siku thelathini (30). Mrufani/ mwenye nia ya kukata rufani atatakiwa kuonyesha ni sehemu gani anayotaka kukatia rufani katika hukumu au amri ya Mahakama Kuu.

Mwenye kutaka kukata rufani anatakiwa kupeleka wito kwa wahusika wote wa rufani husika ndani ya siku kumi na nne (14) baada ya kuweka nia ya kukata rufani. Angalia kanuni ya 84[94].

92 GN. No. 344 of 2019.
93 The Court of Appeal Rules, GN. No. 368 of 2009.
94 The Court of Appeal Rules, G.N. No. 368 of 2009.

ii. Baada ya kuweka nia ya kukata rufani, hatua inayofata ni kufanya maombi ya kibali cha kukata rufaa Mahakama ya Rufani. Maombi haya yanafanyika chini ya Sehemu ya V ya Kanuni za Mahakama ya Rufani[95]. Kanuni hii inamtaka mwenye kutaka kukata rufani apeleke maombi ya kibali katika Mahakama Kuu ndani ya siku thelathini (30) baada ya hukumu au maamuzi ya Mahakama Kuu. Katika hatua hii Mahakama Kuu itazingatia kama kuna hoja ya kisheria inayostahili kwenda kufanyiwa kazi na Mahakama ya Rufani.

Kanuni ya 45 ambayo imefanyiwa marekebisho na kanuni ya 6[96] kwa wepesi wa rejea inasema hivi: -

6. *The principal Rules are amended by deleting rule 45 and substituting for it the following new rule-*

*(a) Notwithstanding the provisions of rule 46(1), where an appeal lies with the leave of the High Court, application for leave may be made informally, when the decision against which it is desired to appeal is given, or by chamber summons according to the practice of the High Court,* ***within thirty days of the decision****;* (Msisitizo umeongezewa).

iii. Baada ya hatua hizo mrufani atatakiwa kusajili rufani yake katika masijala husika ya rufani katika Mahakama Kuu ndani ya siku sitini (60) tangu tarehe ya nia ya kukata rufani. Kanuni mahsusi kwa hatua hii ni kanuni ya 90[97] ambayo inasema: -

95 The Court of Appeal Rules, GN. No. 344 of 2019.
96 GN. No. 362 of 2017.
97 The Court of Appeal Rules G.N No. 368 of 2009 as Amended by GN. No. 362 of 2017.



90.-(1) *Subject to the provisions of Rule 128, an appeal shall be instituted by lodging in the appropriate registry, within sixty days of the date when the notice of appeal was lodged with –*

(a) *A memorandum of appeal in quintuplicate*;
(b) *The record of appeal in quintuplicate*;
(c) *Security for the costs of the appeal*,

*save that where an application for a copy of the proceedings in the High Court has been made within thirty days of the date of the decision against which it is desired to appeal, there shall, in computing the time within which the appeal is to be instituted be excluded such time as may be certified by the Registrar of the High Court as having been required for the preparation and delivery of that copy to the appellant.*

Ni muhimu sana kuzingatia muda na taratibu zinazoongoza Mahakama ya Rufani kwani ni tofauti sana na taratibu zinazotumika na Mahakama za chini yake. Kama ikitokea haujaridhika na maamuzi au amri ya Mahakama Kuu, weka nia ya kukata rufani ndani ya siku 30 tangu maamuzi ya Mahakama Kuu, kupeleka wito ndani ya siku 14 tangu tarehe ya kuweka nia ya kukata rufani Mahakama ya Rufani, kupeleka maombi ya kukata rufaa Mahakama ya Rufani ndani ya siku 30 baada ya maamuzi ya Mahakama Kuu na hatimaye kusajili rufaa katika masijala husika Mahakama Kuu ndani ya siku 60 baada ya kuweka nia.

## 2.24 Wajibu wa Mahakama Katika Kumthibitisha Mtekelezaji Wosia au Kuteua Msimamizi wa Mirathi

Endapo mtu ameomba kuthibitishwa kutekeleza wosia au kuteuliwa kuwa msimammizi wa mirathi, Mahakama ina wajibu ufuatao: -

i. Kuchunguza kwa makini na kujiridhisha kwamba mtu huyo anayeomba kuthibitishwa au kuteuliwa kuwa mtekelezaji au msimamizi wa mirathi, anayo maslahi katika mirathi hiyo;
ii. Kuwa ataweza kufanya kazi hiyo kwa makini na uaminifu mkubwa kulingana na matakwa ya marehemu (kama yanaweza kubainika) katika kusimamia mali hizo;
iii. Kusikiliza mapingamizi yoyote kama yapo na kuyatolea maamuzi;
iv. Kuhakikisha msimamizi au mtekeleza wosia anafunga hesabu za mali za marehemu na kuziwasilisha Mahakamani ndani ya miezi sita (6) au ndani ya muda uliopangwa na mahakama kwa jukumu hilo kama itakavyokuwa; na
v. Kuwa inaongoza na kusaidia wanufaika au warithi kuendesha mirathi kwa mujibu wa sheria na kanuni zilizopo ili haki itendeke na kuonekana kuwa imetendeka kwa watu wote.

Katika shauri la ***Naftal Joseph Kalalu vs Angela Mashirima***[98] Mahakama Kuu (Kimaro, J) ilisisitiza kuwa msimamizi wa mirathi hateuliwi ili anufaike na mali za marehemu. Mahakama kamwe isiruhusu kifo cha mtu kitumike kama fursa kwa watu baki zaidi ya warithi halali au wanufaika wanaostahili kurithi kwa mwamvuli wa kibaguzi wa mila. Katika shauri hili Mahakama Kuu ilitupilia mbali rufaa iliyofunguliwa na baba mzazi wa marehemu ambae alikuwa akipinga kuteuliwa kwa mjane/mke wa marehemu kuteuliwa kuwa msimamizi wa mirathi ya marehemu mume wake. Mahakama ya Wilaya ilikataa kutengua uteuzi uliofanywa na Mahakama ya Mwanzo hivyo ikapelekea kukata rufani ya pili Mahakama Kuu. Kwa kifupi Mahakama Kuu ilisema yafuatayo: -

98 PC Civil Appeal No. 145 OF 2001 at Dar es salaam



*"…An administrator is not appointed for converting the properties of the deceased into his/her own. The court should never allow the death of the deceased to be used as an opportunity for people other than the beneficiaries of the estate of the deceased to benefit from such estate, under pretext of discriminatory customary practices…"*

Kesi hii na nyingine nyingi inadhihirisha jinsi Mahakama inavyosimamia haki bila ya kujali mila na desturi ambazo kwa kiasi kikubwa zimekuwa zikitumika kama daraja kuwanyima wajane haki yao ya kurithi na kumiliki mali.

## 2.25 Miongozo ya Kimahakama

Pamoja na hayo uongozi wa Mahakama umekuwa ukisimamia kikamilifu Mahakama hasa za chini kwa kutoa miongozo mbalimbali ya kisera na maelekezo ili kuimarisha upatikanaji wa haki katika eneo la mirathi. Ifuatayo ni baadhi ya Sera na Miongozo iliyotolewa na uongozi wa Mahakama.

### 2.25.1 Waraka wa Jaji Kiongozi Na. 4/2005 Kuhusu Mashauri ya Mirathi

Waraka huu unaweka ukomo wa mazoea ya kutangaza tangazo la mirathi kwa muda siku 90. Waraka umehamasisha Mahakama kutoa matangazo ya mirathi kwa muda mfupi kadri inavyowezekana kwa kuzingatia aina ya mirathi husika, muhimu ni watu wote wanaohusika kupata taarifa. Jambo lingine linaloelekezwa na waraka huu ni Mahakama kutojihusisha na ugawaji wa mirathi. Waraka huu pia umewakumbusha mahakimu kukamilisha wajibu muhimu wa kufunga mashauri ya mirathi kwa mujibu wa sheria.

### 2.25.2 Waraka wa Jaji Kiongozi Na. 1/2007 Kuhusu Kesi za Madai: Amri za Muda, Kesi za Kiuchumi, Mirathi na zile za Watumishi Serikalini

Waraka huu wa Mhe. Jaji Kiongozi pamoja na mambo mengine umerejea na kusisitiza utekelezaji wa Waraka Na. 4/2005.

### 2.25.3 Chief Justice's Circular No. 1/2018 for District Delegates

Katika kuimarisha upatikanaji wa haki katika mashauri ya mirathi Mhe. Jaji Mkuu kupitia Waraka huu aliwateua Mahakimu wote wa Mahakama za Wilaya kuwa na uwezo wa kusikiliza mashauri ya mirathi, yaani District Deligate kuanzia tarehe 24/1/2018.

### 2.25.4 Waraka wa Msajili Mkuu Na. 1/2019 Kuhusu Ufungaji wa Mirathi na Utumaji wa Taarifa za Mashauri

Mhe. Msajili Mkuu kupitia Waraka huu amewakumbusha Mahakimu wote kuhakikisha mashauri yote ya mirathi yanafungwa kwa mujibu wa sheria. Wadaawa waelekezwe umuhimu wa kurudisha mahakamani hesabu kamili za mali za marehemu ili kufanikisha zoezi la ufungwaji wa mirathi.



# SURA YA TATU

# KUTUNZA MALI ZAKO NA WALE UWAPENDAO HATA BAADA YA KIFO

## 3. Wosia

Sheria ya Mirathi Sura ya 352 kama ilivyorejewa mwaka 2002 *(The Probate and Administration of Estate Act, Cap. 352 R. E 2002)* inatoa tafsiri ya mirathi kama ifuatavyo: -

***Will*** *means the legal declaration of the intentions of a testator with respect to his property, which he desires to be carried into effect after his death*[99].

Also;

**Will** *means the legal declaration of the intentions of a testator with respect to his property which he desires to be carried into effect after his death, and includes an oral will*[100].

Kwa tafsiri ya Kiswahili rahisi wosia ni tamko linalotolewa na mtu wakati wa uhai wake likilenga namna anavyopenda mali yake isimamiwe baada ya kifo chake. Pia Tangazo la Serikali Nambari 436 la mwaka 1963 ambalo linajumuisha sheria za kimila linatafsiri wosia kama *"kauli inayotolewa na mtu wakati wa uhai wake kwa hiari yake kuonesha nia yake jinsi gani angependa mali yake igawanywe baada ya kufa kwake"*.

99 Section 2 of Probate and Administration of Estate Act, Cap. 352 (R.E 2002).
100 Rule 2 of the Primary Courts (Administration of Estates) Rules G.N No. 49 of 1971.

### 3.1 Faida ya Wosia

Mtoa wosia anakuwa na nafasi ya kuamua na kuchagua nani awe msimamizi wa mirathi yake na kuhakikisha mali zake zinakwenda kwa warithi halali tu hivyo kuepusha migogoro, chuki na ugomvi miongoni mwa jamii yake. Pia wosia unamsaidia mtekelezaji/ msimamizi wa wosia kuwa na nafasi nzuri ya kutekeleza na kugawa mali za marehemu sanjari na matakwa ya marehemu mwenyewe. Kwa mapana yake wosia unasaidia kuokoa muda mwingi unaopotea kuteua msimamizi wa mirathi, hivyo watu kupata muda wa kutosha kufanya shughuli mbalimbali za kiuchumi na kuwezesha mahakama kufanya majukumu mengine.

### 3.2 Nani Anaweza Kutoa Wosia?

Kimsingi mtu yeyote anaweza kuandika au kutoa wosia. Isipokuwa kuna vigezo vya msingi vya kuzingatia ili wosia uwe halali na wenye nguvu za kisheria. Vigezo hivyo ni: -

i. Mtoa wosia lazima awe amefikisha umri wa mtu mzima, miaka kumi na nane[101]. Hata hivyo Kanuni ya 26[102] ya sheria ya wosia inatamka kuwa; *"Mtu aliye chini ya umri wa miaka; 21 hawezi kutoa wosia wa mdomo wala wosia uliyoandikwa"* Hivyo basi ni sahihi kusema mtu mzima katika muktadha wa kutoa wosia ni kwa mtu aliyefikisha umri wa miaka 21 au zaidi kwa mujibu wa sheria za kimila.

ii. Mtoa wosia lazima awe na akili timamu wakati anaandika wosia huo[103].

101 Section 23 of The Probate and Administration of Estate Act, Cap. 352 (R.E 2002).
102 Section 23 of The Probate and Administration of Estate Act, Cap. 352 (R.E 2002).
103 Section 23 of The Probate and Administration of Estate Act, Cap. 352 (R.E 2002).



iii. Mtoa wosia lazima atoe wosia kwa hiari yake mwenyewe bila vitisho au kulazimishwa na mtu yeyote.

iv. Mtoa wosia lazima atoe wosia mbele ya mashahidi angalau wawili watakaochaguliwa na mtoa wosia mwenyewe.

v. Wosia lazima uwe na tarehe ya siku ulioandikwa au kutolewa.

vi. Wosia lazima uwe na saini au alama ya dole gumba (kama wosia ni wa maandishi).

### 3.3 Aina za Wosia

Kuna aina kuu mbili za wosia nazo ni "Wosia wa Mdomo" *(Oral Will)* na "Wosia wa Maandishi*" (Written Will)*[104]. Pamoja na kuwa hizi ni aina mbili tofauti zote zina nguvu sawa kisheria kama zimetolewa kwa kuzingatia vigezo muhimu vya wosia kama vilivyobainishwa hapo juu.

#### 3.3.1 Wosia wa Mdomo

Wosia wa mdomo ushuhudiwe na mashahidi wasiopungua wanne (4) yaani, watu wa ukoo wasipungue wawili na watu baki wasipungue wawili. Ikumbukwe kuwa mashahidi wote hawa (maalum) huchaguliwa na mtoa wosia mwenyewe. Wosia wa mdomo unaweza kubadiliswa wakati wowote na mtoa wosia ama kwa kuwatumia mashahidi wale wale kama wapo au kwa kuchagua mashaidi wengine kadri atakavyoona inafaa isipokuwa tu azingatie idadi na aina. Pia ni muhimu kuzingatia zaidi kuwa, zaidi ya mashahidi maalum (yaani mashahidi wawili wa ukoo na watu wawili baki) mke au wake wa mtoa wosia waliopo nyumbani **lazima** washuhudie vile vile.

104 114 The Local Customary Law (Declaration) (No. 4) Order G.N No. 436 & 219 of 1967. Made under the Judicature and Application of Laws Act, Cap. 358

### 3.3.2 Wosia wa Maandishi

Wosia wa maandishi hautakiwi kuandikwa kwa na kalamu ya risasi (inayofutika), lazima uandikwe na kalamu ya wino (isiyofutika) na pia unaweza kupigwa chapa. Wosia wa aina hii lazima uandikwe tarehe ya siku mwenye kutoa wosia ameandika au kusababisha uandikwe. Wosia ulioandikwa lazima ushuhudiwe na mashahidi wawili (mmoja wa ukoo na mmoja mtu baki) ikiwa mwenye kutoa wosia anajua kusoma na kuandika. Endapo mwenye kutoa wosia hajui kusoma wala kuandika basi katika mazingira kama hayo lazima wosia ushuhudiwe na mashahidi wasiopungua wanne ambapo wawili wa ukoo na wawili watu baki.

Mwenyewe kutoa wosia lazima aweke sahihi yake katika wosia ulioandikwa ikiwa anajua kusoma na kuandika; na kama hajui kusoma wala kuandika basi aweke alama ya kidole chake cha gumba cha kulia katika wosia uliondikwa. Hatua inayofata ni mashahidi kushuhudia kwa kuweka sahihi zao kwenye wosia husika. Baada hapo wosia usiongezwe maneno yoyote zaidi ya kuhifadhiwa mahali salama. Wosia uliyoandikwa hauwezi kufutwa au kubadilishwa na wosia wa mdomo; lakini wosia wa mdomo unaweza kubadilishwa au kufutwa na wosia uliyoandikwa, isipokuwa lazima mashahidi wote walio hai na wanaoweza kupatikana walioshuhudia wosia wa mdomo wawepo.

### 3.4 Hatua za Kuchukua Pale Mashahidi wa Wosia wa Mdomo Wanapofariki kabla ya Aliyetoa Wosia

Ikiwa mashahidi wamekufa wote kabla ya mwenye kutoa wosia hajafa, wosia hauwezi kukubaliwa, na urithi utagawanyika kufuata mpango wa urithi usio na wosia. Hivyo mwenye kutoa wosia kama anataka kuusia mali yake, lazima atoe wosia mpya kwa kufata vigezo vyote vya wosia wa mdomo kama ilivoelezwa hapo awali.



### 3.5 Namna ya Kuandaa Wosia wa Maandishi

Kimsingi hakuna kanuni maalumu ya uandishi wa wosia wa aina hii isipokuwa tu unatakiwa kutaja mambo ya msingi ambayo mwenye kutoa wosia angependa yatekelezwe juu ya mali zake au mahali ambapo angependa azikwe baada ya kifo chake. Kimsingi wosia wa maandishi lazima uwe au uonyeshe vitu vifuatavyo: -

i. Jina la mwenye kutoa wosia;
ii. Jina la Msimamizi wa mirathi;
iii. Mali za mwenye kutoa wosia;
iv. Majina ya warithi;
v. Mgawanyo wa mali kwa warithi;
vi. Tarehe ya kuandika wosia;
vii. Saini ya mwenye kutoa wosia; na
viii. Majina na saini za mashahidi.

Endapo mwenye kutoa wosia anahusia sehemu tu ya mali aliyonayo kwa kujua au kwa kusahau, basi sehemu iliyobaki itagawanywa kwa kufuata masharti ya urithi usio na wosia. Hata hivyo, kama mtu anayeusiwa angestahili kurithi kufuata mpango wa urithi usio na wosia, mali anayoachiwa katika wosia itahesabiwa wakati wa kugawanywa baki[105].

105 Kanuni ya 29 ya sheria za wosia; The Local Customary Law (Declaration) (No. 4) Order G.N No. 436 & 219 of 1967. Made under the Judicature and Application of Laws Act, Cap. 358

## 3.6 Mfano wa Wosia wa Kuandika

1. *Huu ni wosia wangu wa mwisho mimi …………………..........……wa S.L.P……. ninaoutoa kwa hiari yangu na kwa akili zangu timamu kama ifuatavyo.*
2. *Namchagua/Ninawachagua ndg/bi….........…………………………….....wa S.L.P. ……………........... na simu…………………………………………… ambaye/ambao anaishi/wanaishi ………………….kuwa msimamizi wa mirathi yangu.*
3. *Nitakapokufa mwili wangu ukazikwe……………….Wilaya ya ……………….… Mkoa wa ……………………….*
4. *Mali zangu ni kama zifuatavyo: -*
   *(a) …………………......……………………….……...............................*
   *(b) Nina akaunti zifuatazo: - …………………………….................….......*
5. *Natamka kwamba mali zangu zote zinazohamishika na zisizohamishika zitamilikiwa na mke/ mume wangu aitwaye ……………………… iwapo atakuwa hai baadaya kufa kwangu.*
6. *Iwapo mke/ mume wangu aitwaye……………..……….... atafariki mapema kuliko mimi, mali zangu zitarithiwa katika mafungu yaliyo sawasawa/au katika mgawanyo ufuatao kwa watoto wangu wafuatao;*
   *a)……………………………………….wa SLP/Simu.....…………………......…*
   *b)…………………………………………wa SLP/Simu.........…………….....…*
   *c)…………………………………………wa SLP/Simu......……………….........*
   *d)…………………………………………wa SLP/Simu....…………......…....…*
   *Mimi………………nimeweka saini yangu hapa ……………….….....….*
   *Leo……….siku ya…………Mwezi wa…………….Mwaka……………......*
   *Saini /alama ya dole gumba ya mwosia………………………………......…*

   ***Shahidi wa Kwanza***
   *Jina: ……………………………………………………………….......….......*
   *Saini: ………………………….tarehe..…………………….……...............*
   *Anuani: ………………………………………………………………….........*
   *Kazi: ………………………………………………………….………...........*

   ***Shahidi wa Pili***
   *Jina: ………………………………………………………….……….......….*
   *Saini: ………………………………….tarehe……………………………......*
   *Anuani: ……………………………………………………………….….........*
   *Kazi: …………………………………………………………………..........*

   ***Mbele yangu***
   *Jina: ……………………………………………………..............................*
   *Wadhifa…………………………………………………...........................*
   *Saini: ……………………………………………………...........................*
   *Tarehe: ………………………………………………….........................*



## 3.7 Namna ya Kutunza Wosia wa Kuandika

Baada ya mwenye kutoa wosia kuandika na kuweka saini yake mbele ya mashahidi, na baada ya mashahidi kuweka saini zao namna inavyoonyeshwa kwenye mfano wa wosia hapo juu, hatua inayofata ni kuhifadhi wosia huo sehemu salama na ya kuaminika. Hivyo mwenye kutoa wosia anawaweza kuutunza wosia wake mahali popote palipo na ulinzi na usalama wa kutosha, ili kuepuka kubadilishwa au kughushiwa na watu wasio waamminifu. Sehemu zinazopendekezwa kwa ajili ya kutunza wosia ni pamoja na sehemu zifuatazo;

i. Ofisi ya Kabidhi Wasii Mkuu (RITA);
ii. Kwenye vyombo vya kutoa msaada wa kisheria;
iii. Asasi za kidini kama kanisa au msikiti;
iv. Katika Kampuni ya uwakili;
v. Mtu yeyote asiye mrithi katika wosia husika na ana sifa/ uwezo wa kutunza siri;
vi. Benki; au
vii. Mahakamani.

## 3.8 Namna ya Kubadili/ Kurekebisha Wosia Wako

Wosia haubadilishwi kwa njia yoyote ile zaidi ya wosia mwingine. Hivyo mwenye kutoa wosia endapo atapenda kufanya mabadiliko kwenye wosia wake wa awali ataandika wosia mwingine kwa kufata hatua zote muhimu za kutoa wosia kama zilivyoandikwa hapo awali. Hii inamaanisha kuwa mwenye kutoa wosia anayo nafasi ya kubadilisha wosia wake mara nyingi kipindi cha uhai wake kama anavyoona inafaa. Mwenye kutoa wosia anapofariki wosia ule wa mwisho kabisa ndio unakuwa na nguvu za kisheria.

## 3.9 Pale Inapotokea Mabadiliko ya Wosia Yanajulikana Baada ya Mahakama Kumthibitisha Msimamizi kwa Kuzingatia Wosia wa Zamani

Kwa kuwa mwenye kutoa wosia anao uwezo wa kubadili wosia wake mara kwa mara, hii inaweza kupelekea wosia wake wa mwisho kabisa kutojulikana kirahisi kama hakuwa na mpango mzuri wa utunzaji wake. Wosia wa mwisho kabisa unaotumika ni ule wenye tarehe ya mwisho kabisa ambao mwenye kutoa wosia ameandika enzi za uhai wake. Endapo ndugu wa marehemu watafata taratibu za msimamizi wa mirathi kuthibitishwa na mahakama kwa kutegemea wosia ambao sio wa mwisho, na Mahakama ikafanyia kazi wosia huo ikiamini ni wosia wa mwisho wa marehemu, na msimamizi akathibitishwa na Mahakama, usimamizi huo au mirathi hiyo inaweza kutenguliwa na Mahakama baada ya kuridhika kulikuwa na wosia mwingine wa mwisho wa marehemu. Baada ya kutengua Mahakama itathibitisha msimamizi mwingine kama kuna mabadiliko kwenye wosia wa mwisho wa marehemu. Pia mirathi kwa ujumla wake itazingatia wosia wa mwisho na sio kinyume cha hapo.

Kifungu cha 26 cha Sheria ya Mirathi na Usimamizi wa Mali ya Marehemu[106] kinaelezea juu ya mazingira ya namna hii. Kifungu kinasomeka hivi: -

S. 26 *"Where, after probate has been granted, a codicil of the will is propounded, probate may be granted of the codicil: Provided that where the codicil expressly or impliedly revokes the appointment of any executors to whom probate has been granted, such probate shall be revoked, and a new probate granted of the will and codicil together."*

106 The Probate and Administration of Estate Act, Cap. 352 R.E 2002



Kwa tafsiri isiyo rasmi ya Kiswahili, kifungu hiki kinasomeka hivi:-

"Pale inapogundulika uwepo wa wosia wa mwisho baada ya mirathi kuwa tayari imetolewa basi mirathi inaweza kutolewa upya kufatana na wosia huo wa mwisho.

Isipokuwa kama wosia huo wa mwisho unaeleza moja kwa moja au kwa namna nyingine kubadilisha msimamizi wa mirathi ambayo tayari amedhibitishwa na mahakama, mirathi hiyo itatenguliwa na mirathi mipya itathibitishwa na Mahakama kulingana na wosia huo wa mwisho na ule wa awali kwa pamoja."

### Mfano:

*Ndugu 'X' aliandika wosia wake tarehe 2/2/2018. Alifuata taratibu zote za kuandika wosia na akaupeleka benki kwa ajili ya kuutunza. Katika wosia huo alimteua mtoto wake wa kike 'Y' kuwa msimamizi wa mali zake na kuzigawanya kama alivyoelekeza kwenye wosia wake. Miezi sita baadae, (1/8/2018) ndugu 'X' aliandika wosia mwingine ambao pamoja na mambo mengine alimteua mke wake 'Z' kuwa msimamizi wa mirathi yake na akaamua kuupeleka RITA ili uhifadhiwe. Ilipofika tarehe 3/9/2018 ndugu 'X' alipata ajali ya gari na kupoteza maisha yake. Baada ya shuhuli za mazishi kukamailika ndugu zake waligundua marehemu 'X' aliacha wosia benki. Hivyo wakaendelea na hatua za kuomba uthibitisho wa Mahakama.*

*Mwishowe Mahakama ilisikiliza mirathi ya marehemu 'X' na kumthibitisha bi 'Y' kuwa msimamizi wa mali za marehemu baba yake. Baada ya 'Y' kupewa jukumu hilo la usimamizi na kuendelea na kazi hiyo ilijulikana kuwa marehemu 'X' aliacha wosia mwingine*

*katika ofisi za RITA. Hapa ndugu wanapaswa kurudi Mahakamani na wosia huo wa 1/8/2018 ambao ni wosia wa mwisho wa marehemu 'X'. Mahakama itatengua usimamizi wa 'Y' na kumdhibitisha bi 'Z' kuwa msimamizi mpya wa mirathi ya marehemu mume wake kama wosia wa mwisho unavyotamka. Sanjari na hayo, msimamizi 'Z' atasimamia mirathi na kuigawa kama unavyotamka wosia huo wa mwisho.*

### 3.10 Idadi ya Wosia Unaoweza Kuacha au Kuandika

Hakuna ukomo wa idadi ya wosia ambao mweye kuandika wosia anapashwa kuandika isipokuwa wosia pekee utakaozingatiwa na kuwa na nguvu za kisheria ni ule wosia wa mwisho kabisa wa marehemu. Hapa ndio umuhimu wa tarehe katika kila wosia unapoleta maana yake. Hivyo ni vema kuelewa kuwa mwenye kutoa wosia anayo nafasi kipindi cha uhai wake kufanya mabadiliko juu ya usimamizi na au mgawanyiko wa mali zake kadri aonavyo inafaa.

### 3.11 Jinsi ya Kurithisha kwa Wosia

Kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Haki na Matumizi ya Sheria mbali mbali, Sura ya 358[107], muusia anaweza kuusia mali yake yote bila kutaja kila kitu alichonacho wakati wa kufa kwake. Ikiwa muusia anapenda kuusia sehemu tu ya mali yake, basi sehemu iliyobaki itagawanywa kulingana na masharti ya urithi usio na wosia. Vifungu vya 28 na 29 katika nyongeza ya tatu (3)[108] ya Sheria za Wosia zinasema ifuatavyo: -

107 The Judicature and Application of Laws Act, Cap. 358 R.E 2002

108 The Local Customary Law (Declaration) (No. 4) Orders.



(28) *Mwenye kutoa wosia anaweza kuusia mali yake yote bila kutaja kila kitu atakachokuwa nacho wakati wa kufa kwake.*

(29) *Ikiwa mwenye kutoa wosia anausia sehemu tu ya mali atakayokuwa nayo, baki itagawanywa kufuata masharti ya urithi usio na wosia-isipokuwa kama mtu anayeusiwa angestahili kurithi kufuata mpango wa urithi usio na wosia, mali anayoachiwa katika wosia itahesabiwa wakati wa kugawanywa baki.*

Vifungu hivi vinahusika kwenye aina zote za wosia, yaani wa maandishi na wa mdomo. Hivyo ikitokea mwenye kutowa wosia hajataja mali zake zote sio kama wosia huo hauna maana yoyote, isipokuwa kama sheria inavyotamka hapo juu, mali zilizotajwa zitasimamiwa na kugawanywa kama vile alivyotaka marehemu na zile mali ambazo hazijatajwa zitagawanywa kwa mujibu wa mirathi ambayo haina wosia. Kwa mantiki hiyo wosia ambao haujataja mali zote za marehemu usihesabiwe kuwa ni batili, ila inaweza kuaminika kuwa mali alizotaja marehemu ndio zilikuwa zinagusa moyo wake sana au ndio alizokumbuka kwa haraka kabla ya kifo chake.

### 3.12 Mrithi Kunyimwa Urithi na Mwenye Kutoa Wosia

Sheria ya Usimamizi wa Haki na Matumizi ya Sheria mbalimbali, Sura ya 358[109] inatoa mazingira ambapo mwenye kutoa wosia anaweza kumnyima mrithi urithi wake ikiwa mwenye kutoa wosia amegundua kuwa mrithi: -

109 The Judicature and Application of Laws Act, Cap. 358 R.E 2002

i. Amezini na mke wa mtoa urithi;
ii. Amejaribu kumuua, amemshambulia, au amemdhuru vibaya mtoa urithi au mama mzazi wa mrithi;
iii. Bila sababu ya haki, hakumtunza mtoa wosia kutokana na njaa na ugonjwa;
iv. Ameharibu mali ya muusia, uharibifu wake utahesabika katika kukadiria kiwango cha urithi atakaostahili kupata.

Hata hivyo, mwenye kutoa wosia hawezi kutumia dini au sababu zingine zinazoashiria ubaguzi kama kigezo cha kumnyima mrithi urithi.

### Angalizo:

Ikitokea mwenye kutoa wosia amemnyima mrithi urithi wake, lazima ampe nafasi ya kujitetea mbele yake au Baraza la Ukoo, na lazima atoe sababu za kumnyima urithi. Mrithi baada ya kujua amenyimwa urithi akikaa kimya bila ya kujitetea mbele ya mtoa urithi au Baraza la Ukoo, hawezi tena baadaye kupinga huo wosia. Kama mrithi hakuwa na habari za kunyimwa kwake urithi, atatoa malalamiko yake kwenye Baraza la Ukoo ambalo litamsikiliza na linao uwezo wa kukubali au kukataa. Ikibainika kwamba mwenye kutoa wosia alimnyima mrithi urithi kimakosa, wosia utabadilishwa na urithi utagawanywa kulingana na urithi usio na wosia.



# SURA YA NNE
# ANAYESTAHILI KUWA MSIMAMIZI WA MIRATHI

## 4. Utangulizi

Hii ni hoja ya msingi sana kwa kuwa hata kama sheria ni nzuri, msimamizi au mtekeleza wosia akiwa mtu wa ovyo anaweza akafuja mali za marehemu wakati wa kukusanya na kuzigawa kwa warithi au wanufaika wa mali za marehemu. Kwa mantiki hiyo ni sahihi zaidi na salama msimamizi awe mtu mwadilifu na mwaminifu.

### 4.6 Nani awe Msimamizi wa Mali za Marehemu

Sheria zinazosimamia mirathi hapa nchini (sheria ya Serikali, sheria ya Mila na sheria ya Kiislamu) zinatamka kuwa **mtu yoyote mwenye uaminifu** na uadilifu anafaa kuwa msimamizi wa mirathi **bila kujalisha kuwa ni ndugu wa marehemu** au la. Kwa utaratibu uliopo baraza la ukoo ndio huteua msimamizi wa mirathi (ambaye baadae anathibitishwa na Mahakama), lakini iwapo linashindwa kuafikiana katika uteuzi basi mtu yoyote anaweza kwenda Mahakamani kuomba kuteuliwa na Mahakama.

Katika kitabu cha **Justice and Rule of Law in Tanzania**[110] waandishi wanasema kuwa: -

*"…Relatives of the deceased, are generally unsuitable to be appointed, because very often they tend to favour one section of the beneficiaries, and so it is better whenever it is possible to avoid them for this onerous task. After all the function of the administrator is merely to* ***distribute*** *the property of the deceased to the rightful* ***heirs in accordance with the law*** *and he has no room for maneuver…"*

110 Helen Kijo-Bisimba & Chris Maina Peter, Page 568

Waandishi wanamaanisha kuwa, ndugu wa marehemu sio watu sahihi sana wa kusimamia mirathi ya marehemu ndugu yao kwa sababu mara nyingi wanapendelea upande mmoja wa warithi, hivyo ni vizuri kuwaepuka kwa kadri inavyowezekana katika kutekeleza jukumu hili nyeti. Hata hivyo kazi ya msingi ya msimamizi ni kugawanya mali za marehemu kwa warithi halali kwa mujibu wa sheria na hana nafasi ya kufanya vinginevyo.

Ni vizuri jamii ielewe zaidi kuwa, mara nyingi mjane wa marehemu anakuwa muhanga katika mirathi kwa kuwa ndugu wa marehemu wanadhani kuwa asipoteuliwa kuwa msimamizi wa mirathi inamaanisha kuwa hana haki ya kurithi mali za marehemu mume wake. Dahana hii ni potofu na ya kulaaniwa kabisa. Kama ambavyo tumeona awali msimamizi hana haki ya kunufaika na mali za marehemu kama yeye mwenyewe sio mrithi wa mali za marehemu na pia kama kuna wosia na haujatamka nufaa yoyote kwa mtekeleza wosia. Hivyo kwa kuondoa utata **pale ndugu wa marehemu anapoteuliwa kuwa msimamizi wa mirathi ya marehemu ndugu yake hapati uhalali wa moja kwa moja kuwa mrithi au mnufaika.** Kazi kuu ya mtu anaeteuliwa kuwa msimamizi wa mirathi ni kukusanya na kugawa mali za marehemu kwa warithi halali kwa mujibu wa sheria, tena atafanya kazi hiyo kwa kujikana nafsi yake na kuweka mbele kwa uaminifu, maslahi ya warithi halali. Hivyo ni bayana kuwa kwa mujibu wa sheria mtu yeyote mwenye maslahi na mali za marehemu anaweza kuwa msimamizi wa mirathi, mradi tu awe mwaminifu na mwadilifu.

## 4.7 Haki za Warithi au Wanufaika wa Mirathi

Endapo warithi halali au wanufaika wa mali za marehemu watagundua au kubaini kuwa mtekelezaji wa wosia au msimamizi wa mirathi amesimamia au ametumia mirathi ya marehemu vibaya, waweza kuchukua hatua zifuatazo: -



i. Kulingana na fungu namba 49(1) (e) na (2) cha Sheria ya Mirathi na Usimamizi wa Mali za Marehemu, Sura ya 352[111] warithi, wanaweza kupeleka maombi Mahakamani *(zingatia lazima kupeleka maombi hayo katika Mahakama ile ile iliyomteua msimamizi wa mirathi au iliyomdhibitisha mtekeleza wosia)* wakiomba Mahakama kumfutia utekelezaji au usimamizi wa mirathi na hivyo kulazimika kurudisha Mahakamani hati zote zilizotolewa na mahakama kuthibitisha utekelezaji au usimamizi wake wa mirathi, ili Mahakama iweze kumchagua mtu mwingine,

ii. Ikitokea mazingira yanayoashiria kuwa mtekeleza wosia au msimamizi wa mirathi anakataa kurudisha Mahakamani hati zote zilizotolewa na Mahakama kuthibitisha utekelezaji au usimamizi wake wa mirathi, warithi wanaweza kumshitaki chini ya kifungu cha 51 (2)[112], na akikutwa na hatia anaweza kutozwa faini au kifungo kisichozidi miezi mitatu au vyote faini na kifungo, Kifungu kinasomeka ifuatavyo;

> 51. (2) *If such person wilfully and without sufficient cause omits so to deliver up the probate or letters, he commits an offence and on conviction is liable to a fine not exceeding two thousand shillings or to imprisonment for a term not exceeding three months, or to both such fine and imprisonment.*

111 The Probate and Administration of Estates Act, Cap. 352 R. E 2002.

112 The Probate and Administration of Estates Act, Cap. 352 R. E 2002.

iii. Kama mtekelezaji huyo na/au msimamizi wa mirathi amesimamia vibaya au ameharibu mali ya marehemu, warithi au mtu yeyote mwenye maslahi na usimamizi huo, anaweza kumfikisha Mahakamani akimtaka alipe fidia kwa uharibifu au hasara aliyosababisha.

### 4.8 Maombi ya Kupewa Usimamizi wa Muda wa Mirathi

Kuna mazingira ambayo mara nyingine yanaleta changamoto kwawarithi na wanufaika kabla Mahakama haijamteua msimamizi wa mirathi au kumthibitisha mtekeleza wosia. Hivyo mazingira ya namna hiyo yasipelekee ndugu kufarakana au kugombana. Ili kuondoa hali ya mifarakano au kuharibika, kupotea au kuibiwa kwa mali za marehemu kabla ya uteuzi, na wakati maombi ya kuomba usimamizi au utekelezaji wa wosia yanaendelea Mahakamani, mwombaji anaweza kuioomba Mahakama impe usimamizi wa mirathi wa muda. Msimamizi aliyepewa usimamizi wa muda anakuwa na majukumu sawa na msimamizi aliyethibitishwa au kuteuliwa na Mahakama ya kukusanya na kutunza mali ya marehemu, isipokuwa hawezi kugawa mali ya marehemu kwa warithi. Lengo la kutoa usimamizi huu wa muda, ni kuwawezesha waweze kutimiza majukumu ya haraka kama vile matunzo kwa watoto na mjane.

Sehemu ya III ya Sheria ya Mirathi[113] kuanzia kifungu cha 10 hadi 17 vinaelezea jinsi ya kutunza au kulinda mali za marehemu wakati maombi ya usimamizi wa mirathi au uthibitishwaji wa mtekeleza wosia ukiendelea Mahakamani.

113 The Probate and Administration of Estates Act, Cap. 352 R. E 2002.



### 4.9 Mwangalizi wa Mali za Marehemu kabla ya Uteuzi

Kifungu cha 10 cha Sheria ya Mirathi kinatoa mwanya kwa Kabithi Wasii Mkuu au mtu yoyote anayedai haki kwenye mali ya mtu aliyefariki na kuacha mali yake nchini Tanzania au mtu mwenye kusimamia au mwenye mamlaka juu ya hiyo mali wakati wa kifo cha marehemu, kufanya maombi Mahakamani kuonesha kuwa kuna hatari ya hiyo mali kuteketezwa hivyo ateuliwe kuisimamia hiyo mali kadri Mahakama itakavyoona inafaa hadi hapo atakapoteuliwa msimamizi. Kifungu hicho cha sheria kinasomeka ifuatavyo: -

*10. Where any person dies leaving property within Tanzania, the court may, if it appears on the application of the Administrator-General or of any person claiming to be interested in such property, or having the custody or control thereof at the time of the death of the deceased, or being at such time an attorney of the deceased, that there is danger that such property may be wasted, appoint the Administrator-General or such other person as the court thinks fit, to be a receiver of such property pending a grant of probate or letters of administration.*

Kufuatia maombi ya uangalizi wa muda wa mali ya marehemu kwa mujibu wa kifungu cha 10 kama tulivyoona hapo juu, Mahakama inaweza kumteua mtu yoyote chini ya kifungu hicho, kuagiza kuuzwa kwa mali yote au sehemu ya hiyo mali kama itaonekana kwa kufanya hivyo itakuwa kwa maslahi ya mali za marehemu.

Kwa upande mwingine kuna mazingira ambapo mwagalizi wa muda wa mali za marehemu anakosa ushirikiano au anakwamishwa na watu wenye hila katika kusimamia hiyo mali kwa muda akisubiri uteuzi wa Mahakama. Sheria haijafumbia macho vitendo vya namna hii kwani inatoa adhabu chini ya kifungu cha 13. Sheria

inafafanua kuwa, mtu yoyote asiye na mamlaka kamili akihamisha au kujaribu kuhamisha mali ya marehemu au sehemu ya mali hiyo ambayo ipo chini ya mwangalizi wa muda, au akiiharibu, kuficha au akikataa kuonyesha kwa mwangalizi anafanya kosa na ikidhibitika atahukumiwa tozo ya shilingi 5,000/= au kwenda jela kwa muda usiozidi miezi sita au vyote viwili. Kwa wepesi wa rejea kifungu cha 13 kinanukuliwa hapa chini;

*13. Any person who, without lawful authority, removes or attempts to remove from Tanzania any portion of the property of which a receiver has been appointed under section 10, or destroys, conceals, or refuses to yield up the same to the receiver, commits an offence and on conviction is liable to a fine not exceeding five thousand shillings or to imprisonment for a term not exceeding six months or to both such fine and imprisonment.*

Ikizingatiwa kuwa maombi ya usimamizi/ uangalizi wa muda chini ya kifungu cha 10 cha Sheria ya Mirathi kama tulivyoona hapo awali yanafanyika kwa nia njema ya kulinda mali za marehemu, kwa kuzingatia hilo sheria inamlinda zaidi mwangalizi wa muda aliyeteuliwa na Mahakama kwa kuzuia asishitakiwe kwa jambo alilofanya au analokusudia juu ya mali za marehemu au pale anapojaribu kutumia mamlaka aliyopewa na Mahakama. Hata hivyo kama kuna mtu ana hoja au malalamiko juu ya hatua zilizochukuliwa na mwangalizi wa muda anatakiwa afanye maombi Mahakamani kwa mwongozo wa Mahakama. Kifungu cha 14 kinahusika na kinasomeka kama ifuatavyo: -



*14. No suit shall be brought against a receiver appointed under section 10 in relation to anything done or intended to be done by him in respect of the property of the deceased in exercise or intended exercise of the powers vested in him; but any person aggrieved by anything so done, or intended to be done, may apply to the court for directions in the matter, and the court may make such order as is just.*

Hata hivyo kuna mazingira ambapo mwangalizi wa muda anachukua jukumu la kufanya mambo mbalimbali juu ya mali za marehemu hata kabla ya kuthibitishwa au kuteuliwa na Mahakama. Ikitokea kuwa mtu yeyote amechukua jukumu la kusimamia mali za marehemu na kuchukua hatua juu ya mali hizo ili kuzihifadhi, kuzilinda ama vinginevyo kwa kufanya hivyo sheria inamuhesabu kuwa mwangalizi au msimamizi anayewajibika kwa makosa yake mwenyewe. Hii inamaanisha kuwa kama mtu ameamua kusimamia au kuangalia mali za marehemu kabla ya kupata kibali cha Mahakama cha kufanya hivyo, atawajibika kwa kosa au makosa yoyote atakayoyafanya juu ya mali za marehemu. Vifungu vya 16 na 17 vya Sheria ya Mirathi vinafafanua haya.

*16. A person who intermeddles with the estate of the deceased or does any other act which belongs to the office of executor, while there is no rightful executor or administrator in existence, thereby makes himself an executor of his own wrong:*

*Provided that–*

*(a)* *intermeddling with the goods of the deceased for the purpose of preserving them or providing for his funeral or for the immediate necessities of his family or property; or*

*(b)* *dealing in the ordinary course of business with goods of the deceased received from another; or*

*(c)* *action by an administrative officer under section 14 of the Administrator-General (Powers and Functions) Act *;*

*(d)* *action by a receiver appointed under section 10, does not make an executor of his own wrong.*

*(e)* *Where a person has so acted as to become an executor of his own wrong, he is answerable to the rightful executor or administrator, or to any legatee or creditor of the deceased, to the extent of the assets which have come into his hands, after deducting payments made to the rightful executor or administrator, and payments made in due course of administration.*

Ni muhimu kuzingatia kuwa mtu anayechagua kusimamia au kuangalia mali za marehemu kabla ya kupewa jukumu hilo na Mahakama lazima afanye hivyo kwa uaminifu na uadilifu. Na kigezo cha msingi cha kufanya hivyo ni kutetea, kulinda au kuhifadhi mali ya marehemu isipotee au anafanya hivyo kwa maslahi ya mali za marehemu. Vinginevyo mtu huyo atawajibika kwa makosa atakayofanya juu ya mali za marehemu.



# SURA YA TANO

# WAJIBU WA MSIMAMIZI WA MIRATHI NA TARATIBU ZA KISHERIA PALE ANAPOSHINDWA KUKAMILISHA WAJIBU WAKE

## 5. Utangulizi.

Wajibu wa Mahakama wa msingi kabisa ni kumteua msimamizi wa mirathi au mtekeleza wosia. Baada ya hapa wajibu wa Mahakama unabaki kuhakikisha aliyeteuliwa au kuthibitishwa anafanya kazi yake kwa misingi ya sheria. Kwa upande mwingine msimamizi au mtekeleza wosia anabaki na jukumu lake la kugawanya mali zote za marehemu kwa warithi halali. Mahakama haihusiki wala haina jukumu la kugawa mali za marehemu.

### 5.1 Majukumu ya Msimamizi wa Mirathi na Mtekeleza Wosia

Jedwali la tano la Sheria ya Mahakama za Mahakimu na kifungu cha 99 cha Sheria ya Mirathi na Usimamizi wa Mali za Marehemu, kinaeleza kuwa mtekelezaji au msimamizi wa mirathi ya marehemu ndiye mwakilishi wa marehemu kisheria na mali zote za marehemu ziko mikononi mwake. Hivyo mtekelezaji au msimamizi wa mirathi ya marehemu anao wajibu na majukumu kama inavyoainishwa hapa chini;

i. Kukusanya mali zote za marehemu kwa uaminifu na uangalifu mkubwa;

ii. Kupeleka Mahakamani orodha ya mali ya marehemu au madeni alivyoweza kukusanya;

iii. Kupokea na kulipa madeni halali ya marehemu, ikiwani pamoja na kulipa gharama zitokanazo na usimamizi;

iv. Kugawanya mali iliyobaki kwa warithi halali wa marehemu;
v. Kuifahamisha Mahakama juu ya ugawaji wa mali za marehemu ulivyofanyika na kama umekamilika au muda zaidi uongezwe ili aweze kukamilisha ugawaji wa mali ya marehemu na kuiwezesha Mahakama kufunga jalada la mirathi;
vi. Mtekelezaji wa wosia au msimamizi wa mirathi anaweza kushitaki au kushitakiwa katika shauri lolote jipya au ambalo marehemu ama alianzisha au lilifunguliwa dhidi yake;
vii. Kadri atakavyoona inafaa, na kadiri ilivyo kwa masilahi ya warithi, mtekelezaji au msimamizi wa mirathi, anaweza kuuza mali inayohamishika kutoka katika mirathi ya marehemu; na
viii. Mtekelezaji wa wosia au msimamizi wa mirathi hawezi kutengeneza au kupata faida kutokana na usimamizi wake, isipokuwa kama wosia umesema hivyo.

Pia sehemu ya XI ya Sheria ya Mirathi na Usimamizi wa Mali za Marehemu[114] kuanzia kifungu cha 99 hadi 113 vinaelezea nguvu na wajibu wa msimamizi wa mirathi au mtekeleza wosia. Ni vema kukumbuka kuwa sheria hii ya Mirathi haitumiki katika Mahakama ya Mwanzo ila inaanzia ngazi ya Mahakama ya wilaya.

### 5.2 Hatua za Kuchukua Pale Msimamizi Anapokosea Kutekeleza Wajibu Wake

Kama tulivyoona hapo awali, msimamizi anayo majukumu ya msingi na ya kisheria katika kusimamia mirathi. Sheria pia inamtaka msimamizi kuhakikisha anatekeleza lengo hilo kwa haki na uaminifu mkubwa. Hivyo ni kosa kisheria kwa msimamizi kutapanya mali za marehemu, kudhulumu, kujinufaisha au kudanganya juu ya mali za marehemu. Ili kuweka ufanisi sheria inamtaka msimamizi kukusanya mali za marehemu kwa Fomu maalumu, Kugawanya mali za marehemu kwa kutumia Fomu

114 The Probate and Administration of Estates Act, Cap. 352 R. E 2002



maalumu na hatimae Kuweka hesabu sawa na kupeleka mahesabu Mahakamani, pia kwa kutumia Fomu maalumu. Kama msimamizi hafanyi haya kwa kuzingatia muda na taratibu zilizopo, kutakuwa na mianya ya kufuja mali za marehemu hivyo kutenda kosa kisheria.

Kifungu cha 138[115] cha Sheria ya Mirathi na Usimamizi wa Mali za Marehemu kinasema kuwa kama msimamizi au mtekeleza wosia atakayetapanya mali za marehemu au kuharibu mali au kupoteza mali atawajibika kufidia uharibifu au upotevu huo. Pia sheria inamtaka msimamizi wa mirathi au mtekeleza wosia kuwajibika kwa hasara yoyote itakayotokana na uzembe katika kutekeleza jukumu hilo la usimamizi au utekelezaji wosia[116] Kwa wepesi wa rejea vifungu hivyo vinaeleza ifuatavyo: -

*138. When an executor or administrator misapplies the estate of the deceased, or subjects it to loss or damage, he is liable to make good the loss or damage so occasioned.*

*139. When an executor or administrator occasions a loss to the estate by neglecting to get in any part of the property of the deceased, he is liable to make good the amount.*

Sheria haijamuacha salama msimamizi wa mirathi au mtekeleza wosia kwa makosa yatakayofanywa kinyume na matakwa ya Sheria ya Usimamizi wa Mirathi na Usimamizi wa Mali za Marehemu kwani inatoa adhabu. Kifungu cha 157[117] kinatamka kuwa mtu yoyote atakaefanya kosa kinyume na Sheria ya Mirathi na Usimamizi wa Mali za Marehemu atakuwa na hatia ya kulipa tozo isiyozidi shilingi 2,000/= (elfu mbili) za kitanzania au kifungo kisichozidi miezi sita (6) au vyote kwa pamoja. Kifungu kinasomeka hivi: -

115 The Probate and Administration of Estates Act, Cap. 352 R.E 2002.
116 The Probate and Administration of Estates Act, Cap. 352 R.E 2002.
117 The Probate and Administration of Estates Act, Cap. 352 R.E 2002.

157. *Any person who commits an offence against this Act shall on conviction be liable to a fine not exceeding two thousand shillings or to imprisonment for a period not exceeding six months or to both such fine and such imprisonment.*

Kwa msingi huo kucheza na mali za marehemu ukiwa kwenye nafasi ya msimamizi wa mirathi au mtekeleza wosia au namna nyingine ni kosa linaloadhibiwa kwa kifungo. Hivyo ni wajibu wa watu wanaodahi haki kwenye mali za marehemu kuhakikisha msimamizi wa mirathi au mtekeleza wosia anafanya majukumu hayo kwa mujibu wa sheria. Kama kuna ujanja ujanja, ulaghai au uongo unaingizwa kwenye mirathi malalamiko hayo yapelekwe Mahakamani ambapo yatasikilizwa na uamuzi kutolewa kwa haki.

### 5.3 Utaratibu wa Usimamizi Pale Aliyeteuliwa au Kuthibitishwa na Mahakama Anapofariki Kabla ya Kumaliza Kazi Yake

Kuna wakati inatokea msimamizi wa mirathi au mtekeleza wosia anafariki dunia kabla ya kumaliza jukumu lake la kusimamia na kugawanya mali za marehemu. Tukumbuke kuwa jukumu la msingi la msimamizi wa mirathi au mtekeleza wosia ni kukusanya mali za marehemu, kulipa madeni, kugawanya mali za marehemu kwa warithi halali na wanufaika wote na mwisho kurudisha hesabu Mahakamani. Kwa ufafanuzi, msimamizi wa mirathi wakati akitekeleza jukumu lake hilo huwa kimantiki anaingia kwenye viatu vya marehemu na kugawa mali za marehemu kama vile ni marehemu mwenyewe anazigawa. Ikumbukwe kuwa msimamizi sio mnufaika kwa vile tu ni msimamizi, ni lazima awe ametamkwa kwenye wosia au ni mmojawapo wa warithi. Hivyo, kwa kuwa msimamizi wa wosia au mtekeleza wosia ni mtu mzima na ikitokea amefariki, ile kazi yake ya usimamizi nayo inakufa na badala yake atateuliwa mtu mwingine wa kumalizia usimamizi wa mali ambazo alikuwa anazisimamia kabla ya kifo chake.



Endapo msimamizi wa mirathi au mtekeleza wosia alikuwa peke yake na akafariki kabla ya kumaliza kazi yake, basi Mahakama itateua mtu mwingine kukamilisha kazi hiyo. Na ikiwa wasimamizi walikuwa zaidi ya mmoja, na mmoja wapo akafariki wale wanaobaki wataendelea na usimamizi hadi kukamilisha kazi hiyo.

**Mfano:**

a). *Iwapo **X** anasimamia mirathi ya **Y** na kabla ya kumaliza kazi yake kikamilifu na kupeleka hesabu Mahakamani **X** nae anafariki dunia. Ikitokea hivyo warithi au wale wanaodai haki juu ya mali za **Y** wataenda Mahakamani kuiomba Mahakama iteue msimamizi mwingine amalizie kazi iliyoanzwa na **X** katika kusimamia mirathi ya **Y**. Hivyo kama Mahakama itamteua **B** kuendelea* kusimamia *mirathi ya **Y**, basi **B** ataendelea kama vile ni **X** anafanya kazi hiyo. Na hata kama kuna mashauri ya madai ambayo **X** alikuwa anayasimamia kwa niaba ya **Y** basi **B** ataingia na kuendelea. Kwa upande mwingine pia warithi wa **X** na wote wanaodahi haki juu ya mali zake watafanya maombi Mahakamani ya kuteuliwa kusimamia mirathi ya **X**.*

b). *Kama wasimamizi wa mirathi au watekeleza wosia walikuwa zaidi ya mmoja yaani **A**, **B** na **C** wanasimamia kwa pamoja mirathi ya **D** na ikitokea kuwa **B** amefariki dunia, basi **A** na **C** wataendelea kusimamia kwa pamoja mitathi ya **D** hadi kukamilisha kama wataishi hadi kumaliza kazi hiyo.*

Kifungu cha 45 na 46 cha Sheria ya Mirathi na Usimamizi wa Mali za Marehemu vinaeleza juu ya mazingira haya na nini kifanyike kama tulivyoona. Vifungu hivyo ni kama tunavyoona hapa chini: -

45. *Where probate or letters of administration have been granted to more than one executor or administrator and one of them dies, the representation of the estate administered shall, in the absence of any direction in the will or grant accrue to the surviving executor or executors or administrator or administrators.*

46. *On the death of a sole or sole surviving executor who has proved the will or of a sole or sole surviving administrator, letters of administration may be granted in respect of that part of the estate not fully administered, and in granting such letters of administration the court shall apply the same provisions as apply to original grants:*

*Provided that where one or more executors have proved the will or letters of administration with the will annexed have been issued, the court may grant letters of administration under this section without citing an executor who has not proved the will.*

## 5.4 Utaratibu Pale Mtekeleza Wosia Anafariki

### 5.4.1 Kabla ya Aliyetoa Wosia

Katika mazingira haya mwenye kutoa wosia anayo nafasi ya kubadilisha msimamizi na kuweka mwingine aliye hai. Hii inafanyika kwa ama kuandika wosia mwingine au ukandika kiambatanisho kwenye wosia ambao tayari upo na kumtaja msimamizi mwingine kwa kuwa yule wa awali amefariki dunia.

Pia ni vizuri wakati wa kuandika wosia kufikiria mazingira kama hayo na kuweka kipengele kinachoonyesha kuwa msimamizi wa mali zangu atakuwa **"X"** na kama **"X"** hataishi kusimamia mirathi yangu basi isimamiwe na **"Y"**.



### 5.4.2 Kama Mtekeleza Wosia anafariki kwa Pamoja na Aliyetoa Wosia

Mazingira ya namna hii hutokea kwa nadra sana lakini ni jambo linaloweza kutokea hivyo hatuna budi kulizingatia. Kimsingi mantiki ya wosia kama ambavyo tumeona awali ni kwa yule mwenye kutoa wosia kuhakikisha mali zake zinasimamiwa na mtu aliyemchagua yeye na kuzigawanya kwa warithi wake kwa utaratibu alioupanga yeye mwenyewe. Hata hivyo matamanio haya ya mwenye kutoa wosia yanaweza kuingia doa endapo mwenye kutoa wosia atafariki kwa wakati mmoja na yule aliyemtaja/ kutamka kuwa msimamizi wa mirathi yake. Mfano kwa ajali, au watafariki kwa kufuatana ndani ya muda mfupi sana au kwa namna nyingine yoyote.

Hivyo basi katika mazingira hayo, kama mweneye kutoa wosia alimtaja msimamizi mmoja tu kwenye wosia wake na aliyetajwa hakuishi hata kuweza kuianza kazi hiyo basi warithi au wale wanaodahi haki juu ya mali za marehemu watapeleka maombi Mahakamani kuomba uteuzi wa mtu mwingine ili atekeleze wosia kama ulivyoachwa na marehemu.

# SURA YA SITA

# ULIPAJI WA FEDHA ZA MIRATHI KUPITIA MAHAKAMA

## 6. Utangulizi

Kwenye sura zilizotangulia tumeona jinsi sheria zinazoongoza mashauri ya mirathi zinapelekea yule mwenye haki ya kurithi kupata haki yake. Hata hivyo sheria hizi zote hazielezi wazi wazi njia na taratibu ya kuwalipa wanufaika fedha zitokanazo na mali za marehemu. Hivyo utaratibu unaotumika na Mahakama baada ya uteuzi wa msimamizi wa mirathi ni kutoa barua ya kufungu akaunti zote za fedha za marehemu na kuelekeza fedha zote zitumwe kwenye akaunti maalumu ya Mahakama (mirathi) iliyopo Benki Kuu[118]. Baada ya fedha hizo kuhamishiwa kwenye akaunti ya mahakama, mgao wa fedha hizo kwenda kwenye akaunti za warithi, utafatia kutoka akaunti ya mahakama baada ya uhakiki wa nyaraka zote muhimu zinazothibitisha uhalali wa malipo. Hatua hii ya mwisho ya uhakiki na ulipaji hufanywa na kitengo cha mirathi kilichopo Mahakama ya Rufani kwa mkoa wa Dar es salaam. Kwenye mikoa mingine utaratibu haupishani na huu wa Dar es salaam, fedha zinaingia kwenye akaunti ya mahakama katika mkoa husika. Na malipo hufanyika katika mahakama ya mkoa baada ya uhakiki[119].

118 Benki Kuu ya Tanzania.

119 Utaratibu huu umeanza kutumika kuanzia tarehe 1/7/2020. Kabla ya hapo ofisi za Hazina ndogo zilizopo mikoani zilikuwa zinatumika. Akaunti hizi maalumu zinasimamiwa na watendaji wa mahakama kwa kila mkoa.



## 6.1 Utaratibu wa Malipo

Malipo yanayofanyika kupitia Mahakama yana mlolongo wake ambapo baada ya msimamizi wa mirathi kuteuliwa na Mahakama atapewa barua ya utambulisho kwenda kwenye taasisi za kifedha, mifuko ya hifadhi ya jamii na sehemu ambapo marehemu alikuwa anafanya kazi. Taasisi za fedha zitafunga akaunti ya marehemu na kuhamishia fedha zote kwenye akaunti ya Mirathi ya Mahakama.

Msimamizi wa mirathi atapashwa kupeleka orodha na mchanganuo wa malipo kwa wanufaika katika Mahakama iliyofanya uteuzi. Kila mnufaika anatakiwa kuwa na akaunti ya benki ambayo itahakikiwa kwa Fomu maalumu zinazopatikana mahakamani[120]. Mchanganuo utapokelewa kwenye ofisi ya mhasibu wa Mahakama na akijiridhisha kuwa, ni kweli fedha za marehemu zimeingizwa kwenye akaunti ya mirathi ya Mahakama[121]. Pia atajiridhisha orodha ya warithi waliopo kwenye mchanganuo kama ni sawa na warithi waliopo kwenye nakala ya hukumu. Baada ya hapo ataandaa vocha ya malipo na kuipeleka kwa hakimu mfawidhi kwa ajili ya kusaini na kuruhusu mchakato wa malipo uendelee.

Endapo mirathi imesikilizwa Mahakama ya Mwanzo basi jalada litachukuliwa na kupelekwa Mahakama ya Wilaya ili kufanyiwa uhakiki na mhasibu wa Wilaya na kupitishwa na hakimu mfawidhi wa Wilaya ili kwenda Kitengo cha Mirathi kilichopo Mahakama ya Rufani (kwa mkoa wa Dar es salaam)[122].

120 Vendor Form.

121 Uhakiki unafanywa kwa kuangalia taarifa ya benki *(Bank Statement)* ya akaunti ya mirathi ya Mahakama. Uhakiki huu huchukua muda kulingana na upatikanaji wa taarifa ya benki kwa mhasibu wa mahakama husika.

122 Kwa upande wa mikoa mingine jalada likihakikiwa ngazi ya wilaya litapelekwa mahakama ya mkoa ili kufanya uhakiki wa mwisho na kufanya malipo kwa warithi kama hakutakuwa na dosari yoyote.

Kimsingi, Kitengo cha Mirathi kinapitia na kinakagua upya kila nyaraka na majina ya wanufaika kama yapo sawa sawa na yanavyoonekana kwenye hukumu. Endapo kuna dosari kwenye moja wapo ya majina ya wanufaika jalada litarudishwa Mahakama iliyomteua msimamizi wa mirathi kwa ajili ya kurekebisha dosari hiyo. Mfano, kwenye kusikiliza maombi ya uteuzi mnufaika au mrithi ametaja jina lake kuwa ni TINA MAIKO alafu taarifa zake za kibenki zinasoma CHIRISTINA MICHAEL malipo yatakwama kwa sababu majina hayafanani. Wanufaika wazingatie kutaja majina yao rasmi kama yalivyo kwenye vitambulisho vyao vya benki au taifa. Baada ya ukaguzi na uhakiki hatua za malipo kwa mfumo wa serikali hufata na fedha zinalipwa moja kwa moja kwenye akaunti za wanufaika.

### 6.2 Mambo ya Kuzingatia

Kuepusha ucheleweshaji wa malipo kwa wakati ni vema kuhakikisha kila kitu kimeandikwa kwa usahihi kabisa. Hii ni pamoja na majina kamili ya mleta maombi, majina kamili ya warithi na akaunti sahihi za benki. Pia kuzingatia kutunza nyaraka zote mahali salama ili kila kitu kinapohitajika kipatikane kwa wakati na kikiwa kwenye hali nzuri.



# SURA YA SABA

# MAPENDEKEZO NA HITIMISHO

## 7. Mapendekezo

Kwa kiasi kikubwa katika nchi yetu watu wengi wanahudumiwa na Mahakama za Mwanzo kwenye mashauri ya mirathi. Mahakama hii ndio iliyopo karibu zaidi na mwananchi na pia uendeshaji wake haufungwi sana na taratibu za kisheria ili kuirahisishia kufanya kazi zake na kutoa haki kwa wakati kwa wadaawa. Tafiti mbalimbali ambazo zimefanyika[123] zinabainisha kuwa wanachi wana uelewa mdogo sana wa mambo ya mirathi na taratibu za kimahakama katika kufungua na kusimamia mirathi.

Hivyo basi kwa kuongeza ufanisi wa Mahakama na kukuza kiwango cha wananchi kuridhika na huduma za Mahakama inapendekezwa mambo yafuatayo yazingatiwe: -

### 7.1 Elimu Ya Mirathi kwa njia mbalimbali

Elimu ni njia inayotumika kwa umri wowote kuwajuza watu kitu ambacho hawakielewi au kuwaongezea uelewa. Katika eneo hili la mirathi imethibitika kupitia tafti kuwa wananchi wanahitaji kupatiwa elimu ya mara kwa mara na njia zifuatazo zinapendekezwa zichukuliwe na mamlaka husika.

#### 7.1.1 Elimu ya Mirathi Shule za Sekondari

Kutoa elimu ya mirathi kuanzia elimu ya sekondari inaweza kutafsiriwa kuwa sawa na kuelimisha taifa zima. Somo la mirathi likiwa sehemu ya mitaala ya shule zetu baada ya muda mchache kila atakayepita shule atapata maarifa ya kusimamia mirathi na kupata picha hata nini maana ya mirathi. Kwa sehemu kubwa watu wanakuja kukumbana na haya majukumu ya mirathi wakati wapo

123 Report on Strengthening Beneficiaries' Access to Deceased's Estates in Tanzania (March, 2019) and Taarifa ya Utafiti Juu ya Ushughulikiaji wa Mirathi Dar es Salaam (April, 2019)

kwenye majonzi na mazingira magumu. Tena mtu hafahamu lolote juu ya mirathi, hivyo katika mazingira ya majonzi na mazingira ya msiba inamuwia vigumu kufahamu haki na wajibu wake katika kuendesha mirathi ya mpendwa wake. Naamini hali itakuwa tofauti kabisa kama elimu hii itatolewa katika shule za sekondari ambapo ufahamu wa wanafunzi katika ngazi hiyo tayari umeimarika na pia watoto wengi wanapata nafasi ya kufika elimu ya sekondari tofauti na elimu ya chuo kikuu.

Thamani nyingine ya kutoa elimu hii katika mashule yetu ni kwamba wanafunzi watakuwa mabalozi wazuri kwa kupeleka elimu hiyo katika kila kaya wanapoishi nchini. Hivyo itafikia wakati kila nyumba kuna angalau mwanafunzi mmoja ambaye amesoma na kupata maarifa ya mirathi ambae atakuwa mjumbe au mwalimu kwa wanandugu wake katika kaya yao. Kwa kuzingatia mtiririko huu wa kufundisha kwenye kaya kupitia wanafunzi baada ya muda kila mwananchi atakuwa na uelewa juu ya elimu ya mirathi hivyo kupunguza au kuondoa kabisa changamoto nyingi zilizopo kwa sasa. Mfano; dhana ya kuwa msimamizi wa mirathi lazima awe ndugu wa marehemu ambayo bado inatumika kwenye jamii itapungua sana baada ya elimu kupatikana. Hii itasaidia kupunguza mashauri mengi yaliyo Mahakamani yanayotokana na usimamizi wa mirathi usiofata taratibu.

### 7.1.2 Dawati la Elimu ya Mirathi ngazi ya Mahakama ya Mwanzo na Serikali ya Mtaa

Changamoto za mirathi zinagusa kila kaya nchini, kwa kuwa kifo kinapita kwa kila anayeishi kwa wakati wake. Kwa kuwa kwa sasa hakuna mpango rasmi wa kusaidia wananchi kuondoka na kadhia hii inayogusa moja kwa moja hisia za mtu, ingefaa sana kuweka dawati la kutoa elimu kwa wananchi juu ya mirathi na taratibu zake. Dawati hili lisogezwe karibu kabisa na wananchi kupitia Mahakama za Mwanzo na ofisi za Serikali za Mitaa kwa kushirikiana na Tawala za Mikoa na Serikali ya Mitaa (TAMISEMI). Wakati mwananchi anakwenda Mahakamani kufungua mirathi ingefaa yeye pamoja na hao wanaodai haki juu ya mali za marehemu kupata elimu juu ya mirathi na nini hasa wajibu wa msimamizi wa mirathi.

Dawati hili la elimu ya mirathi liratibiwe na Mahakama moja kwa moja kwa ushirikiano na Shule ya Sheria (Law School) ili kupata mpango endelevu wa wanafunzi kupitia hatua ya kutoa elimu kwa jamii kama kozi ya lazima. Mahakama itakuwa na nafasi ya kusimamia ubora na kutoa alama za ufaulu kwa wanafunzi kupitia Mahakama za Mwanzo.

### 7.1.3 Elimu kupitia vipindi vya Radio na Runinga

Kwenye vituo mbalimbali vya Radio na Runinga kuna vipindi vingi sana vya elimu kwa umma vinavyorushwa bila malipo. Mahakama kupitia kitengo chake cha habari na elimu kwa umma kingeratibu vipindi hivi nchi nzima kwa kupitia kanda za Mahakama Kuu. Kila kanda iwe na mpango wake wa mwaka mzima na kuteua wataalaamu wa kwenda kutoa elimu kwa wananchi. Hii ingesaidia sana hasa kwa kutumia vituo vya habari vya maeneo husika *(local stations)* kwa kutoa elimu kwenye eneo hilo. Kila kanda ikipanga vipindi vyake kwa mwaka mzima inamaanisha Mahakama itakuwa hewani nchi nzima kwa mwaka mzima ikitoa elimu juu ya taratibu za mirathi. Zoezi hili likifanyika kwa miaka miwili mfululizo hakuna sikio ambalo litakuwa halijasikia habari hii. Kwa mpango huu umma utaelimika, taratibu za kufungua mirathi kwa kiasi kikubwa zitazingatiwa hivyo kupunguza mashauri yasiyo ya lazima Mahakamani. Kwa kufanya hivyo pia tutakuwa tumepunguza msongamano wa mashauri na mizigo mizito inayowalemea Majaji na Mahakimu wetu nchini.

### 7.1.4 Elimu ya Mirathi kupitia Mitandao ya Kijamii

Hivi karibuni tumeshuhudia mapinduzi ya mawasiliano na dunia kwa kiasi kikubwa ikiegamia kwenye mitandao ya kijamii. Taaarifa nyingi na biashara kubwa sana zinafanyika kwenye mitandao ya kijamii. Hii inaashiria kuwa mitandao hii ina watumiaji wengi na inatembelewa na maelfu ya watu kila wakati. Mahakama isibaki nyuma katika hili kupitia kurasa zake za tweeter, facebook, istergram na mingineyo kuwe na vipeperushi au njia rahisi ya kufikisha ujumbe kwa umma juu ya mirathi na taratibu za kimahakama katika kutekeleza wajibu wa kusimamia na kugawa mirathi ya marehemu kwa warithi halali. Mahakama ifikirie pia kuanzisha *application* (App) ambayo mwananchi anaweza kuipakua kwenye simu yake na kupata taarifa mbalimbali za kimahakama ikiwemo pamoja na mirathi.

## 7.2 Mafunzo ya Mara kwa Mara kwa Majaji na Mahakimu juu ya Mirathi

Tafiti zinazofanyika Mahakamani zinaonesha kuwa kati ya mashauri 1,057 ya mirathi yanayosikilizwa hadi msimamizi kuteuliwa au kuthibitishwa na Mahakama, ni mashauri 75 (7%) pekee ambayo majalada yake yalifungwa kwa mujibu wa sheria na taratibu[124]. Hii inamaanisha kuwa mashauri mengi hayafikii hatua ya kufunga jalada kwa kuwa ama wasimamizi hawaleti hesabu za mali za marehemu kwa wakati au kwa kuwa Mahakama haisimamii kikamilifu ukamilishaji wa hatua ya ufungaji wa mashauri ya mirathi.

Ni vema kuwa na utaratibu wa kuwapa semina elekezi Majaji na Mahakimu ambao ndio huongoza mashauri haya ili kuhakikisha kila mtu anayeteuliwa au kudhibitishwa na Mahakama kuwa msimamizi wa mirathi anafunga hesabu za mali za marehemu kwa wakati unaopasa. Ni lazima Mahakama kupitia Majaji na Mahakimu

124 Report on Strengthening Beneficiaries' Access to Deceased's Estates in Tanzania (March, 2019).



kuhakikisha kuwa shauri la mirathi halihesabiki kuwa limeisha kabla ya hesabu ya mali za marehemu kufungwa na msimamizi wa mirathi au mtekeleza wosia. Semina za mara kwa mara kwa Majaji na Mahakimu zitasaidia kukabiliana na changamoto mpya zinazoibuka kwenye mashauri ya mirathi hivyo kusaidia kufikia lengo kuu la Mahakama la kutoa haki kwa wakati.

## 7.3 Matangazo ya Vifo

Kama tulivyoona awali ili shauri la mirathi lisikilizwe Mahakamani ni lazima litangazwe kwenye magazeti au mbao za matangazo za Mahakama au sehemu za wazi zenye mkusanyiko wa watu. Dhumuni la msingi ni kufikisha taarifa kwa jamii ili kama kuna yeyote mwenye maslahi na mali za marehemu aweze kufika mahakamani na kusikilizwa. Kwa maeneo ya vijijini na hata mijini wigo wa kutangaza mashauri ya vifo ungetanuliwa ili pamoja na matangazo mengine mashauri haya pia yatangazwe kwenye nyumba za ibada ambapo marehemu alikuwa akiabudu enzi za uhai wake. Hii itasaidia taarifa kufika kwa watu wengi zaidi na kuepusha migogoro mingi mahakamani.

## 7.4 Ulipaji wa Fedha za Mirathi kupitia Akaunti ya Mahakama

Mlolongo wa ulipaji wa fedha za mirathi kwa wanufaika unahusisha hatua na nyaraka nyingi sana. Hii inaleta urasimu na kufungua mianya ya rushwa. Utafiti uliofanywa na Mahakama[125] umebaini kuwa wastani wa hatua 34 tofauti hupitiwa na wanufaika/ wasimamizi wa mirathi hadi malipo yafanyike. Mahakama inashauriwa kurejea mfumo hu una kuona namna bora ya kuwahudumia warithi ili wapate haki zao kwa wakati.

125 Ripoti ya Utaratibu wa Malipo ya Fedha za Mirathi Inayopitia Mahakamani, Novemba, 2020

## 7.5 Hitimisho

Kifo ni tukio litakalompata kila mwanadamu anayeishi sasa. Hivyo kila mtu anayeishi sasa kuna siku atatoweka kwenye uso wa dunia, yaani atafariki. Baada ya kufariki na mazishi kukamilika, taratibu za mirathi kwa mali ambazo ulijaliwa kumiliki enzi za uhai wako zitaendelea. Hivyo kila anayeishi kifo chake kitapelekea shauri la mirathi ili kutunza na/ au kugawanya mali zake kwa warithi halali aliowaacha duniani.

Kwa muktadha huo basi ni vema kila mtu anayeishi leo hii afanye mpango bora wa kusimamia mali zake hata baada ya kifo kwa kuandaa wosia wa kutunza mali na kuzigawa kwa warithi halali kama atakavyopendezwa. Kwa kupitia wosia kama tulivyoona awali, mwenye kutoa wosia atachagua yeye mwenyewe mtu wa kusimamia mali zake hivyo atakuwa amepunguza kwa kiasi kikubwa mgongano wa nani asimamie.

Pia kwa kupitia wosia mwenye kutoa wosia atagawanya mali zake kwa uwiano anaopenda yeye hivyo kuondoa mivutano na chuki kwenye familia na jamii kwa ujumla.

Tukumbuke zaidi kuwa msimamizi wa mirathi au mtekeleza wosia si lazima awe mrithi bali anaweza kuwa mtu yeyote mwaminifu na mwadilifu. Majukumu yake makubwa na ya msingi ni kukusanya mali za marehemu, kulipa madeni na kisha kugawa bakaa kwa warithi halali. Msimamizi hapaswi kupata au kudai faida yoyote katika kutekeleza wajibu huo labda tu kama yeye mwenyewe ni sehemu ya warithi walioachwa na marehemu.

Tuzingatie kuwa mjane anayo haki ya kurithi mali za marehemu mume wake bila ya vikwazo vyovyote. Tena ana haki ya kuwa msimamizi wa mali za marehemu kwani kimsingi yeye ni sehemu ya mali hizo kwa kuwa kwa namna moja au nyingine alichangia upatikanaje wake. Kwa kuondoa sintofahamu, mjane hata kama



alikuwa mama wa nyumbani hiyo pekee ni mchango tosha wa kuwa na stahili katika mali zilizopatikana wakati wa ndoa yake na marehemu mume wake. Jamii lazima ielewe kuwa mjane anayo haki kisheria kurithi na kumiliki mali za marehemu mume wake.

Watoto ni kundi jingine linalonyanyasika katika kutekeleza taratibu za mirathi. Mara nyingi tunashuhudia marehemu anaacha watoto wadogo na wanaishia kuwa watoto wa mitaani huku mali zilizoachwa na wazazi wao zikifujwa na watu ambao sio waaminifu. HILI NI KOSA KISHERIA na tusisite kuwafichua watu wote wenye tabia hizi. Pamoja na mambo mengine msimamizi wa mirathi au mtekeleza wosia anapaswa kutumia hekima katika kukusanya na kugawa mali za marehemu akizingatia umri wa watoto na mahitaji muhimu ya watoto kama elimu, matibabu, mavazi na malazi. Watoto wasikose shule au mahali pa kulala kwa kuwa nyumba iliyopo inatakiwa iuzwe na kugawana fedha. Lazima kuangalia uwezekano wa kupata kipato endelevu katika mali zilizoachwa na marehemu ili kusaidia elimu na malezi ya watoto. Hii ndio italeta tija kuliko kukimbilia kuuza na kugawana fedha.

Hali ilivyo kwa sasa inaonesha kuwa mashauri ya mirathi yenye changamoto kubwa ni yale ambayo hayana wosia pamoja na yale ambayo mwanaume anakuwa na watoto na wanawake kadhaa. Mirathi ya namna hii kwa kiasi kikubwa hakuna maelewano baina ya wanawake wanaobaki, pia watoto wa mama mmoja hawaelewani na wa mama mwingine kitu ambacho kinapelekea chuki na uhasama mkubwa katika kugombea mali za marehemu. Ingefaa kuishi maisha yatakayoepuka changamoto kama hizi hasa kwa wanaume kuepuka kuzaa bila kuzingatia taratibu za kidini na maadili mema.

Kwa kuhitimisha, ni vema kila mtu akaanda wosia wake na kuuhifadhi mahali salama kama tulivyoona kwenye kitabu hiki. Pia kila mmoja ahamasishe ndugu, jamaa na rafiki kuandika wosia wake ili kuwaacha salama wale tuwapendao na pia mali tulizochuma ziwasaidie katika maisha yao na sio kuwafarakanisha.



# VIELELEZO

## A: Fomu I

FOMU MIRATHI - 1

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA TANZANIA**

Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya ……………………………….

Kituo cha………………………… Mkoa ……………………..

Usimamizi wa mirathi Na……………./20………………

| Na. | Jina | Uhusiano |
|---|---|---|
| 1 | | |
| 2 | | |
| 3 | | |
| 4 | | |
| 5 | | |
| 6 | | |
| 7 | | |
| 8 | | |
| 9 | | |
| 10 | | |

6. Maombi haya yamewasilishwa na mimi kama (eleza sababu za kuomba)…………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………
……………………………………………iwapo marehemu alitunga wosia na mwombaji si aliyetajwa msimamizi katika wosia wala msimamizi aliyetajwa hajatoa idhini yake, eleza jina na anwani ya msimamizi huyo na kwa nini idhini yake haijapatikana
……………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………

7. Naamini kuwa mali yote itakayokuwa katika mirathi hii itakuwa na thamani ya: (eleza aina ya mali na thamani yake).

……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………

8. Marehemu alipofariki alikuwa mkazi wa (taja mahali)………………………………… na/au alikuwa na mali katika eneo la mamlaka ya mahakama hii.

9. Marehemu alikuwa (eleza kabila lake)……………………………….. na alikuwa mfuasi wa dini ya ……………………………………………….

10. Hakuna daawa lolote la kuthibitisha wosia wala kuomba kumteua msimamizi wala jambo lingine linalohusika na mirathi ya marehemu huyo ambalo limeanzishwa mbele ya mahakama au mamlaka yoyote wala katika mahakama nyingine nje ya Tanzania.

Ameapishwa/amethibitishwa na kutiwa saini ya huyo

…………………………………………………………………

anayejulikana kwangu/aliyejulishwa kwangu ……….  ………………………….. Sahihi ya mwombaji

…………………………………………………………

Mbele yangu ……………………………………….

Tarehe……….Mwezi………….Mwaka………….

Saini ya Hakimu…………………………………….

# B: Fomu II

FOMU MIRATHI - 2

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA TANZANIA**

Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya …………………………………..

Kituo cha…………….............. Mkoa ………….........

Usimamizi wa mirathi Na……………../20………………

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**

MAREHEMU...........................................................WA.......................................

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA**

NA...........................................................................

**TANGAZO**

**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe............................Mwezi………………………..Mwaka……………… kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**

Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.

*Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa.

*Marehemu hakuacha wosia

*Futa isiyohusika

Imetolewa leo Tarehe...........Mwezi………Mwaka………..........

…………………………………………..

**HAKIMU**



# C: Fomu IV

FOMU MIRATHI - 4

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA TANZANIA**

| | | | |
|---|---|---|---|
| Katika Mahakama ya Mwanzo | …………………… | Kituo cha | … … … … … . |
| Wilaya ya | …………………… | Mkoa | … … … … … . |
| Usimamizi wa Mirathi Na. | …………………… | Mwaka | … … … … … . |

**HATI YA USIMAMIZI WA MIRATHI**

**(Kanuni ya 7(2) Kanuni za Usimamizi wa Mirathi katika Mahakama za Mwanzo)**

Mirathi Na ………………….. Mwaka …………………….

Marehemu ………………………………………………..

Mwombaji ………………………………………………..

Mnamo Tarehe ……. Mwezi ………………. Mwaka …………………….

Bwana/Bibi......................................................................................... ameteuliwa/wameteuliwa kuwa Msimamizi/Wasimamizi wa Mirathi ya Marehemu .................................................................... aliyefariki mnamo Tarehe .............Mwezi…..........Mwaka………....... akiwa ameahidi kusimamia

Mimi/Sisi ................................................................ naapa/tunaapa/nathibitisha/tunathibitisha kuwa;

1) Nitasimamia/tutasimamia kwa wema na uaminifu Mirathi ya Marehemu aliyetajwa hapo juu.
2) Nitalipa/tutalipa madeni yake ya haki na kugawa baki ya mirathi yake kwa mujibu wa Sheria.
3) Nitaweka/tutaweka hesabu kamili na za kweli za mali yote ya mirathi ya marehemu pamoja na jinsi nitakavyogawanya/tutakavyogawanya.
4) Nitaonyesha/tutaonyesha hesabu hizo mbele ya Mahakama ndani ya miezi minne.
5) Nitahakikisha/tutahakikisha ninatimiza/tunatimiza majukumu yangu/yetu ili Mahakama ifunge Mirathi ndani ya miezi minne baada ya kuteuliwa au baada ya hapo kama Mahakama itaongeza muda

Imetiwa sahihi leo Tarehe......................Mwezi.....................Mwaka…...........

.....................................

**MSIMAMIZI I**

.....................................

**MSIMAMIZI II**

## D: Fomu V

FOMU MIRATHI - 5

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA TANZANIA**

Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya ……………………………………..

Kituo cha…………………............ Mkoa ………………..........

Usimamizi wa mirathi Na……………../20………………

Shauri la Mirathi Na…………Mwaka …………….
Msimamizi ………………………………………………………………
Marehemu………………………………………………………………

**ORODHA YA MALI**

(Kanuni ya 10 (1) Kanuni za Usimamizi wa Mirathi katika Mahakama za Mwanzo)

Tarehe ya kuteuliwa ........................................................................

1. Orodha ya mali

a) Mali isiyohamishika (Mfano ardhi/nyumba)

| Na | Aina ya mali | Eneo ilipo | Thamani |
|---|---|---|---|
| 1. | Nyumba | | |
| 2. | Ardhi | | |

b) Mali inayohamishika (mfano, mafao, hisa, mifugo, fedha na vyombo vya usafiri)

| Na | Aina ya mali | Eneo ilipo | Thamani |
|---|---|---|---|
| 1. | Mafao | | |
| 2. | Hisa | | |
| 3. | Fedha | | |

(Kama kuna mali zingine ambazo hazijaanishwa hapa au hazitoshi kwenye nafasi hii, unaweza jaza karatasi nyingine)

.

2. Madeni:



| NaJina | Madeni anayodai | Madeni anayodaiwa | Thamani |
|---|---|---|---|
| 1. | | | |
| 2. | | | |

3. Gharama nyinginezo:

| Maelezo | Thamani |
|---|---|
| 1. Gharama za kuzikwa | …………………… |
| 2. Vitu vilivyowekwa rehani | …………………… |
| 3. Madeni mengine | …………………… |
| 4. Gharama za matibabu | …………………… |
| 5. Gharama za usimamizi | …………………… |

Jumla ya thamani ya mali za kugawa kwa warithi …………………………..

Mimi ............................................................................... msimamizi wa mirathi ya marehemu................................................................................ nathibitisha kuwa

orodha hii ya mali ya mirathi hiyo ni kweli kadri nijuavyo, niambiwavyo na nisadikivyo.
Ameapishwa/amethibitishwa na kutiwa saini ya huyo

………………………………………………………

anayejulikana kwangu/aliyejulishwa kwangu ……………………..

……………………………………………………… Saini ya Msimamizi

Mbele yangu leo Tarehe ……. Mwezi ………………

Mwaka ………………

..........................................

HAKIMU

# E: Fomu VI

FOMU MIRATHI - 6

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

MAHAKAMA YA TANZANIA

Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya ........................................

Kituo cha............................... .......................... Mkoa ..........................

Usimamizi wa mirathi Na................/20.................

Msimamizi ....................................................................
Marehemu......................................................................
Tarehe ya kuteuliwa..........................................................

**HESABU ZA MIRATHI**

(Kanuni ya 10(1) na (2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)

Mapato:

1.Thamani ya mirathi katika orodha ya mali (kwa mujibu wa fomu Na.V)..........................

2.Thamani ya fedha zilizopatikana .................................................................................... Jumla ya Thamani.......................................................................................................

Matumizi:

1. Gharama za kuzika....................................................................................
2. Madeni yaliyolipwa..................................................................................
3. Gharama za Usimamizi.............................................................................
4. Thamani ya mirathi tayari kugawiwa..............................................................

Mirathi hiyo ya Shilingi ..................................................................imegawanywa (au itagawanywa) kwa warithi halali tajwa hapa chini kwa utaratibu ufuatao:

| Na. | JINA | ANA HAKI GANI | KIASI KWA ASILIMIA% |
|---|---|---|---|
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |

Mimi…..................................................ambaye ni msimamizi wa Mirathi, nathibitisha kuwa nimegawa na kuwasilisha hesabu ya Mirathi kikamilifu na kwa uaminifu kwa kadri nijuavyo.

Ameapishwa /amethibitishwa na kutiwa saini ya huyo..............

Anayejulikana kwangu/aliyejulishwa kwangu na.........................
..............................................................................Sahihi ya Msimamizi

Mbele yangu.............................................

Tarehe.............Mwezi..........Mwaka............

Sahihi ya Hakimu..................................….



# F: Form

## APPOINTMENT OF AN ADMINISTRATOR OF A SMALL ESTATE

THE PROBATE AND ADMINISTRATION ESTATES ACT

(CAP. 352)

(Section 6)

In the Court of
Administration of the estate of ..................................................................
On this .................................. day of .......................................... 20........ ,
was appointed administrator of the estate (or of the assets specified below)

of the late .................................. who died on the ..............................
day of .................................. , 20........
having undertaken well and faithfully to administer the estate as hereunder mentioned.

(A copy of the Will of the deceased is annexed and the estate is to be administered accordingly.)

....................................

**(Signature and designation of officer holding the Court)**

I (or we) hereby solemnly and sincerely declare that I (or we) will well and faithfully administer the estate of the above-named deceased person, paying his just debts and distributing the residue of his estate according to law, and will keep true and fully detailed accounts of all and singular the estate and effects of the deceased and of my (or our) dealing with the property and will produce them to the said court whenever required.

Dated this ......................... day of .................................... , 20........

**(Signature of administrator)**



## G: Form No. 76

### APPLICATION FOR APPOINTMENT OF ADMINISTRATOR OF SMALL ESTATE

**(Rule 85)**

**(Title)**

I, C.D., of ....................................................................................

hereby

apply to be appointed administrator of the estate of A.B., late of

deceased, who died at..............on the day of 20
..........................

2. The writing hereunto annexed and marked "A" is the last Will and testament of the said A.B. (or, if the deceased made an oral

   Will: The said deceased made an oral Will the terms whereof and the circumstances in which it was made are stated in the

   affidavit, of ..........................................................................

   dated the ........................ day of........................ 20........ annexed hereto and marked "A" or, if

   the deceased died intestate: The said deceased died intestate and due and diligent search has been made for a Will but none has been found).

3. The said deceased left surviving him the following relatives

(give names and addresses of the relatives).

..........................................................................................

..........................................................................................

..........................................................................................

..........................................................................................

..........................................................................................

4. This application is made by me as (state the right or interest of the applicant in the estate. If the application is made by someone other than the person named in the Will, if any, as executor, and no consent of such person is available, a paragraph should be added here giving name an address of such executor and reasons why consent has not been obtained).

..........................................................................................

..........................................................................................

5. I believe that the gross assets which are likely to come to my hands will be (state amount and nature of the assets).

..........................................................................................

..........................................................................................

..........................................................................................

6. The said deceased at the time of his death had a fixed place of abode at ..................................................................................................... .............................and/or property within the jurisdiction of this court.



7. The said deceased was ......................................................(state nationality) and professed the ...............................religion.

8. No proceedings for the grant of probate or letters of administration or appointment of an administrator or otherwise for the administration of the estate of the said deceased have been commenced before any Court or authority whether inside Tanzania or outside it.

Dated at .................. this ............. day of......................... 20........

Signature of the Advocate (if any)

(Signature of the Applicant)

## H: Form 78

### APPOINTMENT OF ADMINISTRATOR OF SMALL ESTATE

(Section 76, Rule 93)

**(Title)**

BE IT KNOWN that C.D., of ....................................is hereby appointed administrator of the estate of A.B., late of .................. deceased, who died at ...................................................on the ......................... day of ......................... 20........ the said C.D., having undertaken well and faithfully to administer the said estate.

A copy of the Will (or a statement of the contents of the oral Will) executed (made) by the said deceased is annexed hereto.
day of Given under my hand and the seal of the Court this

......................... 20...............

..................

Resident Magistrate



## I: Form No. 62

### CAVEAT

(Section 58, Rule 82)

**(Title)**

Let nothing be done in the matter of the estate of A.B., deceased,

who died at .................................... on the .............................. day of

20 ...........................without due notice to .. ......................................

(name of the caveator) whose address of service is ..................
...............

(state address of service).

Dated at.............this ..................... day of..................... 20.........

(To be signed by the caveator or his advocate)

MTENDAJI MKUU WA MAHAKAMA YA TANZANIA,
MAKUTANO YA OHIO NA KIVUKONI FRONT,
S.L.P 9004, 1409 DAR ES SALAAM
**SIMU NAMBARI:** +255 22 212 3897 | 211 1586,
**NUKUSHI:** +255 22 211 6654,
**BARUA PEPE:** info@judiciary.go.tz,
**Tovuti:** www. judiciary.go.tz,

tanzaniajudiciary.blogspot.com @judiciarytz The judiciary of Tanzania judiciary Tanzania